# MLANGO
WA
# HISTORIA

(SWAHILI HISTORICAL READER).

SOCIETY FOR PROMOTING CHRISTIAN KNOWLEDGE,
LONDON: NORTHUMBERLAND AVENUE, W.C.
1894.

Digitized by Google

WIDENER LIBRARY
HX 5112 X

SWAHILI HISTORICAL READER.

MLANGO WA HISTORIA.

S·P·C·K

Google

2 235. 75. 107

HARVARD COLLEGE LIBRARY
THE GIFT OF
FRIENDS OF THE LIBRARY
Oct 28, 1929

*Richard Clay & Sons, Limited, London & Bungay.*

Digitized by Google

# PREFACE.

The *Mlango wa Historia* is meant to serve as a text-book for instruction in the history of the earth and its inhabitants up to the epoch of the Incarnation. From that point the "Church History" (*Mambo ya Kanisa*) may serve for a continuation of the course.

A considerable number of these Readings have already appeared in *Mambo na Hadithi*, and *Visa vya Kale*.

A. C. M.

*Zanzibar*, 1892.

---

## KWA MWALIMU.

Ukisomesha watoto walio wadogo, afathali uanze penyi Sura vii., Ndoto za Nabii Daniele.

Digitized by Google

# FAHIRISI

## YA MAMBO YALIYOMO KITABUNI HUMU.


| | | UKARASA |
|---|---|---|
| 1. | HISTORIA ... ... ... ... ... | 9 |
| 2. | MILANGO YA MAARIFA ... ... ... | 10 |
| 3. | DUNIA ... ... ... .. ... | 12 |
| 4. | WAANA ADAMU WA KWANZA ... ... | 17 |
| 5. | MIANZO YA MATAIFA YA KALE ... ... | 19 |
| 6. | MAMBO YA MATAIFA MAKUU YA ZAMANI ... | 24 |
| 7. | NDOTO ZA NABII DANIELE ... ... ... | 26 |
| 8. | INCHI YA BABEL ... ... ... ... | 31 |
| 9. | SULTANI NEBUKADNEZAR ... ... ... | 33 |
| 10. | SULTANI KURO NA BABEL ... ... ... | 35 |
| 11. | SULTANI KURO ALIVYOKUFA ... ... | 38 |
| 12. | SULTANI DARIO ... ... ... ... | 39 |
| 13. | VITA YA DARIO NA WASIKUTHI ... ... | 40 |
| 14. | SULTANI DARIO NA WAYONANI ... ... | 41 |
| 15. | SULTANI SERKISI NA WAYAHUDI ... ... | 44 |
| 16. | VITA YA SERKISI NA WAYONANI ... ... | 48 |
| 17. | HABARI ZA WAYONANI ... ... ... | 51 |
| 18. | HADITHI YA ULISSE ... ... ... | 52 |
| 19. | KROISO NA SOLON ... ... ... ... | 70 |
| 20. | LUKURGO NA WASIPARTA ... ... ... | 73 |


Digitized by Google

| | | UKARASA |
|---|---|---|
| 21. | MASULTANI WA WAYONANI ... ... ... | 76 |
| 22. | WAATENE ... ... ... ... ... | 78 |
| 23. | SOKRATI ... ... ... ... ... | 81 |
| 24. | ISKANDER ... ... ... ... ... | 84 |
| 25. | VISA VYA ISKANDER ... ... ... | 88 |
| 26. | ANTIOKO EPIFANI ... ... ... ... | 91 |
| 27. | YUDA MAKABIO ... ... ... ... | 94 |
| 28. | WARUMI ... ... ... ... ... | 98 |
| 29. | HADITHI YA ROMULO NA REMO ... ... | 99 |
| 30. | WARUMI WA KWANZA ... ... ... | 100 |
| 31. | MJI NA MWILI ... ... ... ... | 102 |
| 32. | KORIOLANO ... ... ... ... ... | 104 |
| 33. | MAFABIO ... ... ... ... ... | 105 |
| 34. | VITA YA WATURUSKI ... ... ... | 107 |
| 35. | KINKINATO ... ... ... ... ... | 107 |
| 36. | WAGALLO NA MABATA ... ... ... | 108 |
| 37. | VITA YA WASAMINITI .. ... ... | 109 |
| 38. | PURRO MYONANI ... ... ... ... | 112 |
| 39. | TABIA YA WARUMI ... ... ... ... | 112 |
| 40. | NJIA NA MAKOLONIA ... ... ... | 113 |
| 41. | KARTAGO ... ... ... ... ... | 115 |
| 42. | REGULO ... ... ... ... ... | 115 |
| 43. | HANIBALI ... ... ... ... ... | 117 |
| 44. | MILKI YA WARUMI ... ... ... ... | 120 |
| 45. | MAKAISARI ... ... ... ... ... | 120 |
| 46. | WAYAHUDI ... ... ... ... ... | 124 |
| 47. | YERUSALEMI ... ... ... ... | 126 |

Digitized by Google

# TARIHI ZA KUKUMBUKWA.


| B.C. | | UKARASA |
|---|---|---|
| 588. | NEBUKADNEZAR ALIPOUTEKA YERUSALEMI ... ... ... ... | 27 |
| 490. | MARATHONA ... ... ... ... | 43 |
| 480-430. | ATENE ULIPOSITAWI ... ... ... | 78 |
| 399. | KUFARIKI SOKRATI ... ... ... | 84 |
| 336-323. | VITA ZA ISKANDER ... ... ... | 84 |
| 218-200. | VITA ZA HANIBALI ... ... ... | 117 |
| 166-161. | VITA ZA JUDA MAKABIO ... ... | 94 |
| 31. | KUTAWAZWA AUGUSTO KAISARI ... | 123 |
| 4. | KUZALIWA BWANA WETU *ĪSA MASIYA* ... | 123 |
| A.D. 70. | KUHARIBIKA YERUSALEMI NA WARUMI | 126 |


Digitized by Google

Digitized by Google

# MLANGO WA HISTORIA.

## 1. Historia.

Historia ni habari ya mambo yote ya dunia hii, na zayidi ya waana Adamu, ginsi yalivyofuatana tangu mwanzo hatta leo hivi.

Mwanzo wake twaujua, kama "Muungu aliumba mbingu na inchi," kwani mwenyewe ametujulisha; tena ya kwamba aliumba akatengeneza yote kwa hekima na taratibu. Lakini matengeneo yenyewe, ginsi yao na wakati wao, hakueleza sana, kadiri tu; akatuachia sisi waana Adamu kazi hii kubwa ya kutafutia habari za nguvu yake na shauri lake, ginsi alivyoiendeleza dunia na vyote vilivyomo, akatengeneza mambo ya watu tangu zamani za kale hatta sasa.

Nani awezaye kujifunza habari hizi zote? Hakuna mmoja. Lakini watu wa siku hizi wamejaliwa kuzidi sana kujua, kuliko wote wa zamani.

Jambo moja lililo kubwa peke yake na lenyi maana kwetu sisi duniani, ndio uzazi wake Bwana wetu Isa Masiya katika Bethlehemu, mji wa Yuda, B.C. 4. Ndio sababu twahesabu miaka yote hivi, mwaka

Digitized by Google

fullani mbele ya kuzaliwa Masiya (B.C.), ama mwaka fullani baada ya kuzaliwa Masiya (A.D.). Jambo hili likapata kuwa tangu miaka karibu mia tissatashara. Mambo yote ya mbele yake ni mambo ya kuitengeneza dunia tayari, na mambo yote ya baada yake ni mambo ya kuikamilisha.

Na taifa moja lililo kubwa peke yake na lenyi maana kwetu sisi tangu zamani ndio Warumi, na mji wao upo hatta leo katika Italia. Na taifa hili lilipositawi, ndio haswa wakati ule ule wa Bwana wetu alipotokea duniani, siku za Kaisari Augusto; dunia ikastarehe chini yake, ikawa amani katika inchi zake zote.

---

## 2. Milango ya Maarifa.

Killa kitu kina mwanzo, na mwanzo wa vyote ndio Muungu. Lakini killa kitu hakikuumbwa chenyi umbo na hali hii kiliyo nayo sasa. Kwanza dunia yenyewe yenyi kama mbegu na mianzo ya viumbe vyote vinginevyo; dunia ikaendelea ikapata tabia ya kufaa, mbegu zile kama zikaanza kukua, vitu vingi vikapata kuwa; vilivyofaa vikakaa vikaendelea. Mwisho dunia ilipotengenezwa na vitu vilivyomo, ndio nyama wakatokea, na mkuu wa viumbe vyote, Mtu. Kazi hii ya miaka mengi mengi na isiyohesabika; lakini "kwa Muungu miaka elfu kama siku moja"; na siku hizi amejalia watu wazidi kujua maajabu ya nguvu yake alivyoumba vitu, na hekima yake alivyoviendeleza na kuvikamilisha.

Siku hizi killa kiumbe kimekuwa kama kitabu chenyi maarifa mengi na habari nyingi kwao wenyi

Digitized by Google

akili ya kukisoma na kukifasiri. Wanafasiri kwa akili, wanasoma kwa "telescope," na kwa "microscope" na kwa "spectroscope"; zote hizo durabini.

"Microscope," kazi yake, inaongeza vitu vidogo vionekane kama vikubwa, hatta kiroboto awe machoni kama sura ya tembo, na nyele kama mianzi, na mavumbi kama majiwe. Kumbe vile vidogo vina vidogo vyao, kiroboto ana viungo vyake, kanwa, macho, tumbo, damu; mavumbi yapondekana hatta kuwa mavumbi membamba zayidi, wala mwisho hapana ya kuchungulia ndani ya kitu cho chote. Hatta macho yaishiwe nguvu za kutafuta, kitu hakiishiwi habari za kutafutika; kwani vyote kazi ya Muungu.

"Telescope," kazi yake, inaongeza vitu vilivyo mbali vionekane kama karibu; hatta jua likaonwa likizungukazunguka na lenyi mawaa meusi usoni pake; mwezi uko kama si mbali, kama mwendo wa siku tatu nne tu, tena wenyi milima na boonde; nyota zingine ni nyota mbili si moja, na hizo mbali sana, na zingine zenyi pete na miezi yao inazungukazunguka.

"Spectroscope," ni ajabu sana. Yatuonyesha vitu vilivyomo katika jua na mwezi na nyota, tena miendo ya nyota mojamoja. Hivi tumejua kama mwanga wa jua na mwezi na nyota, ndio chuma chokaa na hewa na lisasi na makaa na soda na vingine, yote yanawaka sana na kutoa moto na kung'aa. Tena miendo yao, hazisimami, zinakwenda sana, zingine kuja kwetu, zingine kwenda mbali.

Bassi yaliyo mfano wa vitabu vyenyi kutuarifu zayidi habari za mambo ya kale sana, ndio saba.

1. *Kitabu cha Mwanzo* katika Maandiko Matakatifu.
2. *Nyota*, elimu yao inakwitwa ASTRONOMIA.
3. *Mawe*, elimu yao inakwitwa JIOLOJIA.
4. *Masalio* ya watu wa zamani, ndio ARKIOLOJIA.
5. *Lugha* zingine zingine, ndio FILOLOJIA.

Digitized by Google

6. Hadithi na kazi na desturi na mambo ya watu, ndio ANTHROPOLOJIA.
7. Maandiko ya watu wa kale, ndio HISTORIA haswa.

Hayo ndio kama milango saba ya kuingia hekaluni na kutazama kazi za Fundi Mkuu. Kujua kazi zake ni kumjua Yeye, na kumjua Yeye ni kumpenda, ndio haswa uzima wa milele.

---

## 3. DUNIA.

"Katika mwanzo aliumba Muungu mbingu."

Mbingu zote zikawa moto ulao, mwako wake wa nguvu sana, ukajaa pote, wala hakuna kitu illa moto tu. Na asili ya moto, ndio vitu vidogo (*matter*) vikigonganagongana na kutangamana na kuchanganyika kwa nguvu (*force*). Tena killa kitu, kikubwa kwa kidogo, chamvuta kitu chote kinginecho; vyote vina uvutano (*gravitation*). Bassi moto ule ulipata kugawanyika, kufanya matangamano; mafungu makubwa yenyi kung'aa sana kupita umeme, na killa fungu lenyi kuzungukazunguka katika mwendo wake; fungu moja asili ya jua letu na dunia hii na nyota kubwa zenyi kulizunguka jua pamoja nayo. Hatta mwendo wenyewe wa kuzungukazunguka sana ukarushia mbali mafungu mangine madogo, nayo pia killa mojawapo likazunguka peke yake vile vile, ndio sayari zilivyotengwa na jua letu; lakini fungu kubwa ndilo jua lenyewe. Na kwa sababu nguvu za moto siku zote halafu yake kama hutaka kulegea, kupunguka, kuzimia, kupoa, na vitu

Digitized by Google

vidogo hupoa upesi kuliko vitu vikubwa, bassi hayo mafungu yaliyo sayari yakaanza kupoa kwa nje, yasing'ae sana peke yao illa kwa mwanga wa jua, lililo kubwa, tena halipoi upesi.

Bassi ndio habari (kadiri tuwezavyo kufahamu) ya mwanzo wa inchi yetu, ndio dunia hii. Muungu aliyeiumba, akaiumba kwa kuitenga na jua; dunia ikawa kama hewa iwakayo tu kwanza, nayo ikizungukazunguka kwa nguvu sana na kulizunguka jua. Hatta kwa nguvu ya kuzunguka kule dunia yenyewe ikafanya vile vile kama jua, ikarushia mbali nussu yake, na fungu lile likawa mwezi, wenyi kuizunguka inchi, lakini dogo; likapoa upesi kwa nje likatoka moto mahali mahali tu kama milima ya moto (volkano), likawa kama kitu kifu tu, lakini chenyi milima na boonde kama inchi hii.

Baadaye dunia nayo ikaanza kupoa kwa nje, kama kugandamana; kwanza hewa nzito, mawingu, giza, halafu umande (lakini wa moto sana) na maji ya kuchemka; tena maji mazito kama uji kama tope, matope ya kunata magumu, kama maji na matope yamechanganyika pamoja; na yote machafuko na giza bado.

Bassi dunia ikiwa hali hii ya kupoa na kugandamana, mawingu yakaanza kutakata, dunia ikapata nuru ndio ya jua. "Muungu akasema, Iwe nuru. Nuru ikawa." Bassi jua likaleta nuru na moto pia, inchi ikazidi kugandamana, mawingu yakapunguka yakapanda juu, ikawa nafasi kati. Tena killa kitu kikipoa, hupungukapunguka. Bassi inchi pia ikapunguka; lakini imeganda kidogo nje kama gome la mti, ikapunguka ndani, likafanya milima na boonde; na jua likaikausha inchi, zayidi milimani, ikawa inchi kavu, na maji ikakaa mbali mahali pake, ndio bahari. Jua likazidi kutenda kazi yake ya kufanya pepo zivume, mvua ikanye, ikafanya mito ikachukua

Digitized by Google

mawe na mavumbi na taka ya milimani ikafanya udongo mzuri boondeni kando la mito.

Ndipo ajabu kuu ilipoonekana. Vidogo vile vya asili ya inchi vilikuwa kama vifu kwanza, vyenyi mwendo tu na kuvutana (kitu gani kiwezacho kuwa hayi kwa moto mkali ?) ; kumbe vingine hayi na vyenyi uzima, kama mbegu ; mbegu zikaota zikachipuka zikazaa mbegu zingine, kwanza zilizo ndogo ndogo na nyonge kama majani ya pwani, baadaye mimea mikubwa. Na mathubutu ya jambo hili ndiyo mawe yenyewe, kwani katika miamba ya zamani sana mabaki ya mimea ile midogo yapo hatta leo, yameonekana, yatambulikana kuwa ndiyo ya kwanza, machache na thaifu.

Miaka mengi ikapita, inchi ikazidi kupoa, tabia yake ikatengeneka, wakati wa jua na baridi na mvua, masika na musimu, kipupwe na demani ; konokono zikatokea baharini na kombe na wadudu wa pwani ; tena samaki zenyi magamba makubwa ; na mimea ikazidi pangine pangine kuwa mikubwa na mingi sana juu ya inchi kavu. Na mawe mashahidi vile vile, kwani asili ya yale nawe yawakayo sana, makaa meusi, ndio mimea mitupu.

Baadaye na nyama zikatokea ; zayidi zitambaazo kwa mfano wa mamba na mjusi, zingine kubwa sana kupita nyama zote zilizopo sasa ulimwenguni. Tena ndege. Pakawa na mwitu nene za miti haswa, mfano wa mivinje na misunobari. Tena konokono zikazidi mno baharini, bahari ikajaa sana palipo inchi kavu kwanza. Na mashahidi mawe ; kwani mawe mengi mengi asili yao ni mabaki ya wadudu wa pwani na baharini.

Mwisho dunia ikapata kuwa kama yenyi hali hii na tabia hii iliyo nayo siku hizi ; miti mirefu kama yetu ; nyama kama nyoka, tembo, frasi, paa, ng'ombe, nyamgumi, nyani ; ndege nyingi na wadudu.

Digitized by Google

Hatta kwa wakati wake ajabu ingine ilionekana, nayo ndiyo kuu; mnyama bora mwenyi si mwili tu na akili za nyama zote zinginezo, illa peke yake mwenyi ufahamu wa kujijua na kujifikiri na kujitawala nafsi yake, na kuchagua mema na mabaya, na kumtambua Muumba wake kama yupo, na kumwabudu na kutaka kuwa alivyo Yeye, na kuweza pia. Na mnyama huyu asiye mnyama, ndiye mtu.

Ginsi alivyoumbwa akapata kuwa, hatujui. Lakini tumejaliwa siku hizi kutambua mambo mawili katika matendo ya Muungu yatupasayo sana. Tumefahamu ya kwamba vitu vizima vyote vimeumbwa vyenyi kazi moja ndio kula na kuzaa na kujishindania nafsi, vipate kuishi wala si kufa; vingi vilivyopo sasa havikuumbwa kwanza vyenyi maumbile yayo hayo viliyo nayo sasa, sura, tabia, mazoezi; vimepata kuwa vilivyo sasa kwa mageuzi na maendelezi; bassi labuda na watu pia. Kwanza vimekuwapo vilivyo thaifu sana, mimea na nyama; baadaye vilivyo vizuri na vya nguvu na akili, si kwa kuumbwa killa kitu peke yake, illa kwa kuzaa na kuzaliwa. Kama hivi; mbegu za asili za vitu vyote vyenyi uzima ni kama mamoja kwa ginsi zao. Hakuna tofauti. Na mimea ya kwanza kama ile ya baharini na pwani, mingine ikageuka kuwa mizuri zayidi ndiyo kama ile ya inchi kavu; na hiyo mingine ikageuka ikaendelea hatta kupata nguvu na uzuri kupita wenzio; mwisho ikatokea iliyopita yote, ndiyo ya siku hizi. Vile vile na nyama. Kwanza zile za baharini zilizo kama pofu tu; zingine zikaendelea zikapata kuwa kama kauli; nazo zingine zikageuka kuwa kama funza na kaa; halafu zingine zikapata uzuri zayidi, kama kombe na pweza; zingine tena zikafanya mgongo, zikawa samaki; baadaye zikapata miguu, zikatambaa, kama mjusi na mamba; zingine mabawa, zikaruka juu, ndio ndege; tena zingine zikazidi kuendelea, zikato-

Digitized by Google

kea hizo za siku zetu, frasi, ngamia, ng'ombe, tembo, vipopo, komba, kima, nyani.

Mwisho na juu yao wote, Mtu. Mageuzi na maendeleo ndio habari ya vizima vyote, ginsi vilivyopata kuwa mbali mbali kabisa kama siku hizi, na zamani namna moja. Vikageuka hivi. Killa kitu (mmea kwa nyama) huzaa vitu vingine kwa mfano wake, kama watoto wake. Lakini watoto wote si sawa. Killa mtoto yuna tofauti yake kuliko mzazi, na kuliko watoto wenziwe, wangine thaifu, wangine hodari. Tena ulimwengu wao mbali. Mmoja hupata mahali pema, jua, maji, chakula; mmoja hapati. Hawana buddi kushindania mema hayo, wakiwa wengi, na wote wanayataka. Bassi iliyo thaifu hushindwa, hupunguka, haikai; hatta ikizaa watoto, nao thaifu vile vile ao zayidi. Lakini ile hodari hushinda, huishi, husitawi; huzaa watoto, nao hodari vile vile na wenyi nguvu zayidi, waendelea, wazidi kupata nguvu na kuzaa watoto wenyi nguvu, hatta kama kuwa namna ngine, si kama mzazi wao wa kwanza. Ndiyo killa namna ya mimea na nyama ilivyopata kuwa ilivyo; kwanza mamoja, baadaye mbali sana. Vyote vyenyi uzima huzaa, hushindania chakula; viwezavyo kupatana na ulimwengu wao, hukaa; vilivyo thaifu, hushindwa na wenzio; vilivyo hodari husitawi, hushinda, huendelea kuwa na nguvu na uzuri zayidi.

Ndivyo, twaona, na watu walivyopata kuwa walivyo. Wamefanyika kwa udongo, kwani kwa mwili kama nyama, na chakula cha nyama mimea, na chakula cha mimea udongo. Lakini amejaliwa kuwa na roho ya uzima, na uzima wake kujifahamu nafsi na kumfahamu Muungu, —ndio uzima haswa na wa milele.

Lini alipotokea mtu wa kwanza ulimwenguni, na wapi, hatujui; lakini zamani sana. Kwani mifupa ya watu imeonekana ndani ya mawe chini pamoja

Digitized by Google

na mifupa ya nyama zisizo sawa na nyama za siku hizi, tena mawe yenyewe yamekaa sana. Bassi miaka mengi sana imepita. Lakini wenyi elimu wamethani ya kwamba inchi za milima kati yá Asia ndio makao ya watu wa kwanza, ao labuda inchi iliyozama chini ya bahari ya Hindi.

---

## 4. Waana Adamu wa Kwanza.

Mwana Adamu ni thaifu kuliko nyama wengi. Hana nguvu kama tembo, simba, mamba. Hana meno na makucha kama simba, chui. Hana mbio, kama frasi, paa. Hana mabawa ya kurukia juu kama ndege. Hana jicho kama tai. Hana mikono kama kima, nyani. Lakini akili anazo, na akili ndizo mali na nguvu, akili zikampatia chakula, akili zikamjengea nyumba, akili zikamfanyizia nguo, akili zikamtiishia ulimwengu. Kwani amebarikiwa tangu mwanzo, Muungu akamwambia, "Zaeni kaongezekeni, kajalizeni ulimwengu, kautiisheni."

Bassi watu walipotaka kula, walifanyaje? Hutafuta mimea, huokota mboga chini, ao huangusha matunda yaliyo juu. Lakini kazi kupanda miti. Tena wakikuta nyama mkali ao watu wenzio wakali, sharti kujishindania nafsi. Bassi ndio kazi ya kwanza ya akili, kujiongeza nguvu, kujifanyizia vitu na kuvitumia. Hatta nyani wamepata kutupa mawe, kupiga fimbo, marungu. Na watu vile vile. Huchagua mawe marungu, huzitumia kwa kuangusha matunda, kupiga nyama, kupigana. Halafu hutengeneza mawe, huyavunja kwa akili, hutwaa vipande vye-



Digitized by Google

nyi makali, huvitumia kwa kuchanja kuni, kufyeka msitu, kuangusha miti na vingine, tena kwa mishale, wapate kupiga nyama na kuongeza chakula chao (Stone Age). Ndivyo tuonavyo siku hizi kwa kusoma kitabu chenyi maarifa, ndio masalio yaliyoonekana pahali pahali na chini katika inchi, katika mawe na na matope. Tumeona vyombo vingi, vyote vya mawe, mashoka, mishale, visu, misumeno, nyundo, vya kutobolea. Kwa hiyo na kwa kuangalia watu wa asili wa inchi za kishenzi, twaona kama watu wa kwanza, hali yao ni kuwinda na kuokota chakula wawezavyo na kutega samaki kwa wavu, kupotea mahali mahali wasikae sana mahali pamoja; tena katika inchi za baridi ao pasipo paango, hukata miti na majani, hufanyiza nyumba; hujivalia nguo ndio ngozi, hushona kwa mifupa ndio sindano, na nyuzi za majani ao za matumbo ya nyama. Pangine hujenga nyumba majini juu ya nguzo, hukaza miti chini na mbau juu. Nyumba namna hizi zimeonekana katika maziwa ya Switzerland, kama na nyumba za kando la Nyasa, lakini za zamani sana.

Na mchezo wao ndio kuchora mifano ya nyama juu ya mifupa ao mawe, na sanamu hizo zimekaa hatta leo. Tena hupenda kupiga urembo na umalidadi, hufanya vipambo vya konokono, sandarusi, vingine, halafu na thahabu na shaba; kwani thahabu na shaba yapatikana safi kwa kuchimba tu, tena rahisi kufua (Bronze Age).

Baadaye, lakini yapata miaka mengi sana, wangine walibadilika hali, wakaanza kufuga nyama na kuchunga kondoo na mbuzi; kwani nyama yenyewe tamu, na maziwa pia, na ngozi nzuri kwa kuvaa; wakakaa hemani, kwani hema rahisi kuchukua, nao hawana buddi kufuatana na makundi yao kwenda kutafuta majani. Wangine wakaanza kupanda mbegu na kulima na kungojea mavuno; lakini shidda kwanza

Digitized by Google

kulima, kwani shidda kupata chuma kwa majembe. Wakatafuta njia ya kupika mawe na kuyeyusha chuma ya kufanyizia vyombo, visu, majembe, na vingine tena vingi. Na hivi pia vimeoneka na katika masalio ya watu wa kale (Iron Age). Kwa hivi waliweza kulima na kuvuna, wakaweka akiba, wakaanza kupata mali kidogo na kusitawi.

Baadaye biashara na kazi za mafundi. Kwani killa mtu akijiona ana akiba ya namna moja, akitaka vitu vingine mali ya mwenziwe, marra hubadilisha. Na mabadilisho ya vitu vya akiba ndio asili ya biashara.

Tena killa mtu huona kazi nyingi pamoja hazi fai, afathali moja, mtu apate kujua sana kazi yake akazidi kufanya vizuri na kupata akiba kubwa upesi. Marra hupita wenziwe kufanya kazi ile, amekuwa fundi.

Tena killa mtu atawala nyumba yake, mkewe na watoto, na ndugu zake husharikiana, na jamaa hukaa pamoja, hufanyiza mji, ndio mwanzo wa makabila na mataifa. Hatta wakikaa mbali mbali, ikija vita hawana buddi kukusanyika, kukaa mji mmoja, wasipotee.

---

## 5. Mianzo ya Mataifa ya Kale.

Twaamini ya kwamba waana Adamu wote ni mbegu moja, lakini tangu zamani za kale wamekuwa mbali kwa mambo mengi, kwa umbo, kwa rangi, kwa vitwa, kwa nyuso, kwa nyele, kwa macho.

Pana watu warefu, kama watu wa Patagonia, inchi ya kusini ya Amerika, karibu wote majitu.

Digitized by Google

Pana wafupi, ndio kabila la Bushmen, upande wa kusini wa Afrika, na tena vibeti wabilikimo wakaa mwituni kati ya Afrika. Pana watu weusi katika Afrika na Australia na Polinisia, pana watu wekundu katika Amerika, pana watu rangi ya manjano katika Asia ya mashariki na kati, pana watu weupe pande za Europa na Asia wa magaribi. Tena vitwa, wengine wenyi virefu, wangine vipana. Tena nyuso, wangine mataya mbele, midomo minene, wangine sio. Ziko nyele za singa na nyele za kipilipili, za kusokoteka, za kusongamana. Na tofauti hizo tangu zamani. Kwani iko Misri sanamu katika makaburi ya wafalme wa kale, yapata miaka elfu nne, watu wameandikwa halisi wenyi tofauti zizihizi za rangi na uso na nyele, kama sasa. Kwa miaka hiyo mengi hawageuki.

Bassi watu gani walio wa kwanza, hatujui. Waalimu husema, watu weusi. Wala wakati gani walipotokea, hatujui, lakini yapata miaka elfu marra nyingi. Kwani (kama tulivyosema mbele) mifupa ya waana Adamu yameonekana katika mashimo na paango, katika Ufransa na Uingereza pia, pamoja na mifupa ya nyama zisizo sawa nazo za siku zetu, tena mashimo yenyewe chini chini sana, yamezibwa na taka za mito na furiko, na udongo mwingi na mawe yamekuja juu, ndio kazi ya wakati mwingi. Tena siku zile tabia ya Europa ilikuwa si kama sasa; baridi kali pote na barafu na thuluji na bahari juu ya inchi kavu, kama tabia ya inchi Arktiko. Na tabia ya inchi haibadiliki upesi, yataka miaka mengi sana, yageuka polepole kidogo kidogo.

Wala wapi walipokaa kwanza, hatujui, isipokuwa pande za mto Frati, ndio inchi ya Waajjemi. Hakika ndipo walipoanza waana Adamu kuendelea na kusitawi kidogo. Hatta ndio Historia, mwanzo hatta mwisho, kujua habari za watu waliokaa inchi

Digitized by Google

tangu Frati hatta Bahari Mediterraneo na kuizunguka: kwani habari zao zatupasa walimwengu wote hatta leo, na habari za watu wangineo si sana.

Pana jamaa 'nne za waana Adamu wote, ndio hizi:

(1) Wakokesi (Caucasian), ndio weupe, na walio wenyi umbo mzuri haswa; hukaa kati ya bahari Kaspiano na bahari Nyeusi (Black Sea) milimani pa Kokesus; lakini wameenea zamani katika Europa na Asia wa Magaribi na Afrika wa kaskazini. Hatta watu wote wa Europa ni Wakokesi, illa Maturuki na wangine si wengi, na katika Asia Waarabu na Waajjemi na Wahindi pia Wakokesi. Tena wameenea katika Amerika, hatta sehemu mbili za watu wote walioko ni Wakokesi sasa. Hao wote weupe.

(2) Wamongoli (Mongolian), ndio watu wa Sina, Burma, Japan, Korea, na katika Europa Maturuki, na Wafinni na Walaplandi, na katika Amerika Waeskimo. Hao wote rangi ya manjano.

(3) Wanigro (Negro), ndio watu wa kati ya Afrika na toka huko hatta Kepi, na Wamalee (Malay) ndio watu wa Malaka na visiwa vyake, na wa Nyu Ziland na wa Bukini na kwa Kepi (si wengi), na visiwa vya Polinisia na Melanisia. Hao weusi, lakini kama Wamongoli kidogo maumbile yao.

(4) Wa Amerika wa asili, nao watu wekundu, lakini labuda asili yao Wamongoli kwanza.

Lakini pangine jamaa hizi wamechanganyika sana, wala hapana kuwapambanua vema. Hatta watu wa Australia hatujui asili yao; kama watu weusi, lakini mbali kwa vitwa na nyele za msokoteko.

Habari za mambo ya jamaa hizi za waana Adamu hatunazo nyingi, lakini kwa maarifa ya lugha, ndio Filolojia, twapata kujua kidogo mazunguko na kazi na desturi na hali ya makabila ya Wakokesi.

Lugha ndio tofauti kubwa ya watu na nyama. Watu wote hunena, nyama hawasikiani illa labuda

Digitized by Google

kidogo kidogo. Lugha za waana Adamu ni nyingi sana. Katika Afrika ziko zayidi ya miteen, na katika Hindi kama arobaini. Na lugha hizi zote zina tofauti zao, tena zinabadilika mwaka kwa mwaka; zingine upesi ndizo zisizopata kuandikwa sana; zingine kidogo kidogo, ndizo zilizopigwa chapa, zikawa namna moja yenyi kusomwa na kujulika na watu wengi.

Hatta Kiunguja cha kale, siku za Liongo, mbali na Kiunguja cha leo. Hivi mashairi ya Liongo, "Siwagazi kondo msi lango kapiga kifa, Ili kusifua kwambazo ni tule swifa, Nitangamizapo kondo nzito tenda hakhafa;" maana yake, "Siingii katika vita nisipokuwa na jambo kupiga kifua, Kwa ajili ya kusifiwa ambazo ni mbaya sifa, Hitegemea vita bora kuvitenda hafifu."

Bassi kwa kulinganisha sana lugha za watu wa Afrika, waalimu wamepata kujua kama Uganda hatta Kepi lugha zote asili yao moja.

Kwa hiyo twaona kama wazazi wa kwanza wa makabila haya mengi walikuwa wakikaa pamoja siku za kale wakasikiana maneno, wakawa hali moja na shauri moja. Lakini baadaye wazao wao wakaongezeka wakatawanyika mbali, killa kabila likasema wapendavyo wenyewe, lugha zikabadilika, wasisikiane vema sasa hatta kidogo.

Na vile vile tumepata kujua kama lugha za Kiarabu, Kifoiniki, Kishami, Kiebrania, zote asili yao moja na namna moja. Tena twaona kama makabila hao wanakaa kama majirani hatta leo.

Na vile vile tumepata hakika ya jambo hili. Lugha za Ingereza, Holland, Denmark, Jermania, Norwe na Swiden, Fransa, Hispanya, Ureno, Italia, Uyonani, Warussi wengi wa katika Europa, asili yake ni lugha ile ile ya Armenia na Ajjemi, na ile ile ya Wahindi wengi. Maana yake, zamani za kale palikuwa kabila moja lenyi lugha moja, wakakaa. Baadaye waka-

Digitized by Google

ondoka wakagawanyika, wangine wakafika Ajjemi, wangine Hindi. Wangine wakaenda magaribini wakaenea pote katika Europa. Bassi walipogawanyika hivi, marra lugha ile yao ya kwanza ikabadilika kidogo kidogo, killa kabila likashika maneno yake, usemi wake, tamko lake; hatta baadaye hawasikiani, lugha zote kama mbali mbali.

Lakini kabla hawajagawanyika, walipokaa pamoja kama taifa moja, tunaweza kusikia kidogo habari za kazi zao na desturi na maisha na maarifa; tunasikia hivi. Katika lugha za Ingereza na Uyonani na Ajjemi na Hindi, pana neno moja ile ile maana yake, *baba*, ngine, *mama*, tena *ndugu*, *umbu*, *mwana*, *binti* (maana yake haswa neno hili, mwenyi kazi ya kukama ng'ombe, Kiingereza, *daughter*), *nyumba*, *mlango*, *kujenga*, *kilima*, *kinu*, *nafaka*, *frasi* (si kuwapanda lakini), *ng'ombe*, *mbuzi*, *mbwa*, *nyuki*, *nguo za manyoya ya kondoo na ya ngozi*, *kupika*, *dubu*, *nyoka*, *mbwa wa mwitu*, *thahabu*, *fetha*, *shaba*, *upanga*, *upindi*, *mashua* (si vyombo), tena kuhesabu *mosi* hatta *mia*, *mfalme*. Bassi haina buddi watu waliotumia maneno haya, hali yao kama hivi. Kwanza, walifanya jamaa si kama nyama, mume na mkewe na watoto wao; tena walijenga nyumba zenyi milango, hawakukaa paangoni; walilima mashamba wakapanda wakavuna, si watu wa kuwinda tu, na kuvua samaki na kupotea inchi kwa inchi; walifuga frasi wakawatumia kwa kazi ya kukokota gari, wasijue kuwapanda lakini, tena mbwa; wakachunga ng'ombe, kondoo, mbuzi, wakanywa maziwa, wakala asali, wakavaa nguo; wakajua kusaga nafaka na kupika; wakafanya vita kwa selaha za shaba; wakajipamba kwa vitu vya thahabu na fetha, wakaweza kufua madini hizo. Tena wakawa na mashua, lakini ya bahari hapana habari; walikaa mbali katika bara ya juu. Wakajua kuhesabu, na kupambanua wakati kwa mwezi. Wakawa na wafalme wa kuwatawala.

Digitized by Google

Na Muungu walimtaja jina, maana yake kama *Anga*, wasijue vema habari zake bado, illa labuda kama yuko juu angani, naye mwenyi nuru na uzima.

Bassi hali yao si nyonge wala mbaya. Watu hao wameendelea mbele hatta siku zile za kale sana, si kama washenzi; na hao ndio wazazi wa mataifa yote yenyi sifa baadaye, na mambo yao na ya wazao wao ndiyo yaliyo Historia haswa, mambo yapasayo watu wote wa ulimwengu hatta leo. Na watu hao wametajwa jina, Waariani.

Makao yao kati ya Asia (milima Kushi na Altai), ao labuda katika Russia. Na magawanyiko yao si yote mamoja, na wakati mmoja. La. Kama mawimbi ya bahari, yalifuatana. Waliotoka kwanza wanakaa sasa mpakani mwa Ingereza na Ufransa kwa magaribi, wanakwitwa Kelti. Baadaye wakatoka baba zao Warumi na Wayonani, tena wangine wakaenda Hindi na Ajjemi wakakaa. Miaka ikapita, wangine wakatoka, ndio wakaao sasa pande za Jermania, Norwe, Swiden, Denmark, wanakwitwa Teutoni. Mwisho wakatoka wakaao Russia na mipakani mwake, ndio Slavoni. Hao wote waliwaondoa watu wa asili katika inchi hizi, na hao ndio waliofanya nguvu na kuendelea. Bassi killa mtu hana buddi kusoma zayidi habari za Waariani, na mataifa yao.

---

## 6. Mambo ya Mataifa Makuu ya Zamani.

Mwaka kwa mwaka watu wa siku hizi wanazidi kutafuta habari za watu wa kale, wanazipata kwa njia mbili, kwa kusoma vitabu vyao na maandiko, na kwa kusafiri katika inchi zenyewe.

Digitized by Google

Hatta katika Amerika kumeonekana majengo na kazi nzuri za watu wenyi akili na nguvu na maarifa na dini, watu wa Peru waliokwitwa Inka, na watu wa Meksiko waliokwitwa Aztek. Na katika visiwa pia vilivyo mbali katika Okeani Pasifiko, moja kimekwitwa "Easter Island," pana ajabu vile vile, mawe yaliyofanyizwa makubwa na sanamu za mawe na kazi zingine za akili na bidii. Na katika Afrika pia watu wamevumbua mabaki ya miji na ngome kubwa zenyi maboma ya mawe makubwa mazito kwenyi inchi ya Mashona, upande wa kusini wa mto Zambezi; na miji pwani pa Mrima mingine iliyotoswa sasa majini, na miji mengi kwenyi majangwa ya Usomali, lakini nani waliojenga wakakaa humo, wala ginsi gani ilivyoharibika miji na kuwa ukiwa tu, hatujui. Habari zao zimekwisha potea kabisa.

Za mataifa matatu habari tunazo nyingi, ndio Wasina na Wahindi na Wamisri, mataifa za kale sana, yanakaa hatta leo; na vitabu vyao vya dini tumeyasoma, na inchi zao tumetázama na kazi zao nzuri tume zijua; lakini mambo yao hayatupasi sana, yajapokuwa mataifa makubwa na hodari. Wasina wamefarakiana na watu wote makusudi hatta leo; na Wahindi wamejikalia wakajishughulisha na mambo yao, hawakutoka kwenda kupiga wangine; na Wamisri vile vile.

Bassi tuwekee mbali Wasina, Wahindi, Wamisri, tukazisome habari zao katika "Mlango wa Jografia." Tuangalie tu sasa ya kwamba mahali walipositawi hao, na watu wa Sham na Babel, ndipo siku zote inchi zenyi mito mizuri na mikubwa, na udongo mwingi na uzaao sana, na jua si kali sana lisilolegeza nguvu zao wazalia huko. Maana yake, watu wa zamani wenyi akili walichagua inchi itoayo chakula upesi pasipo kazi nyingi. Wakapata chakula tele, mali ikazidi, wakauza vitu wakaweka akiba wakakaa raha. Tena

Digitized by Google

walio na akili walipopata faragha hivi na nafasi, walitumia akili zao, wakajifunga kupata maarifa, kutazama nyota, kuangalia mambo ya ulimwengu, wakawa waalimu, na mafundi ya kazi zote; wakajenga miji wakasitawi sana wakaendelea katika desturi za kiungwana. Lakini hatta hivi habari zao hazitupasi sisi sana waana Adamu wangineo, kuliko habari za mataifa matatu, moja la Asia Wayahudi, mawili ya Europa Wayonani na Warumi.

Wayahudi, habari zao zasomeka katika maandiko yao wenyewe, walivyopata kuwa taifa, wakachaguliwa washike peke yao dini ya kweli na imani ya Muungu Mmoja, wakalindwa hatta siku alipozaliwa Bwana wetu Isa Masiya, naye Myahudi; baadaye wakaharibiwa kabisa mji wao, wakatawanyika wote katika inchi zinginezo hatta leo. Bassi tukiisha kusoma habari za Wayahudi, tujifunze kwanza kidogo habari za majirani yao, Washami, Wakaldayo, Wamedi na Waajjemi, waliokaa katika inchi sawa ya mito Taigris na Frati, wakawaonea wakapigana nao na Wayonani pia. Baadaye habari za Wayonani na Warumi. Hivi tutaingia mlango wa Historia, tutasikia zayidi habari za watu wa siku hizi na sisi pia tulivyopata kuwa hali hii tuliyo nayo.

---

## 7. Ndoto za Nabii Daniele.

Zamani za kale, imepata, miaka kama elfeen na hamsi mia, twasoma katika Maandiko Matakatifu ya kuwa Muungu alimfunulia nabii Daniele mambo ya ulimwengu, yatakayokuja toka siku zilezile mpaka siku za mwisho. Akamfunulia hivi.

Digitized by Google

Palikuwa na Sultani wa Babel, mji wa Wakaldayo, jina lake Nebukadnezar. Akaondoka akiendea Yerusalemi, mji mkubwa wa Wayahudi, akiutwaa, akachukua mfalme wake na wakuu wake na mashujaa wote, watu elfu kumi, na mafundi wote na wafua chuma; hawakubaki illa wanyonge wa watu, nao si wengi, B.C. 588. Akachukua na mtoto Myahudi, jina lake Daniele. Yule mtoto akakaa nyumbani mwa Sultani, akalewa vizuri, akapata kuwa waziri wake Sultani wa Babel.

Sultani akaota ndoto. Alipoamka assubui, amekwisha kuisahau kabisa; akaona uchungu kwa roho yake akaagiza watu wake wenyi akili na ilmu wamkumbushe ndoto yake wakamfasirie, wasiweze. Naye Daniele mcha Muungu sana, akawa nabii, Muungu akamjalia kumjulisha Sultani habari ya ndoto na tafsiri yake pia. Na ndoto ile ndio hii. Palitokea sanamu ya mtu mkubwa na mrefu, ikisimama mbele ya Sultani, iking'aa sana, na namna yake ya kuogofya, yenyi kitwa cha thahabu safi, kifua na mikono ya fetha, tumbo na mapaja ya shaba, miguu kwa juu ya chuma, kwa chini ya chuma kilichochanganyika na udongo. Hatta baadaye tazama jiwe lisilokatika na mikono, likaipiga sanamu katika miguu ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande. Nacho chuma na udongo na shaba na fetha na thahabu zikavunjika vipande vipande pamoja, zikawa kama makapi penyi kutwangia ng'ano, hatta baridi ikazipeperusha zisipate tena pa kukaa; jiwe lile lenyi kuipiga sanamu likawa mlima mkubwa, likajaza dunia yote pia.

Tena Daniele naye akaona ndoto, na tazama, pepo 'nne za mbingu zikishindana juu ya bahari kuu. Nyama wanne wakubwa wakazuka baharini, nao mbalimbali wao kwa wao. Wa kwanza kama simba, mwenyi mabawa ya tai. Hatta mabawa yake

Digitized by Google

yakanyonyolewa, akainuliwa katika inchi akasimamishwa kwa miguu ya binadamu na kupewa moyo wa binadamu. Na tazama nyama mwingine wa pili kama dubu, akajiinua upande mmoja, na mbavu tatu kinwani mwake katika meno yake, wakamwambia, Ondoka ukale nyama tele. Halafu yake tazama mwingine kama chui, akawa na mabawa ma'nne ya ndege maongoni mwake, nyama huyo naye mwenyi vitwa vinne, akapewa mamlaka. Halafu yake tazama nyama wa 'nne, mwenyi hofu na kuogofya na kuweza mno ajabu, akawa na meno ya chuma makubwa, akameza akavunjavunja akakanyaga mabaki na miguu yake. Huyo mbali na nyama wale wote waliotangulia, akawa na pembe kumi. Daniele akaziangalia zile pembe, na tazama, ikapanda katikati pembe ngine ndogo, mbele yake pembe tatu za kwanza zikang'olewa; na katika pembe hiyo macho kama macho ya binadamu, na kinwa chenyi kunena makuu. Hatta viti vikawekwa taratibu, naye Mzee wa kwanza ameketi, nguo yake kama theluji nyeupe, nyele za kitwani kama sufi iliyosafika, kiti chake kama ndimi za moto, gurudumo zake moto uwakao. Mto wa moto ukatoka ukipita katika mbele yake, elfu elfu wakamngojea, majeshi ya majeshi wakasimama mbele yake, hukumu ikatengenezwa, misahafu ikafunuliwa. Daniele akaangalia, kwa sababu ya sauti ya maneno makuu iliyoyanena pembe; hatta yule nyama akauawa, mwili wake ukaharibika, ukatolewa kwa moto uwakao. Nyama wale waliobaki, nao wakatwaliwa milki zao, wakipewa kukaa kwa muda na wakati. Na tazama, Mwenyi mfano wa binadamu akaja kwa mawingu ya mbingu, akamjia Mzee wa kwanza, wakamkaribisha mbele yake. Akapewa enzi na utukufu na ufalme, watu wote na mataifa na lugha wamtumikie; enzi yake ndio enzi ya milele isiyopita, na ufalme wake usioharibika,

Digitized by Google

Nabii Daniele akaota ndoto ngine, akiwako kando ya mto Kuran, jina lake la kwanza Ulai. Palikuwa na mbele ya mto ule kondoo mume anasimama naye mwenyi pembe; zile pembe zikawa ndefu, lakini moja ndefu kupita mwenzake, iliyo ndefu ikaota baada yake iliyo fupi. Na tazama, mbuzi mume akatoka magaribini, asipogusa inchi na miguu, akawa na pembe moja nzuri kati ya macho yake. Akamjia kondoo mume mwenyi pembe, aliyesimama kando ya mto, akamrukia kwa nguvu na hasira nyingi. Akamkaribia kondoo mume akamkasirikia kwa ukali sana, akampiga, akimvunja pembe zake mbili; yule kondoo mume hana nguvu ya kushindana naye; akamtupa chini akamkanyaga, wala hakuna awezaye kumwokoa kondoo mume katika mikono yake. Bassi yule mbuzi mume akakua sana; alipokwisha kupea, pembe iliyo kuu ikavunjika, zikaota pembe'nne nzuri kwa huko na huko na huko na huko. Na katika pembe moja ikatoka pembe ngine ndogo, ikakua sana kwa kusini na kwa mashariki na kwa inchi yenyi kupendeza. Ikakua hatta kwa jeshi la mbingu, ikatupa chini wa jeshi lile na za nyota, ikazikanyaga. Kumbe akajitukuza hatta juu ya mfalme wa jeshi; naye akatwaliwa ibada ya killa siku, na hekalu lake likaangushwa chini; pembe ile ikatupa chini yaliyo kweli, ikatenda kazi ikafanikiwa.

Daniele akasikia watakatifu wanazumgumza wakiulizana, Hatta lini bassi mambo haya mabaya-mabaya? Akaambiwa, Kwa muda wa siku elfeen na thelatha mia. Ndipo hekalu litakapotakaswa.

Daniele akafunuliwa tafsiri za ndoto hizi, na tafsiri zao sawasawa. Sanamu ile ndio milki 'nne kuu za dunia, na jiwe lile ndilo ufalme wa mbingu. Nyama wale ndio wafalme wa dunia, naye Mzee wa kwanza ndiye Muungu Mwenyiezi. Bassi ndivyo yalivyo-

Digitized by Google

kuwa mambo ya ulimwengu, ndivyo yatakavyokuwa yaliyosalia.

Milki za dunia zilizo kuu, ndizo hizi 'nne.

1. Ufalme wa Babel, na mfalme wake Nebukadnezar; kama kitwa cha thahabu kwa fakhari yake, na kama simba kwa kuwa mkali, na kama tai kwa kwenda upesi katika vita.

2. Ufalme wa Waajjemi, na mfalme wao Kuro; kama kifua cha fetha na kama dubu na kama kondoo mume, kwa maana ya kuwa hodari sana na uzito wake ndio nguvu yake, ukashinda mataifa matatu, wala haukupata fakhari kama wa kwanza.

3. Ufalme wa Wayonani, na mfalme wao Iskander; kama chui na mbuzi mume kwa kugundua na kushinda adui zote kwa gháfala; naye akashika Europa huko na Asia huko kwa nguvu zake, kama tumbo lishikavyo mapaja huko na huko, nalo kati kati.

4. Ufalme wa Warumi, watu hodari kuliko wote; wakavunja na kuponda na kukanyaga mataifa yote ya dunia, wasiweze kuyasuluhisha illa kadiri tu, kama chuma na udongo hazichanganyikani: mwisho wakatengwa wenyewe mafungu mawili.

Mbalimbali ufalme wa mbinguni, na mfalme wake Isa Masiya. Huo ulioanza siku ya Pentekote katika Yerusalemi, si kwa mikono ya watu illa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, umepata sasa miaka themantashara mia na settini, ukienea pote ukitiisha mioyo ya waana Adamu, wala hauna mwisho.

Digitized by Google

## 8. Inchi ya Babel.

Inchi ya Babel ndio inaokwitwa sasa, inchi ya Waajjemi, Ndipo waana Adamu wangine walipopata zamani za kwanza kujua desturi na mathehebu za kiungwana na kuhitimu ilmu nyingi na kazi nzuri nyingi.

Habari zao tunazo katika Maandiko Mtakatifu, kama hizi. Watu wa kwanza wakatoka katika milima ya Asia kwa mashariki, wakaona inchi nzuri na pana na sawa yenyi mto mkubwa ndio Frati, wakakaa humo, wakajenga miji na mnara kwa matofali na lami. Kazi ile ya kujenga mnara haikumpendeza Muungu, akaizuia akiwatawanya watu. Na inchi hiyo ndipo alipokaa kwanza Ibrahimu na jamaa yake, akaitwa na Muungu kuko huko akatoka akiacha ndugu zake na jamaa yake akienda kwa inchi ya Kanaan.

Tena siku hizi tumepata kutambua mambo yao hivi. Watu wa inchi ile wakatwaa udongo, wakaufinyanga, wakafanya matofali, wakapiga chapa maneno mengi na mazuri katika matofali hayo, habari za mambo yao yote, na desturi zao na ilmu pia, habari za miji na mashamba na vita na ibada na sheria na lugha na miti na nyama na ilmu ya nyota na ya kuhesabu nyingi. Matofali hayo yaliyopigwa chapa, yakachomwa moto. Yalipokwisha kuchomwa moto, yakawekwa katika vyumba vikubwa na vizuri, walinzi wakayangojea, na killa tofali limeandikiwa hesabu yake. Bassi watu wakitaka kusoma, huingia chumbani, humtakia mlinzi matofali, kama vitabu, huletewa taratibu, husoma. Kiisha soma huenda zao. Hatta miji ya Babel ilipoharibika, na matofali hayo yakapotea yakistirika na kifusi na mchanga na

Digitized by Google

magugu, inchi ikageuka kuwa nyika, hamna hatta watu, siku nyingi nyingi zikapita.

Hatta siku hizi watu hodari wenyi akili wakasema, Twende tutafute mahali pa miji ile iliyoharibika zamani, tupate kujua habari zao. Wakaenda wakitafutatafuta wakichimbachimba katika nyika, kumbe matofali mengi mengi yakaonekana mazima, tena majumba na mahekalu na miji na vitu vingi. Wakafurahi. Hivyo tulivyopata habari zingine nyingi sana za inchi ile.

Bassi watu wa kwanza waliositawi katika inchi ya Babel, ndio Waakadi; ndio waliopiga chapa matofali wakaandika vitabu vya kwanza, na watu waliwafuata wakaiga wakafasiri maneno yao.

Tena (kadiri tujuavyo sisi) Waakadi ndio waliobuni A, B, Ch, &c., si namna hii tunayotumia sisi. Asili ya kwanza kuandika harufi ndiyo kupiga sanamu ya kitu chenyewe unachokiwaza. Ukitaka kuandika samaki, hupiga sanamu ya samaki. Ukitaka kuandika kitu kisichoonekana, kama Muungu, hupiga sanamu ya mfano wake, ndio nyota. Kwani Muungu juu, na nyota vile vile.

Baadaye sanamu ya samaki ilitumika kuonyesha sauti *sa* kwa neno lo lote, na zingine vile vile. Tena kwa sababu shidda kuandika sanamu nyingi upesi kwa kalamu ya chuma tu, kama kuchora, waligeuza sanamu nyingi kuwa kama harufi tu. Hatta ndio habari ya A, B, Ch, &c. Lilikuwa kwanza sanamu za vitu, zikageuka kidogo zikawa kama alama tu ndio harufi.

Bassi Waakadi watu wa zamani sana. Waliacha maisha yao ya kishenzi, wakajiwekea mfalme (Sargon) kama B.C. 3800, wakajitungia njia ya kuandika, wakaandika nyimbo za dini na hadithi na habari za zamani za kale, wakajifunza maarifa ya nyota wakasitawi sana kwa mambo mengi ya kiungwana. Hatta habari za Nuhu na gharika, na

Digitized by Google

ya kuumbwa ulimwengu na ya mnara wa Babel, na mambo ya Aden na vingine kama tulivyohadithiwa katika Maandiko Matakatifu, yameonekana katika vitabu vya Waakadi.

Baadaye wakaendewa na watu wa Asshur wakashindwa nao. Waashur wakaimiliki inchi, wakafundisha watoto wao lugha ya Waakadi na harufi, kwa maana waweze kusoma vitabu vyao na kuvifasiri na kufuatisha, na kujua maarifa yao. Hatta toka B.C. 2300 wanajimu katika Babel waliandika habari za nyota killa siku mwaka kwa mwaka.

Waliposhitawi Waasshur ndio kama mwaka B.C. 650, na wafalme wao wangine walipigana na wafalme wa Israeli, ndio Tiglath Pileser na Sanherib; na mji wao mkubwa Ninawi; wakakusanyia humo jamii kubwa ya vitabu vya udongo thelathini elfu. Mwisho mfalme wa Babel akawaasi akawapiga, akateketeza Ninawi kama B.C. 607; Babel ukazidi kuwa mji mkubwa kuliko miji yote ya pande zile.

---

## 9. Sultani Nebukadnezar na mji wake Babel.

Palikuwa na Sultani wa Babel, jina lake Nebukadnezar, naye hodari sana akamiliki tangu B.C. 605 hatta B.C. 562. Kwanza akawashinda Wamisri, tena akawashinda Wayahudi, akateka Yerusalemi akachukua watu wake wote (B.C. 588). Akafanikiwa sana.

Alipokwisha kurudi kwake akauongeza mji Babel, akaujengea boma kubwa, akaupamba sana na majengo mengi mazuri na hekalu na mnara na jumba na



Digitized by Google

bustani. Habari za mji wake tumeletewa na mtu Myonani, jina lake Herodoto, aliyekwenda kutazama mwenyewe, akarejea kwake akaandika mambo yote aliyoyaona katika kitabu; kitabu kile kikawapendeza sana Wayonani, sifa zake zikaenea katika ulimwengu wote hatta kwa leo. Na habari zake ndizo hizi.

Babel ni mji mkubwa sana ajabu. Umejengwa kwa mrabba halisi, wenyi boma pande zote 'nne; na pande zote 'nne zimenyoka sawasawa, na urefu wao mmoja, killa upande urefu wake kama mwendo wa saa sita, upande huu na upande huu na upande huu na upande huu, zote sawasawa. Na boma hilo ajabu pia. Limejengwa kwa matofali na lami pia, lenyi kwenda juu mikono miteen, na unene wake mikono hamsini. Hatta na nyumba zimewekwa juu yake huko na huko, na kati ya nyumba njia pana juu ya boma; gari la frasi wa'nne halikosi nafasi ya kupitia njiani katikati ya nyumba zilizoko juu ya boma. Na katika boma milango ya shaba mia na minara mengi mengi. Tena pambele ya boma pia kwa nje shimo limefanyika, limechimbuliwa chini sana, na pana, limejaa maji kama mto. Ndizo habari za boma la Babel. Na ndani yake mashamba mengi na makoonde na majengo na nyumba. Njia zote za mji zimenyoka sawasawa. Tena mto mkuu na mzuri ukiingia katika mji upande mmoja, ukipita katikati yake, ukitoka upande wa pili. Na kingoni pa mto kuta huko na huko; na katika kuta hizi milango mengi ya kupandia mjini. Hatta daraja kubwa na refu la kuuvukia mto, watu wapite upesi kwa miguu kwenda ng'ambo ya pili.

Sultani Nebukadnezar akaupamba sana mji, akazinyosha njia zake, akajenga hekalu kubwa kwa muungu wake, na jumba kwake mwenyewe, akafanyiza tena bustani. Hatta bustani ile imeshinda zote kwa kazi yake ya ajabu. Imetegemea yote nguzo na matao, ikafika juu kwa madaraja mengi,

Digitized by Google

juu kwa juu, kama kilima chenyi kwenda juu mikono miteen; na katika madaraja miti yote iliyojulika, namna zote, na jamii ya maua mazuri, na njia za kutembelea huko na huko kwa kujifurahisha na herufu nzuri ya maua yale na matunda ya miti na uvuli na kupepewa na baridi: ziko na nyumba za kupumzikia na kutazamia mji umetanuka chini na uzuri wake wote na kazi zake zote. Na hiyo ajabu. Bustani ikanyweshwa maji kwa bomba. Bomba ikayavuta maji ya mto upitao chini, ikayapandisha juu, maji yakatoka juu tele, yakainywesha bustani pia.

Sultani Nebukadnezar alipomaliza kazi hizi zote, siku moja akapanda darini kutembea (ndivyo tulivyohadithiwa katika kitabu cha nabii Danieli) akatazama mji wake na jumba lake na mali zake zote, akajivuna sana rohoni mwake, akasema, "Tazama mji huu Babel, nilioujenga mimi kwa nguvu ya enzi yangu na kwa heshima ya utukufu wangu." Akisema haya, marra akageuzwa moyo, akili zake zikampotea, watu wakamfukuza, akala majani kama ng'ombe, akipata miaka saba kwa hali hii. Hatta baadaye akainulia macho yake mbinguni, akili zake zikamrudia, akawekwa katika ufalme wake vilevile, akamshukuru Muungu.

---

## 10. Sultani Kuro na Babel.

Palikuwa na Sultani wa Waajjemi, jina lake Kuro. Akaondoka akawashinda Wamedi. Alipokwisha kushinda Wamedi, akawashinda Waludi, taifa kubwa la Anatolia, akamiliki Anatolia yote pia. Akafanya

Digitized by Google

jeshi kubwa, akauendea Babel, akataka kuutwaa. Alipokaribia boma lake akasangaa, akaingiwa na mashaka, akiona lilivyokwenda juu sana wala halivunjikani, wala hakuna kulibomosha, ginsi lilivyo nene mno; wala hakuna kuwashindisha watu kwa njaa, kwa sababu ya kuwa mashamba mengi na makoonde mengi ndani ya boma; hatta vita haithuru, watu wakilima vilevile na kupanda na kuvuna na kukaa raha na salama. Lakini kwa sababu watu wake wengi, tena sifa zake za vita zimeenea sana katika inchi, aliutwaa mji pasipo uthia wala kupigana sana. Alipata kulivunja boma mahali mahali, watu wa Babel wakaogopa, wangine wakajitoa, wangine wakamkaribisha, mfalme wao akataka kukimbia, akakamatwa. Tena tumehadithiwa na hivi, kama Kuro akafanya shauri ngine, akagawanya watu wake makundi matatu, akaweka kundi moja kuko huko mto ulikoingia mjini kwenda kupita katikati yake, na kundi moja kwenyi ulikotokea upande wa pili. (Na mto ule mkubwa, ukipita katikati ya mji toka upande huu hatta upande wa pili, wenyi kuta huko na huko kingoni mwake na milango ya kupandia mjini katika kuta.) Akaamuru makundi yale mawili, akisema, Mkiona maji ya mto yamepunguka sana, mwingie mtoni mwende mbio ndani ya mji, mkautwae. Alipokwisha kuwaagiza haya, akatwaa mwenyewe kundi la tatu, ndilo watu wasiofaa kwa kupigana, wazee na watoto na walio thaifu, akaenda zake kando la mto kwa kaskazini, ndipo mto ulipotoka, hatta akafikia ziwa kubwa, nalo karibu ya mto. Na ziwa lile limekauka, hamna maji illa kidogo tu. Kuro akafanyiza njia ya maji tokea mto hatta kwa ziwa, akangojea siku kuu ya Wababel, marra akauziba mto akayachurukiza maji yake yote kwa ziwa. Bassi watu wale waliongoja kule karibu ya mji wakauangalia mto, kumbe maji yamepunguka hatta kadiri ya kufi-

Digitized by Google

ka pajani; wakaondoka wakaingia mtoni makundi yote mawili, wakapita mbio ndani ya boma, wakakuta milango ya kingoni mwa mto huko na huko imeachwa wazi, kwa maana watu wanafanya siku kuu, wakautwaa mji (B.C. 539); wakamwua liwali wake ndiye Belshazzar. Yule Belshazzar akawa anafanya karamu kwa siku kuu, na wakubwa wengi, akaamuru watumishi wamletee vyombo vitakatifu, Sultani Nebukadnezar alivyochukua katika hekalu la Yerusalemi, akanywa navyo. Marra ukamtokea mkono wa mtu, ukaandika maneno katika ukuta yasiotambulikana. Liwali akasangaa na wakubwa wake, akatafuta mtu mwenyi kufasiri maneno yale, asipate, illa nabii Daniele ndiye aliyemfasiri maneno. Na maneno yaliyoandikwa ndio haya, Mene, Mene, Tekel, Ufarsin, na tafsiri yao, Mamlaka yako imehesabiwa, imepunguka, imetengwa. Bassi usiku uleule ndipo Waajjemi walipotwaa Babel kwa hila, wakamwua liwali Belshazzar. Na kwa sababu mji ule kuwa mkubwa na mrefu sana, nao watu wakikaa mbalimbali, watu wengi walikuwa hawajasikia habari kama mji umekwisha kutwaliwa.

Marra Kuro akatoa upole mwingi, akasterehisha watu wa Babel na miji yake, akarudishia killa mji sanamu ya miungu yake akayatengeneza sana mahekalu, akawapa na Wayahudi walioko ruhusa kwenda Yerusalemi na kujenga tena hekalu lao; Daniele akawa waziri wake. Na Kuro huyo yuna sifa nyingi katika maneno ya manabii. Isaya alimnena jina lake na kazi yake (Is. Sur. 45, 1-6), na ginsi atakavyoshinda mataifa, na upungufu ule wa maji, na kuwaagiza Wayahudi warejee kwa Yerusalemi. Tena Yeremia alitoa habari nyingi ya ukuu wake Babel na ubaya wake na kuharibika kwake; na ruhusa yake kwa Wayahudi imeandikwa katika kitabu cha Ezra (Sur. 1, 7—11).

Digitized by Google

## 11. Sultani Kuro alivyokufa.

Sultani Kuro alipokwisha kuutwaa Babel na kutiisha Washami, akakaa siku nyingi akakusudi kuondoka kwenda pigana na Wamassageti. Nao wakakaa upande wa pili wa mto Aras, karibu ya bahari Kaspiani, na Sultani wao ndiye mwanamke, jina lake Tomuri. Kuro akatuma mjumbe aende amtake mwanamke yule amwoe. Naye akakataa, akiona kama jambo hili ujanja tu apate kumua. Kuro akaondoka akafika hatta mtoni, akafanya vita kwa wazi. Sultani mke yule akatuma mjumbe, akisema, "Angalia, usitende haya. Hufanikiwi. Nenda kwako, kasterehe. Usipokubali, nakutolea mambo mawili. Nikuache wewe kuvuka mto, kuja huku kwetu mwendo wa siku tatu, ao uniache mimi kuvuka kule kwako sawasawa? Bassi chague." Kuro akafanya shauri akamjibu, "Nivuke mimi kuja kwenu." Akavuka akaenenda siku moja. Kiisha akaandaa vyakula vingi na vizuri, akaacha watu wake wasio na nguvu wala kufaa, akaenda zake. Wakaja Wamassageti, kundi moja, akawapiga walioachwa wakajinyosha kwa chakula. Marra akarudi Kuro, akawagundua katika karamu, akawashinda sana, akachukua wengi sana wamefungwa, na mtoto wa Sultani, jina lake Siparagapisi. Yule Sultani mke akaghathabika sana, akatuma mjumbe, akisema, "Ee mnywaji damu, nakutolea mambo mawili. Uniachie mtoto wangu, uende kwako kwa salama, ao nikushibishe damu?" Hakuyaangalia maneno haya hatta kidogo. Na mtoto yule wa Tomuri akaomba kufunguliwa kidogo; alipopata ruksa akajichinja mwenyewe. Kuro akaondoka, akapigana sana na Wamassageti. Kwanza wakapigana na mishale, halafu yake na mikuke na panga. Mwisho

Digitized by Google

watu wa Kuro wakakimbia, naye mwenyewe akauawa (B.C. 529). Bassi yule mwanamke akatwaa kiriba cha ngozi, akakijaza damu ya watu, akatia kitwa chake Kuro, akisema, "Ulipomua mtoto wangu, umeniua mimi. Nami nimekushibisha damu. Hiyo ndiyo niliyosema. Bassi."

---

## 12. Sultani Dario.

Baada ya Sultani Kuro miaka si mengi, kulikuwa na Sultani wa Waajjemi, jina lake Dario. Akianza kumiliki, rayia zake wakamwasi, akawapiga, akawatuliza. Kiisha akatengeneza kwa akili milki yake yote, akaitengeneza hivi. Akagawanya milki yake mafungu asharini, yaliyokwitwa satrapia, na liwali wake killa satrapia huitwa satrapi. Killa satrapi kama sultani katika milki yake, hutoza watu ushuru, humpelekea Sultani Dario. Tena Sultani Dario akafanyiza njia kuu, zenyi nyumba za kupumzikia, na matalishi wengi, kazi yao kupita huko na huko upesi kwa frasi katika ufalme wake pia, kupeleka barua za Sultani na kutangaza amri zake na kumpasha habari za milki yake yote. Jambo la tatu, Sultani Dario akapiga chapa vipande vya fetha na thahabu, killa kipande chenyi sanamu ya mtu na uta wake, vipande hivi vitatumika kwa mambo ya biashara katika ufalme wake. Akasitawi, akataka kuzidisha ufalme wake, akafanya vita tatu, ya kwanza na Wahindi, ya pili na Wasikuthi, ya tatu na Wayonani. Akaondoka akawapiga Wahindi, wakamlipia ushuru.

Digitized by Google

## 13. Vita ya Dario na Wasikuthi.

Sultani Dario akataka kupiga Wasikuthi: Akatwaa watu elfu mia saba, akaondoka katika mji wake Susa, akafika hatta kwa Bosporo, ndio mlango mwembamba yatokapo maji ya Bahari Nyeusi karibu ya Stambuli. Akavukisha jeshi lake kwa daraja lililotegemea mashua nyingi, akashika njia akafika mtoni Istro, unakwitwa sasa Danubi, akavuka akaingia inchi ya Wasikuthi.

Wakuu wa Wasikuthi wakakusanyika wakafanya shauri, wallakini wangine hawakukubali. Shauri lao ndilo hili, kwanza kumkaribia Dario tena kumkimbia, marra kumkaribia marra kumkimbia, marra nyingi vilevile; nao wakichukua mali zao zote na vitu vyote na watoto na waanake katika magari, wakiharibu tena majani na miti na vyakula vyovyote,—hivyo kumvutavuta Dario kwa nyika kuu, wapate kumshindisha kwa njaa kumpoteza jangwani yeye na watu wake. Ndivyo walivyofanya. Dario akawafuata, nao wakaendelea nyuma, wakamwongoza kwanza makusudi katika mashamba ya wakubwa wale wasiokubali shauri lao, wakawauthi sana. Kiisha wakamvuta siku nyingi hatta kufika nyikani. Dario akachoka, akafanya uchungu mwingi, akatuma mjumbe kwa sultani wa Wasikuthi, akisema, "Gissi gani kukimbia tu? Usipoogopa, tupigane. Ukiogopa, niletee maji na udongo, mimi bwana wako." Yule mfalme wakamjibu, "Hatta sikimbii mimi, natembea tu. Desturi ya Wasikuthi kuhamia huko na huko sikuzote. Hatuna miji, wala mashamba. Bassi hatupigani nawe. Zawadi nitakazokuletea mbalimbali. Si wewe bwana wangu." Wakafuliza kumvuta Dario kwa nyika, hatta Dario akashikwa na matata na

Digitized by Google

hatari na misiba mengi. Wasikuthi wakampelekea zawadi, ndege mmoja na panya mmoja na chura na mishale mitano. Maana ya zawadi hizo haikumwelea vema, akafanya baraza ya wakubwa akasema, "Nathani zawadi hizo ndio Wasikuthi kujitoa kabisa, kwa sababu maana ya panya ndio watu wakaao inchi hii, na ndege ndio frasi zao, na chura ndio maji ya mito na visima, na mishale ndio selaha za vita." Lakini waziri wake, jina lake Gobiria, akasema, "Nami naona zawadi hizo ndio kunena, 'Ee Waajjemi, hamna buddi ao kuruka juu kama ndege, ao kufukua chini kama panya, ao kujitupa majini kama vyura, ao kuuawa na mishale hii.'" Marra Wasikuthi wakakaribu kwa kupigana. Sungura akaruka katikati yao, Wasikuthi wakaacha kwenda pigana, wakapiga kelele wakimfufuza sungura. Ndipo Dario akashangaa, akafanya ajabu mno, akasema, "Tazama watu hawa wanitharauvyo kabisa. Kuliko sungura, mimi si kitu." Moyo wake ukageuka, akafanya shauri la kukimbia. Akaacha kuko huko watu wake wasiofaa wala hodari kwa vita, akawaambia, "Kaeni papa hapa, naenda kutafuta Wasikuthi." Akatwaa wote wenyi nguvu akakimbia, nao walioachwa wakapatwa na Wasikuthi wakauawa. Dario akafika mtoni Istro kwa shidda, akavuka akaokoka.

---

## 14. Sultani Dario na Wayonani.

Zamani za kwanza Wayonani wakakaa katika Uyonani, ndio inchi yao katika Europa, wakakaa pwani pa Anatolia (Asia Minor) kwa magaribi, wakakaa

Digitized by Google

katika visiwa vyingi vya bahari iliyo katikati, inaokwitwa Arkipélago. Nao wa pwani wale wakapigwa na jemadari wake Kuro wakamtii. Lakini Dario alipokuwa Sultani wa Waajjemi, wakamwasi wakaondoka wakateka mji mkubwa Sardisi, wakauteketeza moto. Na Waatene, ndio watu wa mji Atene (Athens) ulio mkuu katika Uyonani, wakawasayidia. Sardisi ni mji wa Waludi, lakini siku zile Waajjemi walioumiliki. Bassi Sultani Dario alipoletewa habari kama Sardisi umeharibika pia, akafanya hasira sana. Nao Wayonani wa Asia hakuwaangalia hatta kidogo, kwa maana kitu chepesi kuwapatiliza mambo hayo. Lakini Waatene ndio aliowachukia sana, naye hajasikia habari zao, sababu wametoka mbali; akauliza, "Watu gani hao wageni?" wakamwambia. Akatwaa upindi akatia mshale katika uzi akapiga juu kwa mbingu, akisema, "Ee Muungu, unijalie niwalipize kisasi Waatene." Akamwagiza mtumishi wake amwambie killa siku saa ya kula jioni, "Ee Bwana, usiwasahau Waatene."

Kwanza akapeleka mkwewe, jina lake Mardonio, awapige Waatene. Naye Mardonio akakusanya watu wengi na merikebu nyingi, akavuka Bosporo, akashika njia ya kwenda Uyonani, asifanikiwe. Washenzi wa barra wakapigana sana naye, wakamzuia njiani, merikebu zake mia tatu zikavunjika na thoruba kuu karibu na mlima Atho, watu asharini elfu wakapotea. Akarudi kwake na watu waliosalia.

Tena Dario akatuma wajumbe kwenda kuwatakia Wayonani udongo na maji, ndio alama ya kujitoa. Wengi wakampa, kwani Wayonani hawakupatana vema siku zote, wala kuwa shauri moja. Hatta watu wa kisiwa Aigina karibu na Atene walijitoa kwa sababu waliwachukia Waatene wakataka waangamie. Marra Dario akapeleka majemadari wakubwa wawili, Dati na Artaferni, wakapita baharini njia ya ku-

Digitized by Google

nyoka, wenyi merikebu nyingi na watu wengi, wakashuka pwani katika Marathona, mji ulio karibu na Atene, kama mwendo wa saa sita. Waatene wakaona, wasipowapiga Waajjemi palepale, wamekwisha kusalimika ajali kabisa. Wakaondoka wakaenda Marathona, wakapanga juu ya kilima, watu elfu kenda tu, na elfu tena ndio watu wa mji Platea, jumla elfu kumi. Na Waajjemi watu elfu mia wako chini pwani kati ya vilima na bahari, nao hodari na wasioshindika siku zile, na wapanda farasi pia. Waatene wakaogopa, wakuu wao wakafanya shauri wakimbie. Hatta palikuwa na mtu mmoja mkuu, jina lake Miltiadi, na mtu huyu mshujaa sana na mwenyi akili, akawashawishi Waatene wakae wapigane kuko huko. Bassi wakaenda mbio wakarukia Waajjemi. Hatta Waajjemi wakastaajabu, wakiona watu haba walivyowarukia, nao kwa miguu tu, hapana mwenyi frasi, wakawacheka kwa kuwa kama watu wenyi wazimu. Wakapigana saa nyingi. Waatene wangawa haba wakipigana taratibu na kusikia amri, kama mfulizo mmoja wote, wakawaweza Waajjemi wengi wengi wasiopigana kwa akili, illa vivi hivi tu kama nyama za mwitu. Waajjemi wakapigwa sana, wakauawa zayidi ya elfu sita, wakafukuzwa hatta vyomboni, wakapanda wakaenda zao. Marra walipokienda, walitwekewa ng'ao mbali na Waatene wabaya, ndio ishara ya kusema, Hapana watu mjini. Waajjemi wakatweka upesi wakazunguka ras Sunio wakaiendea bandari ya Atene. Wasidiriki, kwani Miltiadi na jeshi lake wamerudi upesi, wako wamesimama pwani tayari kupigana marra ya pili. Waajjemi wakakata tamaa wakarudi kwao Asia (B.C. 490).

Sultani Dario akaingiwa na uchungu mwingi, wala hakukubali kushindwa wa Wayonani. Hatta akipatikana na farathi, akafa (B.C. 486).

Na vita hii ya Marathona ni jambo kubwa sana.

Digitized by Google

Mji mmoja Myonani nao mdogo uliwapigania watu wote wa magaribi wasiwe mateka ya watu wa mashariki, ukawaokoa. Ungalishindwa, labuda mfalme wa Ajjemi angalitawala, na watu wa Europa chini yake kama watumwa wake hatta leo. Lakini sivyo.

---

## 15. Sultani Serkisi na Wayahudi.

Dario alipokwisha kufariki, Serkisi mwanawe alikuwa Sultani wa Waajjemi. Akakaa miaka miwili akawatiisha Wamisri waliomwasi. Mwaka wa tatu Sultani Serkisi akaita barazani maliwali wake na wakubwa wake wote, waje kwake katika mji Susa, wafanye shauri la vita kwa Wayonani. Wakakusanyika, wakafanya shauri, wakatazama mali za Sultani zote siku mia na themanini. Kiisha Sultani akawafanyia wote karamu kuu ya siku saba katika bustani yake. Karamu ile ikapambwa vizuri ajabu. Bassi siku ya saba Sultani akanywa mvinyo, akawaita matowashi wake saba, akawaamuru wamletee malkiya ndiye Vashti, awaonyeshe watu uzuri wake. Naye mwanamke yule mzuri sana. Mwanamke yule akakataa, akisema, "Sitaki." Sultani akafanya ghathabu, akamwondoa katika kuwa malkiya.

Baada ya siku nyingi akatafuta mke awe malkiya yake mahali pa Vashti. Palikuwa na mtu Myahudi, jina lake Matakasi (Mordekai), mngoje mlango wa jumba la Sultani. Akawa na mtoto mmoja, jina lake Ester, binti ya nduguye, akimtunza akimpenda sana. Na yule mtoto mzuri sana, akatafutwa akaletwa kwa nyumba ya waanake wa Sultani. Akakaa

Digitized by Google

humo miezi kumi na miwili. Kiisha akavaa mazuri akapambwa vizuri akaingia nyumbani kwa Sultani. Yule kijana akampendeza sana Sultani, akawa malkiya yake.

Hatta siku zile matowashi wawili wa Sultani, wangoje mlango, wakafanya shauri la kumchinja. Jambo lile likajulika na Matakasi, akampasha Ester habari, naye akamjulisha Sultani. Wakatafuta watu wale wakawasulubisha.

Siku zikapita, Sultani akamzidishia mtu, jina lake Hamani, kuwa waziri wake, watu wote wakamsujudia Hamani, illa Matakasi tu, naye hakumsujudia wala kumheshimu. Hamani akaona uchungu mwingi, akafanya shauri awaue watu wote pia walio Wayahudi kwa ajili ya Matakasi. Akaenda kwa Sultani akamwaambia, "Ee Sultani, wako watu wabaya katika milki yako, wanakaa huko na huko mahali pote, nao mbali na watu wote, wala sheria zako hawaziangalii. Bassi naona heri wachinjwe wote pia, nami nitaweka fetha yao nyingi katika hazina za Sultani." Sultani akakubali, akatuma wajumbe killa mahali na barua kwa maliwali, Wayahudi wote wauawe mwezi wa kumi. Yule Matakasi akapasua nguo zake akavaa gunia akalia kwa sauti ya uchungu mjini, Wayahudi wote wakalia na kufunga na kulalia gunia na majifu. Matakasi akampasha Ester habari hizi, akamwagiza aende kwa Sultani awaombee Wayahudi, ndio nduguze. Naye akasema, "Siwezi; killa aingiaye kwa Sultani huko ndani, Sultani asimpungie fimbo lake, huchinjwa." Akamwambia, "Hatta usipomwingilia utachinjwa. Siwe Myahudi?" Akasema, "Ntakwenda; fungeni tu siku hizi tatu, wewe na Wayahudi wote, nami pia." Siku ya tatu akamwingilia Sultani, Sultani akampungia fimbo lake la thahabu, akisema, "Wataka nini?" Akamwambia, "Nataka wewe na Ha-

Digitized by Google

mani, mje kula kwangu." Akasema, "Vema." Wakaja. Sultani akamwambia, "Wataka nini tena?" Akamwambia, "Nataka mje kula kwangu kesho marra ya pili. Ndipo nitakapomjulisha Sultani nitakavyo." Hamani yule akajivuna sana kwa sababu ya kwitwa marra mbili, akaenda kwake, akaona Matakasi yuko mlangoni hamwondokei vilevile, akaingiwa na uchungu. Akafika kwake akawaita wenzake na mkewe, akawaonyesha mali zake nyingi na′daraja lake na daraja lake na mambo yote bora na makuu yaliyompata, na kwitwa kula kule na Sultani na malkiya yake. Akawaambia, "Hatta haya yote hayanifai neno, nikimwona yule Matakasi yuko anakaa mlangoni mwa Sultani." Wakamwambia, "Kesho mtakie Sultani asulubiwe." Akafurahi, akafanyiza msalaba wa mti wa mikono hamsini, ndio urefu wake.

Usiku uleule Sultani halali, akaletewa vitabu vya mambo ya ufalme wake akasomewa habari. Likasomwa jambo lile la matowashi wawili, waliotaka kumchinja mwenyewe. Sultani akasema, "Zawadi gani aliyopewa Matakasi, sababu aliniokoa?" Wakamwambia, "Hapana hatta kitu." Sultani akawaulizo, "Yuko nani huku uani?" Wakamjibu, "Hamani yuko." Akasema, "Mwite." Wakamwita. Sultani akamwambia, "Ikiwa Sultani anataka kutukuza mtu sana, amfanyieje?" Hamani akaona katika nafsi yake, "Atakayetukuzwa ndimi." Akasema, "Ziletwe nguo zake Sultani za kifaume, na frasi wake Sultani na taji yake Sultani, tena mtu aliye na daraja bora azipokee, amvike yule mtu Sultani atakaye kumtukuza, ampandishe juu ya frasi, amwongoze katika njia kuu ya mji, atangaze mbele yake, Hivyo ndivyo atakavyofanyiwa mtu Sultani atakaye kumtukuza." Sultani akasema, "Haya, twae nguo na frasi pia, kama ulivyosema mwenyewe,

Digitized by Google

ukamfanyie vivi hivi Matakasi, yuko mlangoni mwa Sultani. Usikose hatta neno moja." Hamani akazitwaa nguo na frasi pia, akamvika Matakasi, akamwongoza kwa frasi katika njia kuu ya mji, akatangaza mbele yake, "Hivyo ndivyo atakavyofanyiwa mtu, Sultani atakaye kumtukuza." Alipokwisha kurudi, akaenda kwake kwa haraka, mwenyi uso umefunikwa, akawapasha wenzake habari. Wakamwambia, "Yule Matakasi atakushinda." Marra Hamani akaitwa aende kula na Sultani, Sultani akamwambia Ester katika karamu, "Wataka nini?" Akajibu, "Nataka nipone mwenyewe na watu wangu. Kwani tumeuzwa tuchinjwe wote pia na adui yetu." Sultani akamwuliza, "Nani yule adui yenu?" Akasema, "Mbaya huyu Hamani ndiye." Sultani akaondoka kwa ghathabu, akatoka kutembea kidogo katika bustani. Hamani akashikwa na hofu akamwomba Ester, asichinjwe mwenyewe. Sultani akarudi akaona naye Hamani ameanguka kitandani mwa Ester. Sultani akasema, "Hatta atamfanyia malkiya jeuri?" Wakamfunika Hamani uso, wakasema, "Uko msalaba kwake huyu tayari." Sultani akasema, "Msulubisheni bassi." Wakamsulubisha. Moyo wa Sultani ukatulia. Akapeleka wajumbe mahali pote pa mamlaka yake na barua kwa Wayahudi, akiwapa ruhusa ya kupigana na kujilinda, ikiwa mtu anataka kuwaua. Wayahudi wakapigana na adui zao wakaua wengi. Wakafanya siku kuu wakati uleule mwaka kwa mwaka hatta kwa leo, ndio siku kuu ya Purim.

(Mambo haya yameandikwa katika kitabu cha Ester, na Sultani Serkisi ndiye Ahasuero, na Matakasi ndiye Mordekai.)

Digitized by Google

## 16. Sultani Serkisi na Wayonani.

Sultani Serkisi akaita maliwali wake wote na wakubwa wake barazani, wafanye shauri la vita kwa Wayonani. Walipokwisha kufanya shauri, akawaagiza killa mtu kukusanya watu wengi, akafanya jeshi kubwa kubwa ajabu mno, hatta kuwa kama elfu elfu marra tatu ao zayidi, watu wa makabila zayidi ya arobaini, na killa mtu amevaa nguo za taifa lake na selaha zake pia. Serkisi akaondoka akafika Dardanels, ndipo mlango mwembamba wa bahari karibu ya Stambuli. Akaamuru watu wafanyize daraja la mashua nyingi, apate kulivukisha jeshi lake kwa Europa. Wakafanyiza. Ikawa thóruba kuu, daraja likavunjika. Serkisi akaghathabika sana; hatta akatuma watu waende wayapige maji yale na mjeledi, mapigo mia tatu, tena kuyatupia pingu za chuma, wakisema, "Enyi maji makorofi, nawalipiza kisasi cha jeuri yenu. Mkipenda msipende, Sultani Serkisi atavuka." Akawachinja wasimamizi wale waliolifanyiza daraja. Marra wakashika kazi tena wakafanyiza madaraja mawili, wakafanyiza hivi. Wakapanga mashua nyingi wakazipambanisha kimbavumbavu safu mbili, safu moja yenyi mashua mia tatu na settini, wakazifunganisha kwa kamba nzuri na nene, wakatia magogo, na juu ya magogo makoko, na juu ya makoko udongo, wakaupigilia, wakafanyiza ua wa fito huko na huko katika madaraja, frasi wasishtuke wakivuka baharini. Na urefu wa madaraja kama mwendo wa nuss u saa. Serkisi akavukisha jeshi lake lote, na muda wa kuvukia muda wa siku saba, wakivuka mchana na usiku. Akasafiri katika barra, akipita pwani kwenda Uyonani, merikebu nyingi sana zikafuatana naye baharini.

Digitized by Google

Miji yote ikamwogopa ikitoa chakula cha jeshi lake, killa mji kwa siku yake, hatta mengi kuangamia mali zao zikitumiliwa mbali, na mito mengi imekauka isiweze kuwatosha watu na frasi.

Wakubwa wa Wayonani wakakusanyika penyi Isimusi ya Korinto, wakafanya shauri ya vita. Bassi Serkisi akafika Uyonani, hana buddi kupita Mlango wa Thermopuli, ndio njia nyembamba sana, milima huko na bahari huko. Wayonani wakasema, Katika pembamba wachache wataweza kupingia njia wengi. Wakachagua Wasiparta kuwa wakuu wa vita, kwani Wasiparta watu wazoefu wa vita kupita wote, wakaenda Thermopuli. Lakini kwa sababu ya siku kuu yao Wasiparta, wachache sana waliokwenda, watu mia tatu tu na mfalme wao Leonida, na Wathespii mia saba, na wangine jumla yao elfu saba bass. Bassi Serkisi alipofikia Thermopuli, aliwakuta Wayonani wamekaa kule kule njiani wakiivizia, nao si wengi, wanachezacheza, wanajitana nyele, ndio kazi yao. Hatta Serkisi akastaajabu, akakaa mwenyewe siku 'nne, akingoja watu wajitoe. Halafu yake akatuma watu wawafunge wakawalete kwake wazima. Watu wale wakapigana na Wayonani wakapigwa sana, wengi wakafa. Na siku ya pili vilevile. Hatta Myonani mmoja mbaya akawaonyesha Waajjemi njia ya kuzungukia katika mlima na kufika nyuma ya Wayonani. Wayonani wakisikia habari wangine wakakimbia, Wasiparta tu waliokaa, ndio watu mia tatu tu bassi na mkuu wao, jina lake Leonida, na wangine mia saba. Na Waajjemi, hesabu yao kupita elfu elfu. Bassi ndipo mapigano makuu. Kwanza Waajjemi wakakaribia wakikatwakatwa kwa panga na Wayonani, wakifanya hofu, wakitaka kukimbia, wakapigwa nyuma na maakida yao na maamiri, wakaendelea mbele, wakashindana tena. Sultani Serkisi amekaa kitini mwake kutazama, akaruka



Digitized by Google

marra tatu katika kiti kwa hofu na kushangaa. Na Wayonani wale washujaa sana kwelikweli, wakapigana kama simba. Kwanza wakachoma Waajjemi kwa mikuke, hatta mikuke imevunjika; tena wakawachinja kwa panga, hatta panga nyingi zimepotea; wakatenda kazi kwa mikono na meno pia. Mwisho Waajjemi wale wengi wengi wakawazunguka Wayonani, watu haba sana, wakawagharikisha kama mawimbi, wakafa (B.C. 480.) Maneno haya yakaandikwa katika kaburi lao palepale walipokufa, "Ee rafiki, nenda zako Siparta, kamwambie, tumezishika sheria zake, tumekufa, bassi."

Waajjemi wakautwaa Atene, ndio mji mkubwa wa Wayonani, akauteketeza moto. Nao Waatene wakauacha mji wao, wakapanda vyomboni wote, ndilo shauri la mtu mmoja mkubwa na mwenyi akili nyingi, jina lake Themistokli, naye akasema, "Boma la miti, ndipo salama." Waajjemi wakapeleka merikebu, wakapigana na Waatene baharini penyi pembamba, wakapigwa sana, merikebu zao zingine zikavunjika, zingine wakatekeza pwani, zingine zikazama. Hatta Sultani Serkisi akaingiwa na hofu, akiona Wayonani walivyo hodari na washujaa, nao watu haba tu, akakimbia hatta kwake kwa haraka. Mahali pale alipopigwa baharini, panakwitwa Salamisi. Baadaye Waajjemi wakashindana na Wayonani marra mbili tu bassi, wakapigwa vile vile. Sultani Serkisi akafa.

Digitized by Google

## 17. Habari za Wayonani.

Watu gani hao Wayonani, waliokwenda vitani peke yao, wakaziokoa inchi za Europa zisitiishwe na wafalme wa mashariki? Kwa asili yao Wayonani ni mbegu moja na Warumi na makabila yote ya Europa, na mbegu moja na Waajjemi pia na Wahindi; kwani wote kwanza Waariani. Lakini Wayonani mbali sana kwa tabia yao na sifa zao za zamani, na watangalifu kuliko walimwengu wangineo, kama Wayahudi, kama Warumi.

Wayahudi ndio waliojaliwa kumjua Muungu na kushika ibada yake na kutazamia kwa saburi mambo mema yatakayokuja. Warumi ndio waliojiwekea sheria njema, wakazitii wenyewe, wakayatiisha mataifa yote ya ulimwengu wao, wakazisterehisha kwa haki na amani hatta siku nyingi sana. Lakini Wayonani ndio watu wa akili halisi. Hawakupata inchi kubwa wala nzuri sana, inchi ndogo tu yenyi milima mengi, karibu ikazungukwa na bahari, na visiwa vyake vingi. Wakajenga miji mingi pwani, killa mji peke yake ukishika shughuli zake; wakawa watu si wengi, lakini hodari kwa biashara, na hodari kusafiri vyomboni, na hodari kwa vita zao wenyewe. Hawakupatana vema, illa kwa neno moja tu, ndio kujiona sana kuwa ndio wastaarabu peke yao, na walimwengu wote wangineo kama washenzi na watumwa; wakawataja wote wasio Wayonani jina moja tu, ndio Baribari, maana yake washenzi wasiojua kunena. Hatta kwa vita hawakusayidiana sana, labuda wangalifarikiana kabisa, illa kwa sababu ya mambo manne. Wote walikuwa na lugha moja; wote walikuwa na dini moja; wote walikuwa na siku kuu moja waliyoathimisha sana, ndiyo ya michezo na mashindano penyi mji Olimpya;

Digitized by Google

na wote wakaheshimu sana utenzi wa Homero. Bassi Wayonani walitawanyika sana, wakakaa visiwani mwa bahari Arkipelago, wakajenga miji pwani ng'ambo ya pili ndio Anatolia; wangine wakavuka bahari Adriatiko wakajenga pwani katika Italia upande wa kusini, wakapaita Uyonani mkuu, na katika Sikilia; hatta na Marselz katika Ufransa ulikuwa mji wa Wayonani. Wasisahau lakini kama Wayonani ndio taifa moja lenyi akili kupita wote. Bassi mtu atakaye kusikia zayidi habari za tabia yao Wayonani wa zamani, walivyokuwa hodari na wenyi akili, asome hadithi hizi zifuatazo.

---

## 18. Hadithi ya Ulisse.

Homero Myonani aliyoitunga kwa mashairi mengi na mazari zamani sana, imepata kama miaka elfu tatu.

### 1. *Ulisse na mtoto wake.*

Palikuwa na mtu mmoja Myonani, jina lake Ulisse, mfalme wa Ithaka, ndicho kisiwa katika bahari Mediterraneo karibu ya Uyonani, na mkewe jina lake Penelope. Wakazaa mtoto mmoja wa pekee. Yule mtu akawapenda sana na mkewe na mtoto wake. Wakakaa siku nyingi. Hatta mfalme mkuu wa Wayonani akafanya vita, akawaita wafalme wote walio chini yake, akatuma majumbe kwenda kumwita Ulisse.

Hakukubali Ulisse kuwaacha mkewe na mtoto wake, akafanya hila akajifanya kuwa mwenyi wazimu, hatta akaenda pwani akilima mchanga.

Digitized by Google

Na kulima kwake ndio kwa ng'ombe wawili wakikokota jembe kubwa kama jisu. Wajumbe wale wakamkuta analimalima mchanga huko pwani. Ndio kazi yake. Wakafanya shauri wapate kumfahamu, ana wazimu kwelikweli ao mzima. Wakatwaa mtoto yule wa pekee, wakamchukua pwani, wakamweka pale pale katika mchanga mbele ya ng'ombe. Naye babaye hakupenda kumkanyaga mtoto wake, akageuka kidogo katika njia yake ya kulimia, akapita upande. Bassi wajumbe wakamtwaa, wakampeleka vitani.

2. *Vita katika Troja.*

Wayonani wote wakapanda vyomboni, wakasafiri mbali baharini, wakapigana na watu wa Troja, ndio mji karibu na Stambuli, miaka kumi, wasiwashinde. Wakachoka sana wakataka kwenda zao. Wafalme wakaona haya kurudi kwao, wasipouteketeza mji kwanza. Naye Ulisse akawa mwenyi akili sana, akafanya shauri, wasipoweza kushinda kwa nguvu washinde kwa hila. Akawaambia wafalme shauri lake, wakalikubali. Bassi wakaunda frasi mkubwa ajabu kwa mbau, nao wazi ndani, hamna kitu, nafasi tu. Wakaweka ndani yake watu hodari arobaini wenyi selaha, wakamwacha frasi amesimamishwa kule pwani, wakapanda vyomboni, wakaenda zao si mbali. Watu wa mji walipoona Wayonani wanakwenda zao, wakatoka kwa furaha, wakashangaa wakitazama frasi yule mkubwa anasimama pwani. Hatta mtu mmoja mkohani akaingia shaka, akampiga frasi mkuke katika matumbo, yakalia wazi. Akalia, "Hiyo ndio hila." Marra majoka mawili makubwa wakapanda baharini wakamshika yule mkohani na watoto wake wawili pia, wakawasonga; wakafa. Watu wa mji wakaogopa, wakasemana, "Frasi huyu amewekwa wakfu. Haya tumpan-

dishe mjini." Wakampandisha wote pamoja, na wazee na vijana na waanake na watoto, wakikokota kwa kamba wakishangilia na kufurahi. Hatta panapo usiku watu wale waliomo ndani wakatoka, wakawasha moto mkubwa, ndio ishara kwa wenzio warudi, wakaufungua mlango wa mji. Wayonani wakarudi pwani upesi, wakautwaa mji, wakauteketeza moto.

### 3. *Ulisse na Wakikoni.*

Mji Troja ulipokwisha haribika, Wayonani wote wakapanda vyomboni wakafunga safari kwenda kwao. Naye Ulisse akachagua watu akawapakia vyomboni, akaenda zake, akitamani sana kwa nafsi yake kumtazama mkewe na mtoto wake wa pekee, aliowaacha huko kwake. Pepo zikamsukuma kwa inchi ya Wakikoni, akashuka pwani, wenziwe wengi wakafuatana naye; wakapigana na Wakikoni wa mji wakawashinda, wakauteka mji, wakatwaa mateka, wakayagawanya, killa mtu akipata sehemu yake. Hatta Ulisse akawaonya kuingia vyomboni kwenda zao, nao hawakukubali. Wakakaa kitako pwani wakafanya karamu wakala wakanywa mvinyo. Bassi Wakikoni waliobaki wakaenda kwita wenzio waliokaa barani; wakaja watu wengi na wenyi frasi, wengi wengi kama mchanga, kama majani. Wakapigana sana, wakitupiana na mikuke ya shaba mchana kuchwa. Hatta jua lichwapo Wakikoni wakashinda, wakachinja watu wengi wa Ulisse; nao wangine wakakimbia wakaokoka vyomboni.

### 4. *Ulisse na Walotofagi.*

Wakashika njia baharini wakafika inchi ya Walotofagi, ndio watu wenyi kula loto. Ile loto ni boga, na boga hilo kazi yake hii. Killa alilaye boga lile,

Digitized by Google

marra moja amekwisha kuisahau inchi yake, hatamani kurudi kwake hatta kidogo, illa kukaa tu na kula loto. Ulisse na wenziwe wakashuka pwani wakapika chăkula. Akatuma watu watatu kwenda kuzumgumza na Walotofagi, wapate habari zao. Walotofagi wakawakaribisha, wakawalisha loto. Walipokwisha kuila loto, marra moyo wao umegeuka, wamesahau kwao. Wakakaa wakikataa kurejea pwani. Wallakini Ulisse akaamuru watu, nao wakawachukua kwa nguvu wakitoka machozi wakiombaomba wakishindana; wakawaweka vyomboni chini wakawafunga sana, wakatweka matanga wakienda zao upesi.

## 5. *Ulisse na Mkuklopi.*

Wakaenda katika bahari kule katika kuja zao hatta inchi ngine, inchi ya Wakuklopi; ndio inchi nzuri sana, huzaa yenyewe mtama na mchele na mizabibu wasilime watu wala kupanda mbegu hatta kidogo. Nao Wakuklopi watu warefu mno ajabu, wenyi mioyo mibaya; hawaabudu Muungu, hawashiki sheria, hawatendeani haki wao kwa wao; hukaa katika milima, killa mtu peke yake akimiliki mali zake; kazi yao kuchunga kondoo tu bassi, na kulà nyama ya waana Adamu. Bassi Ulisse akashuka, akawaambia wenzi wake, "Haya, twende zetu baathi, tukawatazame watu gani wakaao hapa, ni wema ao wabaya." Nao wakatia nanga wakashuka pwani wakatembea.

Hatta wakaona paango kubwa karibu na pwani penyi miti mengi; liko zizi kubwa mbele yake limezungukwa na ua wa miti na mbau hodari sana, limejaa ndani kondoo wengi na mbuzi. Naye mwenyewe hayuko kwake. Ulisse akawaonya watu warudi chomboni illa thenashara tu, nao wakafuatana

Digitized by Google

naye. Wakaingia katika paango wakitazama killa kitu; vimo vyombo jamii nzima, mitungi na ndoo na mabakuli yamejaa maziwa yote. Bassi watu wale wakafanya shauri kutwaa vitu kwenda zao marra moja, lakini Ulisse akawazuia akiwashawishi wakae kuko huko kumngojea mwenyewe. Wakawasha moto, wakatwaa chakula wakapika wakala wakangoja.

Halafu yule Mkuklopi akarudi kwake, mtu mrefu mno mwenyi uso mbaya; ana jicho moja katikati ya paji la uso wake; naye jina lake Polufemo. Akawa analeta kondoo wengi toka shamba, na mzigo wa kuni begani mwake, akawapeleka kondoo ndani ya zizi akazivumisha kuni chini. Tena akalifunga zizi kwa jiwe; nalo jiwe kubwa sana, hatta watu asharini na wawili hawawezi kulichukua. Kiisha kutia jiwe, akawakama mbuzi, akaweka maziwa katika vyombo, akawasha moto; marra akawaona watu wako wanaketi humo paangoni. Akawaambia vikali, "Nani ninyi? mmetokapi? shughuli gani mlio nao?" Wakashangaa wakaogopa sana sauti yake kama ya radi. Hatta Ulisse akamjibu akisema, "Wayonani sisi. Tumetoka katika Troja, tunarudi kwetu. Bassi sisi maskini wa Muungu, twakusihi tupewe ada twende zetu." Akawaambia, "Wajinga ninyi, mmetoka mbali sana kwelikweli nanyi, bado kutujua sisi Wakuklopi hatumheshimu Muungu wala kumwangalia. Kiko wapi chombo chako bassi?" Ulisse akajibu kwa uwongo, akisema, "Chombo kimekwisha vunjika, sisi tu tuliookoka, hakuna mtu tena." Yule Mkuklopi akanyamaza, akawarukia gháfala, akakamata watu wawili akawagongesha vitwa chini, akawararua vipande vipande akawala. Alipokwisha kula akalala usingizi. Ulisse akafanya shauri kwa roho yake, "Nimchome upanga palepale akilala? Lakini hatuwezi kujongeza lile jewe limewekwa huko mlangoni. Shauri hilo halifai."

Digitized by Google

Hatta assubui yule Mkuklopi akiamka akafanya vile vile, akikamata watu wawili akiwala. Alipokwisha kushiba chakula, akaondoka akaenda zake akichunga kondoo mchana kuchwa. Kwanza akaweka jiwe lile mlangoni, watu wasipate kutoka kukimbia. Hatta jioni akarejea, akawarukia akakamata wawili akawararua vipande vipande akawala. Ndipo Ulisse akafanya shauri lililofaa. Marra Mkuklopi alipokwisha kushiba chakula, Ulisse akamtolea mvinyo, na mvinyo ule ndio wenyi nguvu sana, ukatekwa katika mji wa Wakikoni. Mtu akinywa asichanganye maji tele kwanza, marra hulewa. Ulisse akamwambia, "Haya, rafiki, twae kanywe; mvinyo huu ndio mzuri na mtamu sana. Nimeuleta sadaka kwako. Nawe una wazimo, hukaribishi wageni vema." Yule Mkuklopi akanywa akapendezewa mno, akasema, "Haya! lete tena. Nitakupa zawadi yako." Akanywa hatta marra tatu. Ulisse akamwambia, "Jina langu mimi ndilo Hapana mtu. Nipe zawadi bass." Akajibu, "Hapana mtu ataliwa wa mwisho. Ndio zawadi yake." Akalewa Mkuklopi akajinyosha chini chalichali, akikokomoka makombo ya nyama, akalala usingizi mzito. Ulisse akaondoka akatwaa mti, akauchongachonga akachoma moto, akawaagiza wenzi wake waliosalia killa mtu kazi yake na mahali pake, wapate kumsayidia taratibu; akapanda mwenyewe juu ya meza, akaupenyesha mti katika jicho la Mkuklopi, nao mti wenyi moto sana unang'aa, akaushindilia chini, wenziwe wakaushika huko na huko wakapekechapekecha kwa bidii. Jicho likatoka damu na moshi, likiharibika kabisa. Yule Mkuklopi akalia ajabu, akifingirika akijinyonganyonga akipiga kiyowe, asiweze kuuondoa mti katika jicho lake. Hatta wale wakashikwa na hofu wakakimbia wakajificha kimya huko na huko paaugoni. Bassi yule akaondoka aka-

Digitized by Google

watafuta pote akipapasa na mikono; hatta akachoka akakaa, asiwapate.

Ilipofika assubui, Ulisse akafanya shauri. Akawakamatia wenzi wake killa mtu kondoo wawili, nao kondoo wale wakubwa sana, akawafunga kwa kamba, kondoo wawili na mtu mmoja katikati. Halafu yake Mkuklopi akaamka akasema, "Nitatoa kondoo wangu kwenda lisha nje; tena nitawakamata wale wabaya nitawala." Akaliondoa jiwe akafungua mlango wa zizi, kondoo wakatoka na watu wakichukuliwa nao. Akabaki Ulisse tu bass. Akatwaa kondoo mume aliye mkubwa sana mwenyi manyoya marefu, akajitundika chini ya tumbo lake akashika sana ngozi ya kondoo. Naye Mkuklopi akastaajabu kwa sababu yule kondoo mume hakutangulia kutoka zizini, nao ndio desturi yake; akamwambia, "Ewe kwa nini kuchelewa leo? Siku zote umezoea kutoka wa kwanza, leo umekawia nawe." Akamgusa kondoo mume akampapasa pia, asitambue aliko Ulisse huko chini yake anachukuliwa.

Bassi walipokwisha toka wote salama, wakafika pwani wakapanda chomboni wakapiga makasia; ndipo Ulisse alipomwita Mkuklopi akimfanyia thihaka sana. Mkuklopi akamsikia akafika mbio pwani akatwaa mwamba mkubwa akakitupia chombo, asikipate. Mwamba ukianguka majini upande wa pili wa chombo na karibu yake ukakisogeza pwani. Yule Mkuklopi akaruka akaingia baharini akipiga makelele akitupa mawe, asiwapate. Tena akawaita majirani wake waliokaa karibu, wakatoka wengi na warefu mno na wakali, wakaja wakamwuliza, "Unani wee? Huwezi nini?" Akajibu, "Ee rafiki, Hapana mtu aliyeniumiza, Hapana mtu," sababu Hapana mtu ndio jina lake Ulisse alilomwambia. Watu wale wakamcheka sana, "Ah! Hapana mtu! Bassi wee, bassi. Mbona umetuita? Labuda huwezi tumbo.

Digitized by Google

Haya, twende zetu." Wakarudi kwao. Naye Ulisse na jamaa yake wakaenda katika bahari katika kuja kwao.

### 6. *Ulisse na Aiolo.*

Bassi wakaenda hatta wakawasili katika kisiwa. Na kisiwa kimekwitwa kisiwa cha Aiolo, ndio jina lake mwenyi kisiwa. Chaenda juu sana katika bahari, kama mwamba mtupu pande zote, na juu yake boma la shaba na jumba kubwa. Ndipo anapokaa mwenyewe Aiolo na mkewe na watoto wake thenashara, waume sita na wake sita. Naye Sultani wa 'pepo zote, ndio kazi yake kuzitawala.

Wakashuka, wakapanda juu ya mwamba, yule akawakaribisha akawatendea mazuri akiwalisha mwezi mzima, wakakaa raha, wakila wakimpa habari zote za safari yao. Bassi walipokwisha kupumzika katika taabu ya bahari ile, wakaomba ruhusa kwenda zao, wakapewa. Sultani yule akatia pepo zote pia katika mfuko, zisivume njiani safari yao isizuiliwe, akafunga mfuko kwa kwamba akampa Ulisse, naye akauweka ndani ya chombo chini. Wakaenda zao baharini, safari ile ikafanikiwa sana, hatta wakakaribia inchi yao wenyewe.

Bassi wenzi wake Ulisse wakasemana, "Tazama, sisi fukara hahehohe, na bwana huyu mwenyi mali sana. Mfuko ule unani? Umejaa fetha labuda. Haya, bwana akilala usingizi tutamfungulia mfuko wake tutazame ndani tupate kujua, kama imo hazina kwelikweli." Wakangoja usiku, Ulisse akalala usingizi, nao wenziwe wakafungua mfuko. Marra 'pepo zote zimetokea kwa nguvu, zikavirukia vyombo vyote zikivuma zikipeperusha, hatta zikavipeperushia mbali baharini, inchi yao isionekane tena hatta kidogo. Wakasukumiwa na pepo kwa kisiwa kilekile cha Aiolo, wakamtakia safari njema ya pili,

Digitized by Google

wasipate. Yule akawatukana akawafukuza vikali. Wakaenda zao, wakifanya huzuni nyingi ya ujinga wao na choyo chao.

### 7. *Ulisse na Walaistrugoni.*

Wakasafiri wakafika hatta inchi ya Laistrugoni, wakajongezea vyombo pwani penyi miamba miwili mirefu huko na huko, na kati ya miamba mlango mwembamba wa kuingilia bandarini, na bandari iliyomo nzuri sana. Wakavifunga vyombo ndani, Ulisse akapanda juu ya mwamba apeleleze inchi na watu walioko. Akaona mji wenyi boma kubwa, akatelemka, akawapasha wenziwe habari, akatuma watatu kwenda mjini kuupeleleza. Bassi wale watatu wakaenda wakakuta kijana mwanamke anateka maji kisimani, akawaonyesha njia ya kwenda nyumbani kwa babaye. Wakakaribu wakabisha hodi, akaitikia mwanamke mrefu mno, kama mnazi, hatta wakamchukia. Marra yule akamwita mumewe yuko sokoni, akafanya shauri la kuwachinja. Akakamata mmoja akamchinja kwa chakula, wawili wakakimbia. Yule akapiga kelele kwa wenziwe wakaja wakawafukuza hatta pwani. Wakatwaa mikuke na mawe makubwa, wakawatupia watu na vyombo. Watu wakalia sana wakichomwa kwa mikuke, vyombo vikafanya mshindo vikivunjikavunjika kwa mawe. Walaistrugoni wakavua wengi kama samaki, wakawachukua, wakachoma moto wakawala. Chombo cha Ulisse tu kimesalia, naye akaikata kamba, akaenda baharini hima.

### 8. *Ulisse na Kirki.*

Wakasafiri wakaja zao hatta kisiwa cha pili. Ki siwa kile kinakwitwa Aiaia. Wakashuka wakakaa

Digitized by Google

siku tatu. Hatta Ulisse akapanda kilima, akaona moshi. Akachagua watu asharini na wawili waende kupeleleza. Wakaenda katika mwitu hatta wakafika mahali peupe, iko nyumba kubwa na nzuri, wakasikia sauti ya mtu anakwimba ndani. Wakapiga moyo konde, wakakaribia, wakaona mwanamke mzuri anafanya kazi ya kutarizi naye akiimbaimba katika kazi yake. Akawaita, "Karibuni wangwana, karibuni wangwana, kafungueni kinwa." Na mwanamke yule ndiye mchawi; pana katika nyumba chui tele na simba na mbwa wa mwitu wakitembea ndani, nao wamegeuka katika hali ya kuwa waana Adamu kwa uchawi wake, wakawa nyama, wakakaa huko ndani. Bassi Kirki, ndilo jina lake mchawi, akawakaribisha mezani, meza imejaa vyakula vya mali na vitamu. Wakakaa kitako, wakala wote, illa mtu mmoja tu, jina lake Eurialo, naye hakula, amekaa uani nje, kwa maana hatumaini mambo haya kuwa mema. Kiisha kula, mchawi akewapiga fimbo ya uchawi wake, marra wamekuwa nguruwe; akawafunga katika mazizi. Wakawa kama nguruwe uso na mwili na sauti pia, lakini wenyi moyo wa kwanza na akili za kwanza. Yule Eurialo, yule aliyekaa nje huko, akakimbia akampasha Ulisse habari zao. Ulisse akawa mtu mshujaa sana, hana hofu hatta kidogo, akawapenda wenziwe kuliko uzima wake mwenyewe. Akaondoka akaenda peke yake mwituni, jini akamkuta njiani akamwonyesha boga, jina lake molu; mtu akiwa na hilo hapatikani na uchawi. Akafurahi Ulisse akafika hatta nyumba ile nzuri akaingia. Kirki akamkaribisha akimtendea vizuri akimkalisha mezani, tena akamwandalia chakula akatia dawa baya akamletea ale. Naye akiisha kula, akampiga fimbo ya uchawi akisema, "Haya, nenda zizini kwa wenzio ndio nguruwe." Haendi Ulisse, hageuki hatta kidogo, molu ile ginsi ilivyo-

Digitized by Google

mfaa, akavuta upanga wake akamrukia yule mchawi, kama anataka kumua. Kirki akapiga kiyowe E-e-e-e-e ! akaanguka chini, akamnasihi, "Ee bwana, bassi bwana, usiniue. Mimi hapa nitafanya killa upendayo mwenyewe." Akamwapia uapo ulio mkuu. Ulisse akamwambia, "Jambo la kwanza, uwageuze wenzangu kwa hali ya kwanza. Jambo la pili, huna buddi kunipa habari za mwendo wangu, mambo gani yatakayonipata." Kirki akaenda mbio kwa mazizi, akawaleta wale wenziwe, akawapaka dawa killa mtu, wakageuka kwa uso wa kwanza na mwili wa kwanza. Kiisha akawafanyia karamu, wakala wakanywa; akampa Ulisse habari zote za njia atakayokwenda. Akawaambia, "Kua herini.' Wakasema, "Kua heri." Wakaenda zao.

### 9. *Ulisse na Wafu.*

Wakasafiri siku nyingi wakafika hatta mpakani mwa bahari kuu, ndipo inchi ya Kimmeri. Wakashuka pwani, wakatoa kondoo walioleta katika chombo, wakaenda zao kando la bahari hatta kwa mahali paliponenwa na Kirki. Na inchi ile yenyi giza tupu siku zote. Mchana na usiku haliangazi jua huko hatta kidogo wala lichapo wala lichwapo; ulimwengu umefunikwa dayima na mawingu manene na maghubari. Bassi walipokuja kule, Ulisse akavuta upanga mkali, akafukua shimo urefu wake kama mkono mmoja huko na huko. Tena akatoa kafara ya kumimina pande zote za shimo, asali na mvinyo na maji, akanyunyiza unga juu, akasali kwa maneno mengi. Wenzake wawili wakashika kondoo, naye Ulisse akamchinja kondoo juu ya shimo, damu ikaingia shimoni. Marra wafu wakaonekana wengi wengi, wakitoka katika chini ya inchi, wakisongana-songana wakitaka kuionja damu ile, wapate nguvu

Digitized by Google

za kujizumgumza naye Ulisse; Ulisse akawazuia kwa upanga, hakuwaacha kunywa damu, illa taratibu tu na mmoja mmoja, alivyopenda yeye.

Kwanza akakaribisha nabii mkuu wa Wayonani, jina lake Tiresia, akamruhusu kuinywa damu, ndio iliyomwezesha kunena vema; akampasha Ulisse habari nyingi za kusafiri katika kwenda kwake na za hatari zote na misiba pia itakayompata njiani, na habari ya kufa kwake mwenyewe. Wa pili na mamaye akakaribu akanywa akasema naye, akamjulisha mambo ya nyumbani huko katika Ithaka, ndio inchi yake, ya kwamba mkewe anamtamani sana siku zote, hatta na kumkalia matanga yapata miaka kumi na minane; na watu wengi, wakubwa na wengi mali, wakimposa wakimjia siku kwa siku, naye hataki; huwafanyia hila asipatwe nao, hufuliza akitoka machozi na kufikiri yule mumewe yuko katika kupotea mbali ao labuda amekufa; hakuna kufarijika illa wageni wafikapo tu, naye bibi huwakaribisha vizuri huwauliza habari akitafutatafuta mambo ya mumewe, ndio faraja yake. Hatta na mtoto yule wa pekee, sasa amekua, mtu mzima, naye hukaa huzunini akimngojea baba akimtazamia sana akimtafuta huko na huko. Na baba mzee sana amekwenda mashamba anafifia kwa taabu na hamu peke yake, hapendi kula, hulalia magumu, wala hana amwangaliaye. Na habari ya mamaye mwenyewe, ndio amekufa kwa huzuni na kumtazamia mwana wake, ndiye Ulisse, naye haji siku zote.

Ulisse akalia sana akisikia habari hizo za nyumbani akataka kumkumbatia mamaye, asiweze kumshika mikononi mwake, kwa maana yu pepo mwenyi umbo la mwana Adamu, hana mwili kwelikweli, wala hapapasiki. Akajaribia marra ya pili, asimpate, akajaribia marra ya tatu, asimpate. Akalia sana.

Digitized by Google

Pepo wengi wa wenziwe waliokufa zamani wakamtokea wakazumgumza naye wakamwarifu mambo yao, wakimwuliza habari za watu. Kiisha akaondoka, akaenda zake kule chomboni. Wakapanda wakapiga makasia, halafu yake baridi nzuri ikawasukuma katika njia yao.

## 10. *Ulisse na Masairini.*

Wakasafiri siku nyingi, wakawasili katika kisiwa cha Masairini. Na Masairini, ndio waanake wachawi, wabaya sana, wenyi kwimba nyimbo kwa sauti nzuri nzuri isiyofanana na kitu kwa kuwa nzuri. Kazi yao, hukaa pwani, killa apitaye baharini humwimbia nyimbo kwa sauti nzuri na tamu, naye akisikia hakosi marra kuchukia mambo yote mangineyo illa kwenda upesi kuzisikiliza zile nyimbo. Bassi huenda, hukamatwa na Masairini, huliwa. Nako mifupa mengi ya watu huko pwani, chungu chungu.

Siku hiyo chombo cha Ulisse kikakaribia kisiwani kule, upepo ukatulia ikawa shwari, wakapiga makasia, wakafika karibu, wakasikia Masairini wanaimba zile zile. Marra Ulisse akaondoka kwa haraka akatwaa nta, akakata kipande kikubwa, akaikandakanda kwa mikono, hatta na jua likaiyeyusha, akawapaka wenziwe wote masikio pia, wasipate kusikiliza nyimbo za Masairini wanazokwimba. Ndivyo alivyoamriwa kufanya na Kirki. Na tena hivi roho kyae mwenyewe ikataka sana kusikia kidogo. Bassi akawaagiza wenziwe, wakamfunga kwa kamba penyi mlingote, asiweze kujimudu hatta kidole kimoja; nao wakavuta makasia kwa bidii, hawakusikia neno, Ulisse tu aliyesikia wanavyomwimbia; wakamwimbia hivi, "Ee Ulisse, munyi mkuu, karibu karibu, jongeze chombo pwani utusikilize maneno

Digitized by Google

yetu. Hakuna mtu apitaye asitusikilize kwanza, hukaa siku zote wakifurahi wakipata habari tele. Naswi tumesikia sifa zako za vitani katika Troja, tena tunazo habari nyingi za mambo yatakayokuja duniani." Akafanya wazimo, akishindwa na uchawi ule, akataka sana kushuka pwani, hawezi, amefungwa: akawalilia sana wale wenzi wake wamfungue, haifai; wamepakwa dawa killa mtu masikioni, hawamwangalii; akawakonyezea kwa macho, akikunjana uso, haifai. Hatta watu wawili walio rafiki zake sana wakaondoka wakazidi kumkazia kamba; hatta chombo kimekwisha kupitia mbali kidogo, nazo nyimbo hazisikiliki, akili zake Ulisse zikamtulilia akapata hajambo, akamshukuru Muungu.

### 11. *Ulisse penyi Sikula na Karubidisi.*

Wakashika safari, hatta hawana buddi kupita pembamba pa bahari, napo penyi hofu na mashaka sana. Pana mwamba huko na mwamba huko, nafasi haba katikati, maji mengi. Mwamba mmoja mdogo, hauendi juu sana, wenyi hatari chini. Maji yale yakipita kassi, huzunguka-zunguka chini yake, hufanya mawimbi makubwa yakivuma yakitoka moshi yakichemkachemka kama maji yachemkavyo katika sufuria, na shimo kati. Na habari ya shimo, killa siku marra tatu hutoa maji yake kwa nguvu, huyarusha juu, pofu lafika mawinguni; marra tatu huyameza chini sana, maji yakiboromoka chini, hatta na inchi kuonekana chini ya bahari. Zimo mbau na milingote na vipande vya vyombo, vilivyozama na kuvunjika, vyingi. Na mazunguko yale ya maji yamekwitwa Karubidisi, ndilo jina lao.

Mwamba wa pili mkubwa na mrefu, unakwenda juu sawa na laini kama kioo; hapana kuupanda wala kuutelemka hatta akiwa mtu na mikono asharini na



Digitized by Google

miguu asharini; nako chini paango, na katika paango nyama ya ajabu na kuogofya, ndiyo joka; naye mwenyi mikono kumi na miwili na mashingo saba marefu, killa shingo na kitwa chake, vitwa saba, na killa kitwa meno makali safu tatu. Kazi yake kukaa mle ndani, kuvizia vyombo vinapita karibu, marra hutoa mashingo yale marefu, hukamata watu huwameza. Jina lake Sikula.

Naye Ulisse ametangulia kupewa habari yake na Kirki. Bassi walipokaribia wakiona uvumi na kishindo cha mawimbi na moshi pia wakasangaa wakataka kwenda nyuma, wasiweze. Shurti kupitia njia hiyohiyo. Bassi Ulisse akafanya shauri na nafsi yake hivi, "Nifanyeje? Nipoteze chombo na watu wote wenzangu na roho yangu mimi? Naona heri wangine waokoke. Kweli ndio afathali, tupite upande wa paango." Akawaagiza wenziwe na rubani wake wapige makasia sana waepuke mawimbi makubwa, wasogee upande wa mwamba mkubwa. Wakamtii, hawakujua ya paango na yule joka. Bassi Ulisse akavaa selaha, akasimama katika gubeti kungoja mbele, chombo kiko katika kupenya palepale, mawimbi huko mwamba huko, watu wanatazamia mawimbi yakiruka yakizungukazunguka kwa nguvu na mashindo, yule joka akawagundulia, akatoa mashingo yake marefu, akakamata killa shingo mtu mmoja, watu saba, akawatupa humo paangoni kama samaki, wakipiga kiyowe wakimlilia Ulisse. Hatta yeye akasikiliza kelele, asipate kuwaponya. Aona miguu yao tu, wakichukuliwa paangoni, asikia sauti bass. Chombo kikapitia upesi, kikaenda zake. Akalia sana, yeye na wenziwe waliobaki.

Digitized by Google

### 12. *Ulisse na ng'ombe.*

Wakasafiri hatta wakawasili kisiwa chingine, panapo ng'ombe wengi wazuri waliowekwa wakfu. Naye Ulisse alijua habari zao, ya kwamba kumegombezwa kuwachinja ng'ombe hao; mtu akichinja hatta mmoja hakosi kuuliwa mbali. Bassi akanasihi sana wenziwe waendelee mbele wasiposhuka kisiwani kule, nao hawakukubali kupita; wamechoka, wataka kupumzika katika taabu ile ya bahari. Wakapatana naye, wakamtolea nathiri, "Tutakula pwani tutalala bassi; kesho assubui tutakwenda zetu." Wakashuka pwani, wakala wakalala. Ikawa thoruba kuu, ikishinda siku nyingi, hatta hali yao hawana chakula. Ulisse akafathaika, akaondoka akaenda tembea peke yake kidogo apate nafasi ya kumwomba Muungu katika shidda zake na taabu yake. Alipokwisha kwenda, wale wenziwe wakakamata ng'ombe wakamchinja wakamla. Halafu yake Ulisse akarudi, marra nyama ikamnukia vizuri, akajua ng'ombe amekwisha chinjwa. Akafanya hofu rohoni mwake, asitoe neno hatta moja. Wakapanda chomboni wakashika safari, wala hawajaenda mbali, ikawa tufanu tena, chombo kikakamatwa kikichukuliwa na mawimbi huko na huko, mwisho kikavunjikavunjika, watu wote wakazama wakafa, illa Ulisse tu. Naye kwanza kuogolea, akashika mlingote, akaupanda kama frasi, akichukuliwa huko na huko baharini vilevile siku nyingi asijue yu wapi.

### 13. *Ulisse na Kalupiso.*

Akachukuliwa kwa mlingote hatta kwa kisiwa kinachokwitwa Ogugia, panapokaa mwanamke mmoja peke yake, mzuri sana, jina lake Kalupiso, naye zimwi. Akakaa katika paango, mahali pazuri sana

Digitized by Google

pasipofanana na kitu kwa uzuri. Paango lile liko katika bustani yenyi miti mingi na mizuri, na maua rangi zote, na jamii ya matunda, na ndege wengi wakifanya matundu huko wakipiga sauti nzuri. Moto ukawaka ndani, namo manukato, uudi na ubani na mdalasini. Naye mwenyewe kazi yake kutarizi, hutarizi huimbaimba vizuri sikuzote. Ukawa mzabibu mkubwa mbele ya paango wenyi matawi mengi, na chemchemi 'nne zikitoka maji ya baridi zikipita njia 'nne mbalimbali. Pazuri sana pale kwelikweli. Ulisse akapanda pwani kwa shidda, amethoofika kwa kukaa sana baharini. Yule mwanamke akamtokea akamkaribisha akamlisha chakula akamtunza sana siku nyingi. Wallakini Ulisse, hakuna kwake kitu cha kutamanika illa kimoja tu, ndicho kwenda kwa inchi yake yeye, ndicho moyo wake ukitakacho sikuzote, kwa maana amependa sana mkewe na mtoto wake aliowaacha nyuma tokea zamani, nao wanamtazamia na kungojea, wasikome. Na kwenda kwake hakuyamkini; kisiwa kile kimezungukwa na maji, naye hana mashua, hana hatta mabawa, na yule mwanamke humvuta akae naye, hujaribu kumsahaulisha mkewe na mtoto, asiweze. Akakaa kwa nguvu, akitoka machozi akipotea peke yake killa siku pwani akipenyesha macho mbali katika bahari, wala hakuwasahau mkewe na mtoto hatta kidogo. Hatta mwisho yule mwanamke akaamriwa na Muungu amwache Ulisse aende zake asimzuie tena. Naye alipoamriwa hivi, akampeleka mahali penyi miti mazuri, akamtolea samani za serimala, akafanyiza mashua kwa akili. Akakata miti asharini, akapasua mbau, akapiga shoka, akazichonga vizuri akazikaza mbavuni, akatenda kazi hatta akaimaliza mashua. Akafanyiza mlingote na foramali na shikio, akaushua kwa nyenzo, akasafiri furaha.

Digitized by Google

## 14. *Ulisse katika Faiekia.*

Akaenda baharini siku nyingi, siku kumi na nane, yee peke yake na mashua yake katika bahari kuu asipoona inchi, illa nyota tu ndizo alizoangalia sana; hatta hakulala usingizi usiku kucha kwa kusudi asikose kunyosha njia vema akiziangalia sana nyota zile alizomfundisha Kalupiso. Siku ya kumi na nane inchi ikamtokea mbali, moyo wake ukafurahi, ukiona ndio mwisho wa taabu zake. Akakaribia pwani, marra thoruba ikamwangukia, mashua ile ikavunjika vipandevipande, hana kitu cha kushikia, akaogolea; mawimbi yakamtupa mwambani yakamkokota nyuma, hawezi kuushika mwamba vema, ngozi ya vidole vyake ikachubuka. Akaogolea tena, hatta akaona mahali palipotoka mto, akaingia akatoka pwani; naye hawezi kwenda kwa miguu, amethoofika sana, amekonda kwa njaa, amesumbuka sana na maji; akaanguka maguguni akipatikana na ulegevu na usingizi mzito. Inchi ile ni kisiwa, kinakwitwa Faiekia, na mkuu wa kisiwa, jina lake Alkinoo. Binti ya mfalme siku ile ile akaenda pwani na wajakazi wake, wafue nguo mtoni; kiisha kufua, wakacheze mpira; hatta mpira ukatupwa mbali, ukafika penyi anapolala Ulisse. Akaamka, naye hana hatta nguo, zote zimeoza kwa maji; akawatokea uchi mwenyi tawi la majani mkononi mwake, na nyele ndefu zisizony'olewa kitwani. Wakafanya hofu wakakimbia, illa binti yule wa mfalme tu, naye akakaa akamkaribisha vizuri akamwonyesha njia ya kwenda mjini. Kijana yule, jina lake Nausikaa. Mfalme akamtendea mazuri, akamwuliza habari ya mambo yote yaliyompata njiani akamtazamisha mali zake mwenyewe na ngoma ya watu wake na michezo yao na mashindano na tinge pia; halafu yake akampeleka kwake chomboni.

Digitized by Google

### 15. *Ulisse na mke wake.*

Akafika kwa inchi yake ndio Ithaka, akajifanya maskini akaenda nyumbani kwake, apate kutambua kama habari zile za nyumbani zi kweli ao uwongo; wala hakujulika na mtu kwanza, ginsi alivyogeuka kwa safari ya miaka asharini na kwa nguo za umasikini, illa na mbwa wake; naye mbwa mzee sana, hatta alipokwisha kumtambua uso bwana wake akafa. Ulisse akakuta jumba lake limejaa watu wengi wenyi jeuri, nao walevi na washerati, wanamsumbua sana mke wake siku kwa siku wakimposa wakimwangamiza mali zake, wakimtharau mtoto wake. Naye kazi yake kukaa ndani na wajakazi wake, na kumlilia na kumtazamia mumewe. Bassi Ulisse akafanya shauri, akawaua watu wale wabaya, akajulikana na mkewe na mtoto, roho zao zikafurahi, roho zao zikaona kama wamekwenda ingia peponi, kwa roho zao zilivyofurahi. Wakakaa siku nyingi raha na mustarehe. Ndio mwisho.

---

### 19. Kroiso na Solon.

Palikuwa na mfalme wa Waludi katika Anatolia (Asia Minor), na mji wake Sardisi; akafanikiwa sana, akapata mali nyingi nyingi, akasitawi; hatta habari zake zikaenea katika ulimwengu, kama mfalme huyu ndiye mwenyi mali. Na mfalme huyu jina lake Kroiso. Hatta siku moja akafika kwake mtu Myonani naye mwenyi akili nyingi na busara, jina lake Solon. Yule mfalme akamkaribisha furaha akamtendea mazuri, kwa hesabu alijua habari yake ya kwamba Wayonani wote wenyi akili, lakini huyo

Digitized by Google

aliyewapita wote ndugu zake; akasema, "Huyu atayatambua mambo yangu, kama hapana mtu katika ulimwengu aliye heri kama mimi." Akawaagiza watumishi wake waende wamwonyeshe Solon mali zake zote na hasina yake na pambo la nyumba na fetha zake na vitu vyake vyote vizuri na vya thamani. Wakamwonyesha vyote. Vilipokwisha kutazamiwa vyote, yule mfalme akamwita Solon akamwuliza, "Ewe Solon, nimejua habari zako ya kwamba umepita wtu wote kwa kuwa na akili nyingi na busara. Bassi nataka uniambie, nani aliye heri kuliko watu wote uliokutana nao." Solon hakujipendekeza kwa mfalme hatta kidogo, akamjibu, "Ee mfalme, Tello Mwatene, ndiye mtu aliye heri." Yule mfalme akastaajabu akamwambia, "Kwa nini?" Akamwambia, "Kwa sababu ya kwanza, mji wake ukasitawi siku zake zote; ya pili akazaa watoto wazuri na wema, na mambo ya watoto wale mema na habari zao njema siku zake zote; ya mwisho akafa mwenyewe kwa heshima na sifa nyingi, akipigana na adui akiwafukuza. Watu wake wakamzika pale pale alipokufa, kwa heshima na utukufu mwingi." Yule mfalme akasangaa, akasema, "Na wa pili je baada yake yeye?" akiwaza kwa roho yake, "Sikosi kuwa wa pili mimi." Naye akamjibu, "Kleobisi na Biton, Waargi. Vijana hao wenyi jamaa bora na mali nyingi na nguvu tele. Na habari zao ndizo hizi. Waargi wakifanya siku kuu, kwa desturi za siku kuu wakataka kupeleka mama wa vijana wale hekaluni katika gari la ng'ombe wawili, ng'ombe hawapatikani, wakatafuta wasiwapate. Wale vijana wakasikitika, kwa maana heshima yake inakwenda kumpotea mamao; wakafanya shauri wakampandisha mamao garini, wakakokota gari kwa kamba mwendo si haba, hatta wakafika kule hekaluni. Watu wakawasifu wakishangilia, mamao akafurahiwa sana

Digitized by Google

watoto wake walivyofanya kazi bora; hatta akamwomba Muungu, waanawe wale wajaliwe kupewa kitu kilicho heri kuliko vyote. Bassi kiisha kufanya siku kuu, vijana wale wakalala wasiamke tena. Ndio waliojaliwa na Muungu." Yule Kroiso akakasirika akamwambia Solon, "Bassi kwa nini kutharauliwa hali yangu mimi? Haifai hatta neno?" Akajibu Solon, "Ee mfalme, fikiri kwanza ginsi yabadilikavyo mambo ya waana Adamu siku kwa siku. Labuda mtu atajaliwa kukaa miaka sabwini, ndio kama siku elfu asharini na tano, na hamsi mia, na siku hamsini. Na watu hubadilibadili siku kwa siku katika hali yao. Bassi gissi gani kusema heri huyo na huyo, kabla hajaisha maisha yake?" Yule mfalme asitulie; hatta akamwondoa Solon, akiona shauri lake, ndilo siku zote kungojea mwisho, maneno tu.

Akakaa siku nyingi akajifurahisha moyo kwa milki yake na mali zake pia, hatta mwisho akapatikana na taabu nyingi, akajua Solon ndiye mwenyi shauri jema kweli kweli. Kwani Kuro, Sultani wa Waajjemi, akaondoka akapigana na Waludi akawashinda sana; akateka mji wao mkubwa, ndio Sardisi, akamtwaa Kroiso, akamfunga; wakaleta kuni wamchome moto kule kule. Naye Kroiso akafahamu sana maneno ya Solon alivyomwambia sikuzote kungojea mwisho, akamwita jina lake marra mbili kwa uchungu na huzuni, "Ee Solon, Ee Solon." Kuro akasangaa akaamuru afunguliwe kwanza kidogo, akamwuza, kwa nini anamwita Solon. Naye Kroiso akampasha habari za yote yaliompata, na ginsi Solon alivyokataa kumnena yeye mtu aliye heri. Kuro akafikiri mambo ya waana Adamu, kama hubadilibadili siku kwa siku, akaona huruma sana, akamwacha Kroiso; halafu yake akamkaribisha mezani kwa chakula akamtendea mazuri.

Digitized by Google

## 20. Lukurgo na Wasiparta.

Zamani za kwanza palikuwa miji miwili katika Uyonani iliyo mikubwa, ndiyo Siparta na Atene. Na watu wa miji hii mbalimbali kwa tabia na desturi zao; wote wenyi akili, lakini Waatene wakazidi kujifunza na kuyafanya mambo yote mazuri na ya kustaarabu, wakipata sifa njema kwa mambo haya isiyopitika na wangineo; Wasiparta wakajizoezea vita tu bass. Na habari za Wasiparta ndizo hizi.

Wasiparta watu washujaa sana, wakakaa kwanza upande wa kaskazini wa Uyonani. Wakaondoka wakaenda kwa kusini, wakipiga watu wa inchi wote waliowazunguka. Na inchi waliyoifikia ndiyo Lakonia katika Uyonani. Walipokwisha kuwapiga, wakawatuma kulima mashamba, wakakaa mjini wenyewe. Na Wasiparta haba, Waheloti, ndio watu wa asili, wengi.

Hatta paliondokea mtu mmoja, jina lake Lukurgo, mwenyi kuupenda sana mji wake na watu wake; akawatengenezea mambo yao yote na desturi zote kwa ginsi wapate kukaa salama wakizungukwa na adui, wenyi hali njema na daraja bora. Akatengeneza hivi. Alifanyiza mji mzima kuwa kama ngome, na watu waliomo kama asikari, jeshi moja na jamaa moja. Hawafanyi biashara, hawasomi illa kidogo tu, hawakai nyumbani, hawasafiri baharini. Hujiweza roho, hushika kadiri na taratibu, hujizoeza miili kazi zote ngumu na za bidii na zifaazo kwa vita, huzaa watoto wazuri na hodari, hukaa pamoja, hula mamoja, hustahimili misiba yote, hupigana hatta kufa, bassi.

Digitized by Google

Tumehadithiwa kama Lukurgo akageuza mapesa yao yote kuwa vipande vya chuma, vikubwa na vizito, killa kipande rahisi sana, kasidi awakatizie gharama zote; kwani kuwa na mapesa ndio uthia na kulemewa. Hatta mtu akitaka kulipa hesabu ya reale miteen, hawezi; angeijaza vile vyuma nyumba pia; akinunua kitu cha thamani angetaka ng'ombe wawili, waichukue mali yake.

Meza za kulia, waanaume huandikiwa meza wazi, killa meza yenyi watu hamstashara ao asharini; chakula mchuzi mweusi na unga na mvinyo na tende na kitoweo bassi. Mtu amechelewa kuja mezani, hukaripiwa; mtu asipokuja, hutiwa athabu. Hatta mkuu wao mmoja alipopiga sana adui, akirudi mjini mwenyi heshima nyingi na kusifiwa sana, akataka siku ile ile tu kwenda kwake kula na mkewe. Wakuu wangine hawakubali, hawampi posho lake la chakula. Naye akafanya hasira, akakataa kazi, wakamlipiza fetha. Wakiingia mezani aliye mzee huuonyesha mlango akisema, "Neno litakalonenwa hapa ndani, lisitoke nje." Mazumgumzo mengi walapo, na bishi na mizaha. Hatta ndio sifa ya Wasiparta, kusema maneno haba, lakini merevu.

Siku moja mtu akaja barazani, akiwaomba sana wamsayidie katika vita, akitoa maneno mengi mengi na mazuri. Wakamwambia, "Maneno mengi mno." Akaenda zake yule mtu akaleta mfuko mtupu, hamna kitu ndani, akauweka mbele yao akisema maneno matatu tu, "Mfuko unataka ngano." Wakamwambia, "Nayo maneno mengi. Kwa nini kuunena mfuko? Hatuna macho?"

Wasiparta wakapigana na Waatene marra nyingi. Bassi siku moja Mwatene akawacheka Wasiparta kwa sababu panga zao fupi, akisema, "Panga hizo! Ah! fupi mno! Naona zinalika." Akajibiwa, "Hazikosi kupenya hatta tumboni mwa adui zetu."

Digitized by Google

Palikuwa mtu akamjia Lukurgo akamtolea shauri, ya kuwa haifai Wasiparta watawaliwe na wafalme, heri watu wajitawale wenyewe. Lukurgo akamjibu, "Nenda zako nyumbani, usitawale huko wewe bwana, watoto watawale na kijoli pia. Naona utalia. Na nyumba za wafalme ndio miji yao."

Tena Lukurgo akauzwa siku moja, "Kwa nini Wasiparta humtolea Muungu sadaka ndogo ndogo na zizi hizi tu?" Akajibu, "Tusikose kuwa na kitu cha kumtolea siku zote."

Tena mtu akamtakia Lukurgo shauri, "Tufanye nini, adui zetu wasitujie?" Akaitika, "Mwe hali ya masikini, msitamani mali nyingi."

Tena watu wakamwambia, "Mji hauna boma. Tufanyize boma bassi?" Naye akasema, "Watu ndio boma; mawe si boma, wala miti."

Palikuwa na mtu, akatoa shauri jema sana, illa kwa maneno mengi mengi na wakati kusipompasa kuzumgumza sana. Hatta mfalme wa Wasiparta akamwambia, "Ee rafiki, hakufai kunena yafaayo wakati yasipofaa."

Vile vile na mtu akakaribishwa mezani kwao Wasiparta, naye mgeni, akanyamaa kimya, hakusema hatta neno, watu wakamsangaa. Hatta mkuu mmoja akawaonya hivi, "Ajuaye maneno mazuri, ndiye ajuaye kwa muda wake."

Siku moja Msiparta akasumbuka na mtu mpumbafu, akiulizwa marra nyingi, "Nani aliye mwema sana katika Siparta?" akajibu, "Asiyefanana na wewe bassi."

Wasiparta wakaupenda sana mji wao, hatta na wakajithania kuwa wamezaliwa kwa hesabu yake tu. Wakienda kwa vita, wakishinda hurudi, wasiposhinda hawarudi, hufa pale pale. Ndivyo walivyofanya simba wale waliopigana katika Thermopuli. Hatta na mwanamke aliyefiwa na watoto wake wawili

katika vita, nao Wasiparta wameshindwa, jirani wakamwambia, "Huwalilii?" Akasema, "Siwalilii mimi. Wangalirudi wazima, ningaliwalilia."

---

## 21. Masultani ya Wayonani.

Zamani za kwanza palikuwa wafalme katika miji ya Wayonani. Wasikubali lakini kutawaliwa na mtu mmoja wakasema, "Afathali wakuu wote watutawale, kwani ndio jamaa za mashujaa ya zamani, wanajua tena desturi zetu na sheria." Wakuu hao wakapata nguvu na mali, wakawatharau watu wakawaonea. Watu wakajiona hali yao kuwa mbaya sana, wakawaondokea wakuu wakawaondoa wakachagua mtu mmoja wao wenyewe kuwa mkuu. Ndio mwanzo wa kuwa masultani katika miji mingi ya Uyonani. Kwani watu wale waliochaguliwa kuwa masultani kwanza waliwapendelea watu wenzio, halafu wakapata asikari, wakawa kama wafalme wa mashariki. Masultani hao wakali sana, na wenyi enzi kuu na asikari wengi. Wakawaonea rayia zao, wakawatwalia mali, hatta wakawachinja killa wapendapo. Palikuwa na Sultani mmoja wa Korinto, jina like Periandro, akawa kwanza mwenyi nia njema. Halafu yake akataka kuweka imara enzi yake, akatuma mjumbe kwa Sultani mwingine, aliye rafiki yake, jina lake Tharasibulo, akamwuliza shauri. Naye hakujibu hatta neno, aondoka tu, atoka yeye na mjumbe yule, wakatembea katika mashamba. Kulikuwako mtama tele umeauka kule mashamba. Wakatembea wale wawili, yule Sultani akamwuliza habari za njiani, naye Sultani

Digitized by Google

mwenyi fimbo akivunja killa suke lililo juu ya wenziwe, akafuliza vivi hivi, anatembea anamwuliza maneno mengi, anayavunjavunja masuke yaliyofika juu sana. Hatta mjumbe akastaajabu, akaenda zake akampasha Sultani wake habari, ya kwamba Sultani yule alitembea shamba, alivunja masuke bassi. Periandro akafahamu, shauri lake halikosi kuwa hili, "Uwachinje walio wakuu, utakuwa imara." Akafanya hivyo. Akatawala kwa nguvu miaka arobaini. Asipate raha lakini, akageuka mkali na mbaya sana, akamua mkewe, na waanawe aliwaondosha. Mwisho akafariki.

Hatta na Waatène walikuwa na Sultani yao, jina lake Pisistrato; lakini hakuwaonea sana, akafanya mengi mazuri, akitengeneza njia, akileta maji mijini kwa mfereji, akipamba mahekalu na majumba ya serkali, akikusanya mashairi na utenzi wa Homero akiyasahihisha sana. Waatene wakamkubali, kwani Solon mtu mmoja wa akili nyingi (yule yule aliyemwendea Kroiso akampasha shauri njema), amekwisha kuwapatia Waatene sheria nzuri na desturi za haki, Pisistrato hakuzitangua sheria za Solon, akazishika kwa kadiri yake. Na sheria za Solon zilizo kuu ndizo hizi. Mtu wa Atene yo yote asiuzwe utumwani kwa sababu ya deni. Mtu asiuze mtoto wake. Killa Mwatene ashariki mambo ya serkali kwa kadiri yake, akawe mtu wa baraza kubwa. Na kazi ya baraza kubwa ndio (1) killa mwaka kuchagua watu kumi kuwa wakuu wa Serkali, (2) kukubali ao kukataza sheria walizotengenezewa na wakuu, (3) kuwahukumia wakuu wasipozishika sheria (B.C. 600).

Palikuwa na mkutano wa kale sana katika Atene, ndio jamii ya watu wa cheo bora waliofanya mashauri juu ya kilima Areopago wakaheshimiwa sana na watu, kama baba zao. Solon akawaongezea heshima, kwani

Digitized by Google

alisema, Hao watazuia baraza kubwa wasikate neno lo lote kwa haraka wala kuupasha mji wote hasara.

Akawapa nguvu ya kukataza sheria yo yote isiyofaa, na kurudi Waatene waliotenda mambo yasiyofaa.

Waatene wakafurahi sana wakamtukuza Solon, wakazishika sheria zake siku nyingi, wakazitengeneza zayidi.

---

## 22. Waatene.

Waatene walipokwisha kupiga Waajjemi katika Salamisi wakafanikiwa sana wakapata daraja bora juu ya Wayonani miaka mingi. Wakalipata hivi.

Wayonani waliogopa Waajjemi watarudi halafu vile vile na jeshi kubwa kubwa, watawajia watawapasha taabu nyingi. Wakasema, "Haifai hali hii ya kukaa killa mji peke yake, mji mmoja hauna nguvu, tutaharibika mmoja mmoja. Bassi tupatane sisi kwa sisi." Wayonani wale wengi wamekaa katika visiwa na miji ya pwani. Wakaafikana kutengeneza na kuweka tayari vyombo, killa mji kwa kadri ya ukubwa wake na mali zake. Na shauri la vyombo, wakija Waajjemi vyote vitakusanyika marra kwa vita. Waliotengeneza vyombo vyingi ndio Waatene, kwa hesabu ya mji wao kuwa mkubwa na watu wengi.

Wakakaa siku nyingi. Waajjemi hawaji tena. Wayonani wangine wakachoka kuweka tayari vyombo kwa vita, wakataka kukaa raha na kufanya biashara. Vyombo vile uthia tu. Bassi wakaja kwa Waatene, wakisema, "Vyombo vyenu vyatosha. Naswi tusitoe vyombo, tutoe fetha, ndiyo tutakayo, tupate kukaa

Digitized by Google

raha. Nanyi twaeni fetha zile, mzitumie kwa vyombo." Waatene wakawaambia, "Toeni fetha bassi." Akawa mtu mmoja Mwatene, jina lake Aristide, naye mwenyi moyo sawa na wa haki. Akawaamua watu, akawafanyia hesabu ya fetha, killa mji kwa kadri ya ukubwa wake na mali zake. Na hesabu zile sawa sawa barabba, watu wote wakawa rathi. Aristide akapata heshima nyingi ya kazi hiyo, hatta kwitwa jina lake, "Mwenyi haki." Na fetha zile huwekwa mwaka kwa mwaka katika kisiwa kimoja kidogo kilichofanywa wakfu na Wayonani wote, ndicho Delo.

Wakakaa siku nyingi. Waatene wale wakazidi kuwa na nguvu nyingi na vyombo vyingi. Mji usipotoa fetha yake taratibu, huupiga huulipiza ushuru. Hivyo walivyopata kuwamiliki Wayonani karibu wote waliokaa katika visiwa na miji ya pwani. Mji ukiasi, hupigwa, si yote mamoja, mmoja mmoja tu, ndio werevu wao. Waatene wakasitawi sana, miji mingi ya Wayonani wakiwatumikia, wakitoa ushuru.

Ndizo siku zao Waatene, tangu B.C. 480 hatta B.C. 430. Wakawa na mali mengi na watumwa wengi. Wakapamba sana mji wao, wakajenga mahekalu mazuri na makubwa kwa mawe ya marmár, wakaweka juu mfano wa muungu wao mmoja, (Waatene huabudu miungu mingi ya uwongo,) wakaufunika thahabu. Ndiyo siku walipoondokea waalimu na mafundi wale bora wenyi jina na sifa na kuheshimiwa na watu wote hatta leo. Kwani akili za Waatene si ginsi moja, ginsi nyingi,—akili za kutunga mashairi na utenzi, akili za kutawala na mambo yote ya serkali, akili za kufikiri na kueleza mambo ya ulimwengu na ya waana Adamu, akili za kunena na usemaji mzuri, akili za kupambanua na kufanyiza yote yaliyo mazuri mazuri, uzuri wa rangi, uzuri wa

Digitized by Google

mchoro, uzuri wa nakshi, uzuri wa kazi zote za fundi. Hatta leo mtu akitaka kupata akili za kuchagua vema mazuri, hana buddi kuwakimbilia Wayonani wa zamani, na kuokota mabaki na masalio ya kazi zao nzuri na kuziangalia na kuzifikiri, hivyo apate kuwaiga Wayonani na kusitawisha akili zake kwa mambo ya ginsi hii. Tangu siku zile, hakuna mtu aliyepita Homero na Sofokli kwa kutunga utenzi na mashairi mazuri, wala Fidia kwa kazi nzuri za kuchora mawe na kunakishi, wala Apelli kwa kupiga vizuri sanamu za rangi, wala Perikli kwa kutengeneza mambo ya serkali na mashauri ya akili, wala Sokrati kwa kuongeza watu katika adili na haki, wala Plato na Aristoteli kwa mawazo ya hekima na akili, wala Demostheni kwa usemaji na uzuri wa maneno.

Watu hao majina yao na sifa zao zimeenea katika ulimwengu wote hatta leo, wala haziishi.

Na desturi za Waatene ajabu, si kama Wasiparta. Killa mtu huwaachia watumwa kazi zote za nyumbani, hujifunga kwa kazi za serkali. Hakuna kathi kwao, killa mtu kathi kwa zamu yake, hukaa barazani huamua wenziwe wakitetana. Ndio kazi walioipenda sana Waatene wote. Hakuna mfalme kwao, killa mtu mzima kama mfalme, hujishughulisha na mambo ya mji na ufalme. Siku kwa siku wote walio wazima hufanya baraza kuu, hukusanyika mahali, hufanya shauri hili na hili, hutoa maneno; tena watu wengi wakitaka hivi ao hivi, bassi jambo limekatika, watu huenda zao.

Na michezo yao mizuri. Hujizoeza sana miili yao killa kazi nzuri na ya kufaa, ndio kuruka, kupiga mbio, kupigana mbavu, kupigana mikono, na zinginezo. Na hii ndiyo iliowapendeza sana. Uko mjini uwanda mkubwa sana wa kuweka watu hatta thenashara elfu, umeviringana, wenyi madaraja mengi ya kukalia yakienda juu kwa juu pande zote. Bassi

Digitized by Google

wakifanya siku kuu, huenda ndani watu wote, hukaa madarajani, hudumu mchana hatta kuchwa wakisikiliza wakitazama watu wakiimbaimba vizuri katikati ya uwanda, wakipiga ngoma, wakisumulia hadithi kwa mashairi, wakicheza kama vinyago.

Bassi Waatene wote, wakubwa hatta wadogo, watajiri hatta maskini, wote hodari sana, wote wenyi akili.

Wakapigana na Wasiparta miaka mengi, wakashindwa, ufalme wao ukapunguka.

---

## 23. Sokrati.

Palikuwa na mtu katika Atene, mji mkubwa wa Wayonani, jina lake Sokrati, naye mwalimu mkuu. Desturi yake kutembea huko na huko mjini, kuongea na watu, akiwasikiliza akiwauliza. Ndivyo alivyowafundisha siku zote. Hatta akaona mwenyewe ameaminiwa kazi hiyo na Muungu, maulizano na majibizano. Kwa sababu siku moja mwenzake kijana akaondoka akaenda kwa hekalu lililo kuu la Wayonani katika Delfo. Killa mtu atakaye shauri jema ao habari za mambo yatakayompata huenda hekaluni kule, hupewa majibu yake kwa mkohani. Bassi yule kijana akatoa swali, ndio, "Nani aliye na akili kupita walimwengu wote?" Akajibiwa, "Sokrati Mwatene." Akaenda zake akampasha Sokrati habari. Naye akafathaika sana. Hazisadiki habari hizo kuwa kweli, wala hakubali kijana yule ameambiwa uwongo. Kwani Wayonani wote wakaona maneno ya mkohani alioko katika Delfo ndio maneno aliyofunuliwa na

F

Muungu. Naye Sokrati mcha Muungu sana. Bassi akaingiwa na mashaka, akasema kwa nafsi yake, "Sina buddi mimi kuyashuhudia maneno haya, Muungu aonekane amesema kweli."

Akaondoka akaenda kuamkia watu waliosifiwa kuwa wenyi akili nyingi, mafundi wa kazi na majemadari na waalimu na watabibu na watunga mashairi na wangineo, akawatafutia habari za kazi zao na elimu yao. Kwanza wakamjibu kwa adabu; halafu yake alipozidi kuwahojihoji sana wakafanya hasira, wakionekana hawana elimu kweli kweli wala kujua vema hatta kazi zao wenyewe. Sokrati akawaacha, akisema, "Watu hawa hujithania wamehitimu, wasijejua neno. Nami najua, kama sijui neno. Ndiyo nijuayo. Bassi ninazo akili kupita hawa. Maneno ya Muungu kweli." Akaondoka akajiweka pia kwa kazi hii ya kuwafathili vema watu wa mji wake, ndio kuwafundisha yaliyowapasa na ya haki. Waalimu wangine wakapata fayida ya mafundisho yao, wakitosa waanafunzi fetha. Sokrati hufundisha killa mtu burre, hataki fetha. Naye maskini, hana mali nyingi, huvaa mabovu, huenda kwa miguu, na uso wake mbaya.

Hatta siku moja mtu mgeni akafika Atene, akajivuna kwa kuweza kupambanua watu kwa nyuso, kama wenyi mioyo mema ao mibaya. Waanafunzi wa Sokrati wakamwita wakamwonyesha Sokrati wakasema, "Tazama huyu. Ni mtu mwema ao mbaya?" Yule mtu akamkazia macho akawaambia, "Mzee huyu mbaya na mgomvi pia." Vijana wale wakamcheka sana, wakijua kama Sokrati ndiye mwema na mtulivu. Lakini Sokrati akawachekelea waanafunzi wake, akawaambia, "Amesema kweli mtu huyu. Roho yangu imelekeana na mabaya, nami nimejiweza roho, nikazishinda tamaa zilizo mbaya. Bassi amesema kweli."

Digitized by Google

Naye Sokrati amesema kweli, akisema anajiweza roho yake. Kwa hiyo tena akawa hodari sana na mshujaa. Hatta akaenda kwa vita kuvizia mji, napo penyi baridi nyingi. Ukawa usiku, na pepo za baridi zimetoka milimani, ikanya theluji, wenziwe hawakustahimili, wakaingia vibandani waepukane na baridi, Sokrati akastahimili, akikaa nje usiku kucha, hana viatu, hana illa nguo moja tu, lakini roho yake hodari, hakubali kuiacha kazi yake aliyoagizwa.

Tena siku moja Waatene wakipigana na adui wameshindwa wanakimbia mbio. Yule Sokrati hakimbii, aenda nyuma polepole na taratibu, akitazamia vikali adui zake, nao wakamwacha, hawamfukuzi, hufukuza wale waliopiga mbio. Akaokoka.

Hatta na siku moja Waatene wakafanya baraza kuu, wakataka kuhukumu majemadari waliokosa katika vita, kwa thulumu si kwa haki. Sokrati amekuwa mkuu wa baraza siku ile ile kwa zamu yake. Bassi akawazuia watu, yeye mtu mmoja nao watu wote wa mji wengi wengi, akawakataza wasifanye yasiyo haki. Wakamghathabikia wakubwa hatta wadogo, wakamtukana, wakamfanyia maogofya, wasimshinde. Mwisho wakamwondoa barazani. Ndivyo walivyopata njia ya kufanya mabaya. Bassi hodari sana Sokrati, akajiweza roho yake.

Akafuliza siku zote kazi yake ya kuongoa watu kwa haki. Hatta wengi wakasumbuka sana, wakafanya shauri wamue. Wakamshtaki maneno mawili, la kwanza, hawaamini miungu Waatene wote wanaowaamini, la pili, huwapoteza vijana tabia zao. Bassi kwa neno la kwanza, hana hatiya mwenyewe, hakosi killa siku kusali na kutoa thabihu kwa wazi, yu mcha Muungu sana, lakini kwa akili si kwa ujinga. Hatta watu hawangalimstaki hivi, illa kwa maana alisema marra nyingi ana sauti ndani yake, imwongōayo kwa mema imzuiayo kwa mabaya, akaiona

Digitized by Google

sauti ile ndiyo sauti ya Muungu akaiangalia sana. Kwa neno la pili, hakupoteza vijana hatta kidogo, akiwafunza mema tu, lakini kwa akili. Bassi vijana wale walioongoka wakaacha desturi na nia zisizo kwa akili, baba zao wasioongoka wakazishika kwa ujinga wao. Ndiyo iliyowachukiza watu wengi, wakamchukia Sokrati.

Sokrati akahukumiwa hukumu ya mauti, mtu asiyetenda illa mema tu, akafungwa gerezani akanyweshwa sumu akafa (B.C. 399). Naye hakuogopa kufa, akafa kikondoo akisema, "Sikatai mimi kufa. Kukiwa kutoa kuwa tu, siko hasara. Kukiwa kwenda peponi kwao waliotangulia kufa, ndiko fayida." Wala hajasikia habari ya kiyama ya wafu, Isa Masiya hajaja, bado miaka aroba mia. Amebahatisha tu kwa kuwa roho yake njema tu, kama mtu aliyejaliwa nuru na kuifuata awezavyo halisi.

---

## 24. Iskander.

Siku zile ulipopunguka ufalme wa Waatene, palikuwa na mfalme wa Wamakedoni, jina lake Filipo, naye Myonani, na watu wake nussu Wayonani nussu washenzi, na desturi zao mbali, wakakaa inchi upande wa kaskazini. Akafanya shauri kutiisha Wayonani wote, na kutawala peke yake. Kwanza akawafitini akaiendea miji yao mmoja mmoja, akaitwaa. Kwani, kama siku zote, Wayonani hawakuwa shauri moja, ugomvi tu na kutopatana. Akaondoka mtu mmoja, ndiye yule msemaji bora kupita wote, Demosthenisi, akataka sana kuwapatanisha kwa maneno yake

mazuri na ushawishi. Asiweze. Filipo akaenda akawapiga Waatene akafanikiwa sana, akawa mfalme mkuu. Hatta akazaa mtoto mmoja mume, jina lake mtoto Iskander, na mtoto yule akawa na moyo mkubwa na mashauri makubwa ajabu tokea utoto wake. Hakubali kitu cho chote kilicho kinyonge, hutaka yaliyo bora na makuu tu. Hatta siku moja watoto wenziwe wakamwita ashindane na watu kwa kupiga mbio. Akawaitika, "Watu gani bassi? Sitaki mimi kushindana illa na wafalme tu." Tena baba yake akiwa anateka miji mengi na kupiga adui zake sana, Iskander akaletewa habari zake akafanya huzuni akasema, "Baba yangu akishindashinda siku zote, hatatuachia sisi nafasi katika ulimwengu ya kutendea makuu na yenyi ajabu."

Akawa mtoto bado, mtu akampelekea babaye frasi mzuri, akataka kuuza kwa reale elfu kumi. Na frasi yule mzuri sana, mkali lakini, hajafugika; hatta mtu hawezi kumpanda wala kumtiisha hatta kidogo, alivyo mkaidi pia. Mfalme akaghathabika, akaamuru aondolewe. Iskander akawako akamwambia babaye, "Wamtiisheje watu woga na wajinga?" Mfalme akamwambia, "Ee mwanangu, gissi gani kutukana watu, usipoweza kumpanda mwenyewe?" Yule mtoto akajibu, "Naweza mimi." Akamwambia, "Kapande bassi." Na yule mtoto ameangalia frasi anastushwa na kivuli chake yeye, akampindua uso kwa jua, akamtuliza kwa sauti na kumpapasa. Halafu yake akampanda akamkimbiza mbio sana, hatta amekwisha kumfuga pia; ndipo mfalme akatambua, mtoto gani aliyemzaa. Wakakaa siku, baba yake akafa, Iskander akawa mfalme, amepata miaka asharini tu kwa umri wake (B.C. 336).

Akaondoka akawatuliza Wayonani kwanza. Alipokwisha, akafanya jeshi kubwa, nalo limezoea kazi zote za vita zamani ya babaye, Filipo. Akavuka

Digitized by Google

kwa Asia penyi Dardanels (napo palepale alipovuka Serkisi kwenda Europa), akawapiga Waajjemi penyi mto Graniko, unakwitwa sasa Kodsha-su, akaipata Anatolia (Asia Minor) yote. Sultani wa Waajjemi, jina lake naye Dario, akakusanya watu wengi, wakapigana marra ya pili penyi Isso katika Kilikia, Dario akashindwa, mkewe akakamatwa na binti zake wawili, kwa shidda akapona mwenyewe. Iskander akapata inchi yote ya Sham, akafanya vita ya miezi saba juu ya mji mkubwa Turo akautwaa. Kiisha akatiisha Wamisri, akaandika misinji ya mji palepale pwani, ndipo Iskanderia hatta kwa leo. Kiishaakaenda mtafuta Darío aliko. Akamwona penyi Arbil, mji wa Sham, na jeshi kubwa sana naye. Majemadari wa Iskander wakafanya shauri la kumgundua Dario usiku. Iskander hakukubali akasema, "Simpigi mimi illa kwa wazi." Dario akaogopa, akataka kupatana naye, akimtolea fetha nyingi na sehemu kubwa ya milki yake na binti yake pia. Hatta jemadari mmoja Myonani akamwambia Iskander, "Nikiwa Iskander mimi, ningekubali," Iskander akamjibu, "Hatta nami ningekubali, nikiwa wewe." Bassi hakupatana naye, akawaangukia Waajjemi kwa gháfala, akawashinda sana ndio marra ya tatu; akatwaa miji yote ya Sultani Dario, na mji ule mkubwa Babel, na hazina zake na mali zake zote. Dario akakimbia, halafu yake akafa.

Na Iskander yule bado hajawa rathi. Akaendelea tena, akapiga watu wa Asia mpaka Hindi, akamiliki inchi yote toka Uyonani mpaka Hindi, ndio milki yake. Akajenga miji akafanyiza bandari, akatengeneza njia, akawajulisha watu wote lugha ya Wayonani na elimu na mathehebu zao za kiungwana, akakalisha Wayonani wangine katika miji ya Asia kwa mashariki, na habari za Asia zikazidi kutambulika na kuenea katika Europa. Na kazi hizo zote

Digitized by Google

akazifanya kwa muda wa miaka thenashara tu bassi; akarudi kwa Babel, akakaa huko siku, akapatikana na homa, akafa kuko huko katika Babel, akiwa amepata miaka thelathini na miwili (B.C. 323).

Na Iskander huyo ndiye aliyefananishwa na chui na mbuzi ndume katika kitabu cha nabii Daniele, kwa maana ya kuwarukia adui zake kwa gháfala na kuwapiga thoruba moja na kuwaharibu wote. Milki yake ikagawanyika sehemu 'nne, wakamiliki majemadari yake wa'nne, killa jemadari sehemu moja, Uyonani na Anatolia na Sham na Misri,—inchi nne. Wakakaa siku si nyingi.

Siku zile mji mmoja wa Misri ukaanza kusitawi sana. Wayahudi wengi walikwenda kukaa humo, na Wayonani wengi; tena mfalme wa Misri, jina lake Ptolemayo, akakusanya vitabu vingi sana vya Kiyonani katika jumba moja, Iskanderia ukapata jina kuwa mji wa maarifa mengi na waalimu wengi. Ndipo Maandiko Matakatifu yalipopata kufasirika Kiyonani, ndipo alipotokea Euklid. Na lugha nzuri ya Kiyonani ikaenea ulimwenguni mwote. Killa mtu asiye mjinga alijifunza lugha hiyo. Hatta Warumi walipowashiinda Wayonani, walijifunza maneno yao na elimu yao, wakazidi kuyaeneza killa walipotawala; mmoja wao akatunga shairi kusema, "Wayonani waliposhindwa, ndipo waliposhinda," kwani wote huwatanguliza Wayonani kwa mambo ya hekima na akili na uzuri. Ndio sababu Maandiko ya Agano Jipya yameandikwa Kiyonani, kwani lugha yenyewe nzuri, tena imeenea sana siku za Bwana wetu.

Na desturi za Kiyonani pia zikaenea, watu wengi wakazikubali. Lakini Wayahudi sivyo kabisa. Baadaye wakaja Warumi wakawatiisha Wayonani na Wayahudi pia, wakaweza sana katika ulimwengu.

Digitized by Google

## 25. Visa vya Iskander.

Palikuwa na mtu Myonani, naye mwalimu mkubwa, jina lake Diogenisi, akakaa katika pipa, ndilo nyumba yake, huvaa nguo mbovumbovu, hula mtama tu, hujipasha uthia siku zote. Ndizo desturi zake. Wayonani wakamheshimu sana. Hatta Iskander akaja kumwamkia, akataka mwenyewe kusifiwa naye kama na watu wangineo. Akamwambia, "Salaam. Mimi ndimi Iskander." Akamwambia, "Salaam. Mimi ndimi Diogenisi." Akamwambia, "Baada ya salaam, nataka sana kukufanyia fathili." Mwalimu akamjibu, "Ondoka bassi. Wanitia kivuli. Sitaki." Mfalme yule akasangaa, akawaambia wenziwe, "Nisipokuwa Iskander, ningependa kuwa Diogenisi," kwa ginsi ulivyompendeza ukinaifu wake.

---

Palikuwa mji wa Asia, uliokwitwa Gordio. Na katika mji ule likawa gari lenyi mti wake umefungwa na kamba fundo la ajabu sana, ginsi lilivyopigwa fundo lile la kamba. Haliwezikani kufunduliwa kabisa, likahadithiwa ya kuwa, "Alifunduaye fundo hili, ndiye atakayemiliki dunia pia." Watu wengi wakajaribu kulifundua, wasiweze. Hatta Iskander akafika kwa mji ule katika kwenda kupiga Waajjemi, akalikata fundo kwa upanga wake. Ndivyo alivyolifundua.

---

Akawa Iskander anafukuza adui zake katika jangwa pasipo maji, wakaona kiu sana na yeye na asikari wake; hatta wangine wakazimia, wote wakafathaika. Wakatafutatafuta maji, wasiyapate illa kidogo tu nayo kwa mbali. Likawa jua kitwani wakamwona Iskander anasumbuka na kiu, wakamletea maji katika ng'ao. Akawauliza, "Nani ninyi mnao-

Digitized by Google

niletea maji?" Wakasema, "Watoto wako sisi tunaokufa. Haithuru, uyanywe bassi. Wangine watazaliwa, nawe mtu wa pekee." Akaishika ng'ao, akawaona asikari wake wanamkazia macho wakitaka sana maji, akawarudishia maji, akisema, "Nikinywa mimi, hawa watazimia roho." Wale asikari wakasemana, "Twende zetu, hatuoni njaa wala kiu, tukiwa na bwana huyo." Wakampenda sana, wakaendelea mbio.

---

Iskander akawa jemadari mkuu kweli kweli, illa hakujiweza roho yake akafanya mabaya mengi, kama haya. Akakamata mtu mmoja, aliyepigana naye kwa ushujaa sana, naye jemadari, akamfunga mzima kwa gari lake nyuma, akakimbiza frasi, yule akakokotwa chini akafa. Akatwaa kwa hila majemadari wake mwenyewe, watu wawili, baba na mtoto wake, kwa sababu aliwathania tu wamefanya shauri juu yake, hakujua vema. Akawasumbua sana akawachinja. Siku moja akalewa katika karamu, akachinja pale mtu mmoja, aliye rafiki yake sana.

Bassi aliweza sana katika ufalme wake, hakujiweza vema mwenyewe.

---

Iskander alipokitwaa Turo, alituma watu kwenda Yerusalemi kwa mkohani mkuu, jina lake Yaddua, na barua ya kusema Wayahudi wajitoe kwake, wasimtumikie tena mfalme wa Waajjemi. Naye mkohani alikataa, akisema amemwapia Dario hatamwasi, hawezi kuuvunja uapo. Asirithike Iskander, akakasirika sana. Bassi alipokwisha kuupiga Turo na Gaza, aliuendea Yerusalemi. Yaddua akafanya hofu sana na juhudi, akawaamuru Wayahudi watoe thabihu wakamwombe Muungu, wapate kuokoka; kwani hatari kubwa, nayo karibu. Hatta Muungu akamwonya kwa njozi asiogope, aupambe mji na kufu-

Digitized by Google

ngua milango, na watu wote kuvaa nyeupe, na Yaddua na wakohani wenzake kuvaa mavazi ya ukohani, na kutoka kwenda kumlaki mfalme Iskander njiani pasipo hofu, kwani Muungu yupo naye. Yaddua akaamka amefurahiwa sana akawapasha watu habari.

Iskander akaja, akawasili hatta mahali pazuri pa kutazama na mji na hekalu pia. Akaona mbali watu wengi wanakuja taratibu, hawana selaha, wote wamevaa nyeupe, na wakohani wamevaa nguo za bafta nzuri, na Yaddua mwenyi uzuri mwingi wa samawati na mwekundu, na kofia kitwani yenyi thahabu iliyoandikiwa Jina la Muungu. Bassi akamwendea peke yake akamsalimu mkohani, akalisujudia Jina. Wayahudi wakamsalimu yeye wakamzunguka. Hatta rafiki zake Iskander wakashangaa mno, wakathani ana kichaa; mmoja wao jina lake Parmenio akamjia akamwambia, "Wewe uliyesujudiwa na wote, wamsujudia mkohani wa Wayahudi?" Akamjibu, "Simsujudii yeye illa Muungu aliyemfanya mkohani. Kwani huko Umakedoni nalimwona huyo huyo katika ndoto, amevaa vivi hivi, nilipokifikiri shauri ya kutiisha mashariki; akaniambia, 'Njoo upesi, leta jeshi, nitakujalia kuwashinda Waajjemi na kuwatawala.' Bassi nami naona itakuwa hivyo." Tena Iskander akashikana mkono na mkohani, wakaenda pamoja na wakohani wote wakifuatana mbio, wakafika Yerusalemi.

Iskander akaingia hekaluni, akatoa thabihu kwa kawaida alivyomwonyesha mkohani mkuu, akatendewa vizuri na heshima nyingi. Akaletewa kitabu cha nabii Danieli, akaonywa mahali palipoandikwa kama Myonani atakuja atauvunja ufalme wa Waajjemi. Akafahamu ndiye mwenyewe aliyebashiriwa tangu zamani akafurahiwa mno. Hatta siku ya pili aliwaita Wayahudi, akawauliza, "Wataka nini?

Digitized by Google

mtapata." Yaddua akamwambia, "Twataka ruksa kuzishika sheria za baba zetu; tena killa mwaka wa saba tusitoe kodi." Akasema, "Vema, na Wayahudi wa Babel vile vile." Alipokwisha, akaenda zake Misri.

---

## 26. Antioko Epifani.

Paliondokea mfalme Myonani, jina lake Antioko Epifani, naye mfalme wa Sham, naye mtu mwenyi makuu mengi naye mbaya sana. Kwanza akapiga Misri. Alipokwisha aliuendea Yerusalemi, na jeshi kubwa. Kwanza akaua watu wengi sana. Tena akaingia hekaluni akavichukua vyombo vitakatifu vyote, mathbahu ya thahabu, na kinara cha meshmaa, na meza ya wonyesho, na vitupa, na vyetezo, na pazia, na taji, na vipambo vingi, na fetha nyingi sana. Akayavunja maboma ya Yerusalemi akajenga ngome, akachukua mateka kama elfu kumi, akaenda zake. Tena baada ya miaka miwili, alitoa amri watu wote wawe hali moja, wote wazishike amri na dini ya kiyonani. Marra akatuma watu kwenda pote katika Uyahudi, kuwalazimisha wote kumtii, kusimikisha mathbahu za miungu yake na mahekalu ya sanamu zake, kutoa thabihu za nyama ya nguruwe, ndio unajisi sana kwao Wayahudi, na kutenda kazi siku ya sabato. Akagombeza watoto wasitahiriwe. Kuwatahiri watoto ndio kuchinjwa, na watoto pia. Akazidi kutoa ukali mno, akaingia hekaluni akaichoma milango akauvunja ukuta, akasimikisha mathbahu ya kiyonani juu ya mathbahu kubwa, akaleta nguruwe wengi, mmoja aliye mkubwa

Digitized by Google

akamchinja juu ya mathbahu, akamimina damu yake juu ya mathbahu na Patakatifu pa Patakatifu, akafanya mchuzi akayanyunyizia Maandiko na Torati, mengi akayateketeza.

Bassi ndio "chukizo la ukiwa;" kwani Wayahudi walikimbia, na thabihu za killa siku zikakoma, na taa kubwa ikazimika, kama Danieli alivyozibashiria siku zile na mfalme huyo mbaya mno.

Na hivi pia tumehadithiwa (2 Makab. 7). Palikuwa mwanamke Myahudi na watoto wake saba. Wakakamatwa na asikari wa mfalme wakashurutishwa kula nyama ya nguruwe, wasikubali, wakapigwa bakora nyingi na mijeledi. Mmoja wao watoto akatoa maneno, akamwambia mfalme, "Watakani kwetu sisi? wajifunzani? Tayari kufa sisi, wala si kuzivunja sheria za baba." Mfalme akaghathabika, akaamuru walete masufuria na masinia yenyi moto sana; tena wamng'oe ulimi na kumkata mikono na miguu, nao ndugu zake na mama yake wakimtazama. Alipokwisha kukatwa, naye mzima bado mfalme akaamuru aletwe motoni akapikwe katika sufuria. Bassi akafaraki dunia, nao nduguze wakafarijiana wafe kwa kiume, kwa kikondoo. Tena wakamleta wa pili, wakamtweza wakamng'oa nyele za kitwani wakamwuza, "Utakula bass? Usipokula, utaumia maungo yote." Akakataa akasema, "Sitaki." Akaathibishwa vilevile. Akasema, "Wewe watuondoa maishani humu, lakini Mfalme wa ulimwengu atatufufua kwa maisha ya milele, tuliozifia sheria zake." Akafariki. Na wa tatu vilevile walimthihaki. Akatoa ulimi marra akainyosha mikono, akasema kwa kiume, "Muungu aliyenipa; kwa ajili yake naitoa, Yeye atanirudishia." Hatta mfalme nao walioko wakaajabu. Akafa huyo, na wa 'nne pia, akisema, "Tukichinjwa na watu, heri kutazamia kiyama ya uzima. Nawe, mfalme, hu-

Digitized by Google

pati." Wa tano akasema, "Wee mfalme, waweza watu, wafanya upendavyo, wathani taifa letu limeachwa na Muungu. Ngoja kidogo, atoe nguvu zake kuu, nawe utalia na uzao wako." Na wa sita, "Usidanganyike, tumestahili haya, tumetenda thambi, ndio maana kutendewa hivi; nawe usiseme, Nimeshindana juu ya Muungu, sipati athabu." Lakini yule mama ndiye ajabu, akiwaona watoto wote saba wauawa palepale, naye akiwafariji akiwatia moyo, akisema, "Sikuwaumba mimi, sikuwafanyiza tumboni, sikuwapa uzima. Bassi Muumba ulimwengu hakosi kwa rehema atawafufua tena, kwani mmekufa kwa ajili yake." Akasema haya kwa kiyahudi, Antioko akathani anamnenea yeye, akajaribu sana kumshawishi yule wa saba aliye mdogo, akatoa uapo kama atampasha utajiri mwingi, na raha, na urafiki pia, na ukubwa, akikubali kumtii. Asikubali yule kijana; mfalme akamwambia mamaye, "Bassi wewe umshauri vema, apate kuishi." Akamsujudia mfalme kwa kicheko, akamwambia mtoto kwa kiyahudi, "Ee mtoto, unirehemie mama yako niliyekuchukua mimba, nikakunyonyesha, nikakulea hatta leo. Kumbuka mbingu na inchi nayo yaliyomo, na Muumba haya yote, Muungu. Wala usimwogope huyu mtesi, ukawafuate nduguzo, nipate kuonana nanyi wote tena baadaye." Alipokisema, kijana akalia, "Wangojani? Sitii amri ya mfalme. Naitii sheria baba zetu waliyopewa na Musa; na wewe huokoki. Mimi natoa mwili wangu na uzima kwa ajili ya sheria za baba zetu, nikamwomba Muungu aturehemie sisi Wayahudi, kwani tumestahili ghathabu yake itulizwe naswi." Akatendewa vibaya kuliko wote, akafa, na mama pia.

Digitized by Google

## 27. Yuda Makabio.

Zamani za Antioko Epifani, palikuwa mtu Myahudi, jina lake Mattathia, naye mkohani, mwenyi watoto watano, akakaa katika mji Modini, upande wa magharibi wa Yerusalemi. Akasikia habari za Yerusalemi ulivyotekwa, na kutiwa unajisi mwingi, akasikitika sana. Akakaa na watoto wake. Ḥatta wakaja akida ya mfalme na asikari mjini mlemle, kuwatiisha watu wamtii mfalme wakatoe thabihu kwa miungu ya uwongo. Wakamjua Mattathia ndiye mkubwa na mwenyi heshima, wakasema, "Bassi tumwite huyo kwanza; halafu wangine watamfuatisha upesi." Mattathia akaenda kwitwa, akaja akakataa kabisa kutoa thabihu. Alipokwisha, marra akatokea Myahudi mwingine akatoa. Jambo hilo likamtia Mattathia uchungu sana, akawatwaa watoto akamrukia yule aliyetoa akamua pale, akamua tena yule akida wa mfalme na asikari si wengi, akaivunjavunja mathbahu, akapaliza sauti akisema, "Atakaye kuzishika amri za Wayahudi na ibada ya Muungu, aje nami." Akakimbia milimani, yeye na watoto wake, akaziacha mali na nyumba. Wengi wakamfuata, wakajificha milimani na paangoni, na waanake na watoto. Jemadari la mfalme akasikia habari akafanya jeshi akawaendea, akataka kuwapatanisha kwa maneno, asiweze; akangoja siku ya sabato, kwani haramu kwao Wayahudi kufanya vita siku ya sabato, akaleta moto akawachoma palepale paangoni kama watu elfu; kwani watu hawakupigana, kwani haramu; wakafa kikondoo. Lakini Mattathia hakuwako. Akatoa amri, Wayahudi wapigane hatta siku ya sabato, wakiwa hawana buddi. Akafanya jeshi naye, akazivunja mathbahu

Digitized by Google

nyingi za kiyonani, akawaua waliomtii mfalme, akawatahiri watoto. Halafu akapatikana na ugonjwa, naye mzee sana, akawaita watoto, akawaonya kwa maneno mengi wazipiganie sheria za Torati hatta kufa; akamchagua Yuda Makabio kuwa mkubwa wao, akafariki, akazikwa Modini (B.C. 166).

Bassi huyo Yuda Makabio mtu mgumu sana kama simba na mwenyi maarifa ya vita. Likaja jeshi la mfalme, akawapiga akawafukuza, akamua jemadari akatwaa upanga wake akavaa mwenyewe mpaka maisha. Likaja jeshi la pili, akawapiga akawafukuza akamua jemadari vilevile. Mfalme akasikia habari ya kwamba Yuda Makabio amepiga majeshi mawili akaghathabika sana. Akatuma jemadari naye mkubwa na jeshi lake kubwa, watu arobaini elfu na wapandao frasi elfu saba. Tena wafanyi biashara ya watumwa wakamfuata wengi kwenda kuwanunua mateka ya vita; kwani wakathani watakuwa wengi na rahisi, reale saba saba. Yuda na ndugu zake wakaona vita kubwa inakuja, wakajiweka tayari. Kwanza wakakusanyika wote wakafunga, wakavaa gunia, wakajitia majifu kitwani, wakazirarua nguo, wakakisoma kitabu cha sheria, wakaleta sadaka, wakamlilia Muungu kwa sauti kuu. Tena Yuda aliwagawanya vikosi vikosi, akaondosha walio wameoa karibu, ao wamenunua shamba, wasifanye woga vitani, wakabaki watu kama elfu tatu. Akasema, "Assubui ndio vita." Lakini usiku alisikia jeshi la adui limetengwa, nussu imekaa, nussu inakuja kumgundulia palepale usiku, akasema, "Heri kuwaendea waliokaa." Wakaenda usiku, wakapiga baragumu wakawaendea gháfula, wakawafukuza. Bassi wale waliokwenda kumgundulia Yuda usiku wakamkuta hako kituoni, wakarudi kwa wenzio, wakaona kumbe wenzio wamekwisha kufukuziwa mbali. Bassi nao wakakimbia, Yuda

Digitized by Google

akatwaa mali mengi na mateka; nao pia waliokuja kuwanunua Wayahudi akawauza.

Likaja na jeshi, la 'nne, kubwa zayidi, la watu settini elfu, na wapandao frasi elfu tano; na watu wa Yuda elfu kumi tu. Yuda akawapiga akawafukuza vilevile. Alipokwisha kuwapiga hao, alisema, "Sasa twende Yerusalemi." Wakaenda, wakaingia mjini wakaona hekalu ukiwa tu, magugu pote na takataka, na mathbahu imetiwa uchafu, na milango imeteketea, wakararua nguo wakajitia mavumbi kitwani, wakapiga baragumu wakalia sana. Tena Yuda alichagua wakohani walio wema wakaipenda sheria, nao wakalitakasa hekalu, wakatoa mawe, na mathbahu iliyotiwa uchafu wakaivunja, wakayaweka mawe pahali, wakajenga ngine, wakazitakasa nyua. Tena wakafanyiza vyombo, na taa, na mathbahu, na meza, wakavukiza uvumba wakaiwasha taa. Wakaisha. Halafu wakafanya siku huu ya kulizindika hekalu, siku nane, wakalipamba hekalu mbele, wakaitengeneza milango. Wakatoa thabihu kwa furaha kuu, wakimsifu wakimwabudu Muungu. Ndivyo walivyofanya Wayahudi killa mwaka baadaye, hufanya siku huu ya kulizindika hekalu kwa furaha kuu (B.C. 165). Na mfalme Antioko amekwenda Ajjemi kufanya vita, akasikia habari za Yuda Makabio alivyopiga majeshi yake, akaona uchungu sana akaugua, ugonjwa ukazidi kumshika sana, akataka kufa. Akawaita rafiki, akawaambia, "Ugonjwa umenishika sana, kwa sababu nimewaonea mno Wayahudi; ndio maana." Akafariki.

Lakini Wayahudi hawajapata raha na kustarehe. Kwani mtoto wa Antioko alifanya jeshi kubwa kuliko yale ya kwanza, ndio la tano, jeshi la watu mia elfu, na wapandao frasi asharini elfu, na tembo waliozoelea vita thelathini na mbili. Na tembo hao ndio ajabu. Juu ya killa tembo ngome ya mbau na

watu waliomo wenyi selaha, na Mhindi mmoja ndiye aliyemwongoza tembo. Tena killa tembo alikuwa na watu elfu, wenyi nguo za chuma, na kofia za shaba, wakamfuata tembo killa aendapo, na tena watu wapandao frasi hamsi mia. Jeshi lote likatawanyika juu ya milima na boondeni liking'aa kwa ng'ao za shaba na thahabu, na uvumi wake mkubwa na kitisho. Asiogope Yuda Makabio, akawaendea akapigana sana. Palikuwa na tembo mmoja mrefu mno mwenyi matandiko ya kifalme. Bassi Eleazar ndugu yake Yuda akasema, "Hakosi mfalme yupo mwenyewe juu ya mnyama," akamwendea tembo kwa ushujaa sana akiua watu wengi huko na huko, mpaka alifika; akapenya chini ya tembo akachoma kwa upanga, akamua. Tembo akamwangukia, naye akafa palepale. Yuda akaona jeshi kuwa kubwa mno akarudi Yerusalemi. Jeshi la mfalme likazunguka Yerusalemi; halafu wakasikia vita iko kwao, wakapatana na Wayahudi wakaenda zao.

Hatta jeshi la sita likaja, na mkuu wake Nikanor, Yuda akalipiga akamua Nikanor. Akachaguliwa kuwa mkohani mkuu. Akatuma wajumbe kwenda kufanya urafiki na Warumi, kwani amesikia habari zao kama taifa hodari mno, na tena wamepiga Wayonani. Warumi wakafurahi, wakafanyana urafiki. Asidiriki Yuda kusikia habari, kwani vita ikaja tena marra ya saba, watu asharini elfu, na watu wa Yuda mia nane tu. Akapigana akauawa akazikwa Modini, (B.C. 161), akapigiwa maombolezo mengi sana. Baadaye ndugu zake wakatawala, wakawa hodari vilevile. Hatta Wayahudi hawakutawaliwa na mtu mgeni miaka mengi, hatta wakati wa Herode; ndipo walianza kutawaliwa na Warumi.



Digitized by Google

## 28. Warumi.

Mwisho wa Wayonani, walitiishwa na Warumi. Na mwisho wa Wayahudi, walipigwa na kufukuzwa na Warumi. Nani hao Warumi, walioweza kuwashinda taifa bora na lenyi akili, Wayonani, wakajaliwa kuuharibu kabisa Yerusalemi, mji na watu wateule wa Muungu?

Kweli habari za Warumi na mambo yao yatupasa sisi sote sana hatta leo.

Mataifa makuu yote ya kale yalitiishwa nao yakageuka kuwa kama watoto na watumwa wao na kuifurahia enzi yao. Mataifa makuu mengi ya siku hizi, ndiyo ya Europa na Amerika, yametoka kwao, kama watoto wakitoka nyumbani kwa baba, wakikaa killa mtu mahali pake mbali mbali, wasisahau walivyolewa vizuri na kushika desturi nyingi na sheria za babazo hatta leo. Tena ufalme wa Warumi ajabu sana, ginsi ulivyoongezeka pole pole kidogo kidogo, ukasitawi ukakaa siku nyingi, miaka kama elfu mbili, ukapunguka vile vile, hatta kama kivuli chake kipo sasa. Bassi pasipo kukumbuka sana mambo ya Warumi hapana kuelewa vema habari ya mataifa ya leo walivyopata kuwa na hali hiyo waliyo nayo sasa, na desturi zao na dini zao na kazi zao wanazofanyiza duniani pangine pangine na hapa Afrika pia. Bassi watu gani hao Warumi? walipataje enzi kuu wakaidumisha sana? mbona tunawakumbuka sana hatta leo?

Siku za Bwana wetu Isa Masiya alizokuwapo hapa duniani, Warumi walimiliki inchi zote zilizoizunguka bahari Mediterraneo, toka Uingereza mpaka Misri, toka mlango wa Gibraltar mpaka bahari Kaspiani.

Digitized by Google

Na mataifa yote yaliokaa katika inchi hizo yalikuwa siku zile yakikaa raha na amani.

Habari za Warumi, ginsi walivyotiisha mataifa hayo mengi, wakayatuliza kwa raha na mustarehe, ndizo hizi. Zamani za kale watu waliokaa kati ya Italia walikuwa mbegu moja na Wayonani, lakini mbali kwa tabia na dini yao. Wakakaa makabila, na kabila moja ndio Walatini, na inchi yao inchi sawa na pana upande wa kusini wa mto Taiber. Wakaondoka wakajenga mji ukingoni mwa mto makusudi wazuie adui zao Waturuski waliokaa ng'ambo ya pili. Mji huu ukajengwa juu ya kilima, na vilima vingine sita karibu yake, yapata kama miaka mia saba na hamsini mbele ya kuzaliwa Bwana wetu Isa Masiya. Na jina la mji, Rumi.

## 29. Hadithi ya Romulo na Remo.

Warumi wenyewe wameihadithia asili ya mji wao hivi.

Palikuwa na mtu, jina lake Amulio, naye mbaya sana. Akaondoka akamtwalia ndugu yake mkubwa milki yake akamiliki mwenyewe. Na watoto wa nduguye akawachinja. Akabaki binti ya nduguye tu, naye amezaa watoto wawili waume nao mapacha. Bassi Amulio akaamuru watoto wale watupwe mtoni. Wakawatupa mtoni, ndio Taiber. Maji yakawachukua, wakawasili hatta mahali, wakakwama topeni. Mbwa wa mwitu akawakuta kule ukingoni mwa mto, akawapeleka tunduni kwake akawanyonyesha. Hatta siku moja mchunga kondoo akipita akisikia

Digitized by Google

watoto wanalia akaona ajabu, wamo watoto wachanga wazima katika tundu la nyama ya mwitu. Akawaleta kwake akawalisha siku nyingi. Wakakua wakawa vijana hodari sana, wakajulikana na yule babuo, wakamua Amulio, wakamrudisha babuo katika ufalme wake.. Na vijana wale, majina yao Romulo na Remo. Wakafanya shauri la kujenga mji kando la Taiber pale pale walipoachiwa topeni na maji. Wakapiga misinji wakajenga (B.C. 753). Fitina ikawapata kwa ajili ya nani amilikiye mji huo. Hatta Remo akamfanyia ndugu yake thihaka, akiruka juu ya kuta anazozijenga: nazo fupi, bado kujengwa juu. Romulo akaingiwa uchungu, akamwua pale pale kwa jembe lake, akawa mkuu wa kwanza wa Rumi. Hiyo ndiyo waliyohadithi Warumi.

---

## 30. Warumi wa Kwanza.

Warumi wakalima mashamba, wakafanya biashara, wakafanikiwa. Na desturi zao za kwanza ndizo hizi. Mambo ya nyumbani, killa mwenyi nyumba hutawala nyumba yake. Na mambo ya mji wote, killa mwenyi nyumba huitwa barazani, hufanya shauri na mfalme, ndiye mkuu wa baraza. Wakakaa siku nyingi. Watu wengi wakaangalia mji ule unakua vema unafanikiwa, wakaja wakakaa humo, wakasayidia katika vita, wasiitwe barazani. Watu hao wageni wakaitwa Waplebi, na watu wa asili Wapatri. Rumi ukawa mkuu wa miji ya Walatini, ndio kabila lao Warumi wa kwanza. Halafu yake Warumi wakawaondosha wafalme wao (B.C. 509), na mahali pa wafalme wakachagua killa mwaka watu

Digitized by Google

wawili kuwa majemadari katika vita na maliwali wa mji, wakawaita makonsuli. Tangu siku zile Warumi wote walichukia sana hatta jina la mfalme. Wakiona mtu anajipendezeka kwa watu, humthania ataka kuwa mfalme, humwondosha ama kumua.

Warumi wakashindana sana na makabila waliowazunguka, kwanza Waekwi na Wavoleski na Waturuski, tena Wasaminiti, tena Wayonani waliokaa katika Italia upande wa kusini. Wakashindana nao hatta wakaisha kuwashinda. Na kazi ya kuwashinda watu hao wote, kazi ya miaka kama hamsi mia. Bassi ndio ajabu kuu ya Warumi, walivyojifunga kwa kazi hiyo ya kushinda wote, mwaka kwa mwaka, kizazi kwa kizazi, wasilegee. Ajabu na hii pia. Warumi hodari sana, na wenyi akili nyingi katika vita. Kwa nini hawakushinda adui upesi, si polepole tu? Tazama maana yake.

Kulikuwa na fitina siku zote katika watu wa Rumi. Wale wa kwanza, wale wenyi kwitwa barazani na kutengeneza mambo ya serkali, ndio Wapatri, hawakukubali wageni, ndio Waplebi, washariki nao katika mamlaka yao. Na Wapatri si wengi lakini wakubwa na wenyi mali, na Waplebi wengi na wafaao sana kwa vita, hawana mali nyingi. Bassi Rumi wa kale ulikuwa si hali moja, kama miji miwili, mji wa wangwana na mji wa wanyonge. Nao hawapatani vema, illa kwa shidda. Hatta Wapatri wakawaonea Waplebi, wakawatoza kodi, wakawatumisha vitani. Tena Waplebi wengi wenyi mashamba, wanalima. Bassi ikija vita, mashamba huharibika, chakula hapana, hawana buddi kukopa mali mbegu vyombo kwa Wapatri, hujipasha deni kubwa. Wasipoweza kulipa, hufungwa, huuzwa utumwani. Bassi hali ya Waplebi kwanza thaifu sana. Wakatetana miaka mengi, wasipigane lakini wao kwa wao: kwani walizungukwa na adui. Wangalipigana, wangali-

Digitized by Google

shindwa na adui marra moja, na kuangamia wote. Bassi kwa sababu ya kuhitajiana, walichukuliana. Ndio njia ya salama moja tu. Wapatri pasipo Waplebi hawana nguvu. Waplebi pasipo Wapatri hawana mali. Mwisho Waplebi wakashinda wakajipatia daraja bora na mamlaka kwa kadiri yao katika mji.

Na fitina hiyo ndiyo iliyowapinga Warumi wasishinde adui upesi, kwani nguvu gani ya watu wasio hali moja wala shauri moja? ndiyo iliyowazoeza kujiweza roho zao na kutendana haki, ikawawezesha kudumu hatta wakashinda adui mwisho. Walisema, "Sisi watu wa Rumi tusipopatana, tutakufa. Bora kuishi. Bora kufanya yo yote, kuvumilia yo yote kwa ajili hiyo. Tena njia ya kupatana vema ipo moja tu, ndio kuzitii sheria tulizo nazo. Zikiwa mbaya, zitengenezwe, hatta kwa kushindaniwa sana. Ziwazo zote, tuzitii. Ndio salama." Hivyo Warumi wakapata nguvu ya kuwaweza walimwengu, kwani walijiweza roho zao. Walikuwa watu wa kutanguliza wenzio na kukubali hatta kufa kwa ajili ya mji wao, wakawa watu wa kuzitengeneza na kuzitii sheria zao, wasifuate killa mtu tamaa yake na fayida yake.

---

## 31. Mji na Mwili.

Hii ndiyo hadithi ya fitina ya ndani na za vita za nje, zilizowapata Warumi katika muda wa miaka hamsi mia.

Hapo kale watu wa Rumi walionewa sana na wakubwa wao. Hatta siku moja wakaondoka wakatoka mjini wakaenda zao kwa kilima wakakaa huko.

Digitized by Google

Hawakupenda kupigana na wakubwa, wala kuwaua wala kuwafanyia jeuri. Waliwaacha tu. Wakubwa wakauona mji hapana watu, na adui wengi waliozunguka Rumi, wakaogopa wakinena, "Mambo haya hayafai. Pasipo watu, hatuponi naswi." Wakatuma wajumbe kwenda kutuliza watu na kuwapatanisha, nao hawakubali. Wakatuma wangine vile vile, hawakubali.

Bassi mwisho mkubwa mmoja, jina lake Menenio Ageripa, akaenda pale walipo watu akawaita barazani akatoa maneno haya, "Enyi watu, sikilizeni." Siku za zamani kulikuwa na fitina katika mwili, viungo vyake vyote wakitetana na tumbo, wakimwambia, "Ewe mvivu, gissi gani mambo haya? Sisi kutumwa hivi na hivi, hivi na hivi, siku zote, wee kukaa, kupata fayida, kushiba, bassi?" Naye tumbo hakusema hatta neno. Bassi wale wakanung'unika, wakafanya hasira wakasema killa mtu, "Sitaki bwana huyo, sitaki kazi. Haya, twende zetu." Wakakoma, wasifanye kazi kabisa. Miguu hawaendi chakulani, mikono hawasogezi chakula, masikio hawasikii kengele, macho hawatazami sahani, kanwa hajifumbui, meno hawatafuni. Hatta tumbo mwenyewe akaona njaa. Halafu yake nao wote hawawezi. Hawana nguvu wala miguu kwa kutembea, wala mikono kwa kushika, wala masikio kwa kusikia, wala macho kwa kuona, wala kanwa kwa kujifumbua, wala meno kwa kutafuna. Tumbo akawaambia, "Enyi wavivu, sitendi kazi mimi? Kukaa, kuwaagiza kazi zenu, kushiba mwenyewe, ndio kazi yangu kweli. Na fayida kwenu je? Tazama, mimi ninayewawezesha kwa vitu vyote. Kwa maana yangu ninyi hupata kulishwa, kujipendeza, kukaa raha, kuwa na uzima na hali njema pia. Bassi, kazi yenu ndio fayida yenu. Nami, si mvivu mimi." Watu wa Rumi wakasikia kama kweli hai-

fai fitina katika mji, wakafanya shauri na wakubwa, wakapewa njia ya kujilinda wenyewe wasionewe sana na wakubwa. Walipewa ruhusa kujichagulia wakuu wawili killa mwaka, waliokwitwa Matribuni, kazi yao kuwalinda Waplebi wasionewe na Makonsuli na wakuu wa Wapatri (B.C. 494). Baadaye wakapata kuzijua sheria, kwani Wapatri tu waliojua kwanza nini halali, nini haramu, wakahukumia Waplebi wapendavyo. Lakini B.C. 450 sheria zikaandikwa wazi, wote wakazijua. Ndivyo walivyopatana, wakarudi mjini, wakakaa.

---

## 32. KORIOLANO.

Palikuwa na mtu Mrumi, naye mshujaa sana. Warumi wakapigana na adui zao, watu wa Korioli, ndio mji wao, wakawafukuza hatta wakaingia katika mlango wa mji. Mtu yule akaingia pamoja nao peke yake, mlango ukafungwa nyuma yake. Akawa mshujaa sana, akapigapiga Wakorioli, akawafungulia wenziwe mlango wa mji, wakautwaa mji. Yule mshujaa akaitwa Koriolano kwa sababu ya tendo lile kuu.

Ikawa njaa katika Rumi. Wapatri wana chakula, Waplebi hawanacho. Naye Koriolano Mpatri, akasema, "Waplebi wasipotii Wapatri, hawali." Waplebi wakamkasirikia sana. Hatta akaogopa akakimbia kwa adui wale wale aliowapiga kwanza. Wakamkaribisha furaha, akawa jemadari wao. Akaendoka kwenda pigana na Warumi. Warumi wakafanya hofu, wakatuma wajumbe walio wakubwa na rafiki

Digitized by Google

yake Koriolano waende kupatana naye. Hakukubali. Wakatuma wakohani wenyi sanamu za miungu yao. Hakukubali. Mwisho wakatuma mama yake na mkewe na watoto wake. Wakamlaki wenyi nyuso za huzuni na nguo mbovu mbovu, wakampigia magote. Koriolano akawakaribisha vizuri akataka kumbusu mamaye. Yeye akakataa, akamwuliza, "Wewe adui ao mtoto wangu mimi?" Akamwambia, "Ee mama, ndiwe umenishinda." Akaenda zake, asipigane na Warumi.

Bassi tazama Warumi ginsi gani walivyothoofika kwa maana ya fitina zao, na watoto walivyoheshimu mamao sana.

---

## 33. Mafabio.

Palikuwa na mtu Mpatri jina lake Kaiso, wa nyumba ya Mafabio, nayo nyumba mashuhuri katika Rumi. Akawa shujaa wa vita, na mwenyi haki pia. Akaondoka akawatolea maneno Wapatri wenziwe, "Kwa vita hizi tumepata inchi tele. Haya, tuwagawanyie nao Waplebi kwa kadiri yao; kwani ndiyo haki, washindao vitani na wachumie." Wasikubali Wapatri wakasema, "Kaiso yuna akili, lakini ataka makuu." Kaiso akaona uchungu, akasema moyoni, "Siwezi kupigana na wenzangu, wala sikubali kusharikiana na wasio na haki. Bassi nipigane na adui zetu wote."

Palikuwa na mji wa Waturuski, karibu na Rumi, jina lake Veii. Na watu wa Veii wakawauthi sana Warumi, kwani vita yao ya hila. Warumi wakitaka kupigana, Waveii hukimbilia mji; Warumi wakirudia

Digitized by Google

kwao, Waveii hutokea, huharibu mashamba, huteka ng'ombe na mali. Ndiyo kazi yao, Warumi wakauthika sana.

Bassi Kaiso akafanya shauri na Mafabio wote, ndio jamaa zake, akawaambia, "Sisi tukate jambo hili, Warumi wote wasisumbuke burre." Wakaona rathi, wakajitoa furaha, maisha mali yote; wakaacha nyumba zao, wakajipanga wenyi selaha na bandera mbele ya nyumba, watu thelatha mia na sita, wote Wapatri, na Kaiso ndiye jemadari. Watu wote wakawashangilia sana, wakawasifu mashujaa wakipita mjini, wakienda vitani peke yao kupigana na mji mkubwa Veii. Wakafika karibu na Veii wakatua wakafanya boma, wakawapiga Waveii marra nyingi wakafanikiwa sana. Hatta kwa kufanikiwa wakaanza kulegea, wasifanye mashauri ya vita kwa akili na kuangalia kama kwanza; adui zao wakaona, wakasema, "Tuwashinde kwa hila." Marra kwa marra huwapelekea makundi ya ng'ombe, karibu napo walipotua Mafabio; Mafabio hutokea kwa haraka, huwafukuza hutwaa ng'ombe, huwachukua. Siku zikapita, hatta siku moja Waveii waliwavuta Mafabio vile vile, wakatokea wote wakawafukuzia mbali na kituo, Waveii wakawaotea njiani, wakawarukia gháfala pande zote kuwazunguka, wakawapiga mikuke wakiwasonga sana, kwani wengi, nao Mafabio wachache tu. Vita ikashikika ikawa kali sana, Mafabio wakakimbilia kilima kidogo kando la njia; wasiokoke, kwani Waveii walizunguka nyuma wakapanda wakawarukia vile vile, hatta wakaisha. Mafabio wote wakafa illa mmoja kijana.

Ndio sifa yao Mafabio, kujitoa kwa ajili ya ndugu zao, kwa ajili ya haki.

Digitized by Google

## 34. Vita ya Waturuski.

Baadaye Warumi wakaondoka wakapigana na Veii wakauzunguka miaka kumi wakautwaa. Wakaendea mji mwingine wa Waturuski, Falerio, nao mji wa nguvu wenyi boma. Palikuwa na mwalimu mmoja mjini mle, na waanafunzi wake ndio watoto wote wa watu wakubwa wenyi cheo. Naye huwafundisha mengi. Kiisha fundisha killa siku huwapeleka shamba nje ya boma kwenda kucheza na kujinyosha na matembezi. Akafanya shauri baya sana hivi.

Ilipokuja vita ya Warumi, ashika desturi yake vile vile, huwapeleka watoto nje michezoni. Hatta siku moja aliwachukua mbali na mjini, akawaleta hatta kituoni kwa Warumi, akasema, "Tazama, nimewatoa watoto hao, ndio mji halisi, kwani wote watoto wa watu."

Kamillo, jemadari wa Warumi, akamwambia, "Mtu mbaya wewe, hatupigani na watoto; na mji ntautwaa kwa nguvu kirumi, si kwa hila." Akamvua nguo zake akamfunga mikono nyuma, akawapa watoto bakora, wakampigapiga mwalimu, wakamrudisha mjini. Wafalerio wakashangaa mno, wakasema, "Bora Warumi watuweze sisi kuliko wakubwa wetu, kwani wema na wenyi haki." Wakajitoa wenyewe.

---

## 35. Kinkinato.

Palikuwa vita ya Warumi na Waekwi. Jeshi moja la Warumi likatoka likienda kupigana na Waekwi. Wakafika hatta mahali palipozungukwa na milima

Digitized by Google

na mlango wake mwembamba sana. Waekwi wakawavizia wakiingia humo, wakaja mbio wakaulinda mlango ule, wasiweze kutoka tena. Jeshi lote zima limefungwa ndani. Watu wa mji wakaletewa habari, wakafathaika sana, wakafanya shauri, wakasema, "Tumwite Kinkinato. Ndiye jemadari mkuu." Wakaenda kumtafuta. Naye akawako koondeni, amepiga uwinda, analima katika koonde lake. Akiona wajumbe wanakuja mjini, akavaa nguo kwa heshima yao. Wakamwambia, "Umekwitwa kuwa jemadari mkuu." Akawaambia, "Haya." Akaenda mjini, akakusanya jeshi, akaamuru killa mtu atwae chakula na miti kumi na miwili. Wakatoka wakafika kule kwenyi milima usiku. Nao Waekwi wako wanaulinda mlango wa boonde vile vile. Bassi Warumi wakawazunguka Waekwi kwa hila katika giza, wakafanyiza ua wa miti pande zao zote. Ilipofika assubui, wakaonekana Warumi kwa ndani, Warumi kwa nje, na Waekwi nao kati kati. Marra Waekwi wakajitoa. Kinkinato akarudi Rumi kwa shangwi na majeshi mawili ya Warumi mazima. Baadaye akaenda zake koondeni akalima vile vile.

Bassi tazama Warumi walivyo hodari. Hatta mtu leo mwenyi shamba tu, kesho mkuu wa Rumi na apigaye adui kwa akili akipata sifa nyingi; marra hugeuka mkulima tena, kama maskini.

---

## 36. Wagallo na Mabata.

Palikuwa na watu, wakikaa upande wa kaskazini wa Italia, waliokwitwa Wagallo. Wakafanya jeshi kubwa, wakaenda kupigana na Warumi, wakafika

Digitized by Google

karibu na Rumi penyi mto Alia, wakawapiga Warumi sana. Warumi wengi wakakimbilia mbali, wangine si wengi wakaingia katika ngome ya mji, wakailinda. Walikuwako tena mjini wazee wenyi mvi, nao wakiona haya kuuacha mji, wakavaa mavazi mazuri, wakakaa kitako barazani killa mtu katika kiti chake, wakangoja. Hatta Wagallo wakaja kwa tadi, wakakuta wazee wale wanakaa kimya wasifathaike hatta kidogo, wakasangaa. Mmoja wao akampapasa mzee ndevu, mzee akampiga fimbo kitwani. Wagallo wakawarukia, wakawachinja wote thóruba moja. Kiisha wakauteketeza mji, wakajaribu kuitwaa ngome, wasiweze (B.C. 289).

Na ngome ile imejengwa juu ya kilima kisichopandika na mtu, ginsi kilivyosimama sana; pande zote zaenda juu sawasawa. Ikaitwa Kapitoli ile ngome. Bassi Wagallo wakakaa siku nyingi wasiweze kuitwaa. Hatta mtu mmoja akatafuta njia, akaita wenziwe, wakapanda kwa shidda sana usiku, na Warumi wamelala usingizi wote. Palikuwako katika ngome mabata. Bassi marra Wagallo walipokuwa wakifika juu, mabata wale wakalia sana, Mrumi mmoja akaam'ka, akatwaa ng'ao yake akamsukuma Mgallo aliyetangulia, akamtupa chini. Warumi wangine wakaja mbio, wakawafukuza kabisa.

Walipokwisha kuuteka mji, Wagallo wakaondoka wakaenda zao kwa inchi yao. Warumi wakarudi, wakajenga tena pale pale.

---

## 37. Vita ya Wasaminiti.

Baada ya vita ya Wagallo, Waekwi na Waturuski hawakuwa na nguvu; kwani nao wamepigwa na

Digitized by Google

Wagallo, hawakupigana sana na Warumi tena. Ikaanza vita ngine, ndiyo ya Wasaminiti, ndio kabila hodari sana, waliokaa upande wa mashariki wa Italia milimani; vita hiyo ikaendelea miaka hamsini, mwisho Wasaminiti wakashindwa.

Lakini katika vita hii msiba mkuu uliwapata Warumi. Killa mwaka Warumi walituma makonsuli na majeshi mawili kupigana na Wasaminiti. Palikuwa na jemadari wa Wasaminiti, jina lake Pontio, mwenyi maarifa mengi ya vita na hodari sana. Akawatega Warumi hivi. Alichagua watu thenashara wachunga kondoo, akawapeleka kuchunga kondoo zao si mbali na kituo cha Warumi, akamwambia killa mtu, "Ukikamatwa na Warumi, uwaambie Wasaminiti wako mbali, wameuzunguka mji Lukeria na karibu watautwaa." Watu wale wakafanya hivi; bassi kwa sababu wote walisema sawa sawa, Warumi walisadiki habari hizi kuwa ndizo kweli, wakafanya haraka kwenda kuwaokoa rafiki zao wa mji. Pakawa njia mbili, moja nzuri na sawa lakini mbali, moja ya kukata lakini ipitayo milimani napo pabaya sana, panakwitwa, Panda la Kaudio, penyi namna hii. Kwanza mlango mwembamba wa kuingilia, tena mbele kidogo nafasi wazi peupe pamezunguka na milima, tena mlango mwingine mwembamba sana vile vile pa kutokea upande wa pili. Warumi wakasema, "Haithuru, tupite njia ya milimani, tukafike upesi."

Wakaenda wakapenya ndani, wakaendelea, kumbe mlango wa pili haupitiki, wamepingiwa njia kwa mawe, miti, vitu vingi. Wakasema, "Hila hiyo. Turudi." Wasidiriki. Wamepingiwa njia vile vile. Wamefungwa. Hakuna kutoka wala wokovu. Wakatua pale pale ndani ya milima kati ya milango, na adui wakiwacheka na kutukana; wasile wasilale usiku ule, hofu tu na mshangao.

Wakajaribu marra nyingi kuwapatia adui na kuwa-

Digitized by Google

piga, wasiweze; kwani miamba pande zote haipandiki. Bassi Wasaminiti wakafanya shauri, "Tuwashindishe kwa njaa, ao kuwachinja papo hapo?" Wakamwita mzee mmoja mwenyi akili, baba wa Pontio, akamwuliza shauri. Kwanza akasema, "Waacheni Warumi waende zao salama salamini." Wasikubali Wasaminiti, wakamwuliza tena, akasema, "Wachinjeni wote, asiokoke hatta mmoja." Wakasema, "Maneno hayo mbali mbali. Yuna wazimu yule mzee." Akawaambia, "Sina wazimu mimi. Mkiwaacha, watakuwa rafiki. Mkiwachinja, vita haiji tena upesi." Wasiwe rathi.

Wakasimikisha mikuke miwili na wa tatu juu, wakawaambia Warumi, "Mkitaka kutoka salama, tokeni hivi. Killa mtu atoe selaha zake, akavae nguo moja, akapite chini ya mkuke. Tena, msilete vita hapa tena." Warumi wakakubali lakini kwa shidda sana, kwani walipenda mauti kuliko aibu; wakashurutishwa na makonsuli, wakisema, "Tukiuawa sisi, Rumi umekwisha." Wote wakapita kwa kuinama chini ya mkuke, hatta makonsuli na maakida na asikari wote; wakaenda zao kwa huzuni na majuto makuu. Walipofika Rumi, watu wa mjini waliingiwa na hasira sana na uchungu; halafu wakawahurumia. Wakasema, "Mapatano hayafai, wala sisi hatuyakubali. Bassi waliopatana, ndio makonsuli, warudi huko kwa Wasaminiti, wakajitoe." Wakaenda kujitoa. Pontio akakataa, akasema, "Sitaki watu wawili tu. Rudisheni jeshi zima pale pale penyi Panda la Kaudio, msipofikiliza ahadi yenu." Wakamwambia, "Sisi tuliokosa; bassi tupo." Akawafukuza kwa ghathabu, vita ikashikika vile vile. Baadaye Warumi wakamkamata Pontio wakamua, kwani wameingiwa uchungu, hawana huruma.

Digitized by Google

## 38. Purro Myonani.

Walipokwisha Warumi kuwapiga Wasaminiti, Wayonani waliokaa katika miji mingi ya Italia upande wa kusini wakaogopa, wakamwomba Purro, aliye mfalme wa Epiro katika Uyonani, aje awasayidie. Akaja, na watu wengi naye, na frasi na tembo pia. Akapigana na Warumi, akawashinda, lakini kwa shidda nyingi sana, watu wake wengi wengi waliouawa siku ile. Hatta Purro akasema, "Nikishinda hivi marra mbili tatu, nimeshindwa," kwa sababu ya watu kuwa wengi waliompotea. Akatuma mtu mwenyi akili kwenda kupatana na Warumi. Nao kwanza wakapenda, halafu yake wakakataa, isipokuwa Purro atatoka kwanza katika Italia. Yule mtu akarudi kwa Purro akampasha habari ya baraza ya wazee katika Rumi, akasema, "Haifai kushindana na Warumi. Wazee wale wote sawasawa, wote wafalme." Purro hakumwangalia, akapigana na Warumi akawapiga marra ya pili, asiwatiishe hatta kidogo. Akaenda zake kushinda miaka miwili, akapigana marra ya tatu, akapigwa sana. Akarudi kwake.

Warumi wakamiliki Italia yote kwa kusini.

---

## 39. Tabia ya Warumi.

Warumi waliupenda mji wao kuliko nafsi zao wenyewe. Hatta akawa mtu, jina lake Dekio, naye konsuli mwaka mmoja. Warumi wakakipigana na

Digitized by Google

adui zao, wasiwaweze kwanza. Na yule Dekio amesikia habari, kama jemadari akijitoa afe, watu wake ndio watakaoshinda. Marra akajifunika kitwa, akaruka kati ya adui akauawa. Warumi wakashinda adui zao siku ile.

Na Warumi wagumu sana. Wakapigana siku moja na adui, konsuli jina lake Manlio akatoa amri, mtu ye yote asipigane na adui peke yake. Wakakaa. Halafu adui akatokea akamwita mtoto wake yule konsuli, akamwambia, "Tupigane sisi." Akaitika, "Haya tu." Wakapigana. Mrumi akampiga adui akatwaa mateka yake akarudi. Babaye akasikia habari ya kuwa amepigana peke yake, nayo marufuku, akaamuru aletwe kwake akamhukumia kukatwa kitwa, sababu aliasi. Akakatwa kitwa akafa kuko huko mbele ya baba yake. Watu wote wakaingiwa na machukio, wakaona amefanya vema lakini yule konsuli.

Warumi wa kwanza hawana choyo. Hatta siku moja Wasaminiti wakitaka kujipendekeza kwa jemadari mkuu wa Warumi, wakampelekea zawadi, thahabu nyingi. Wajumbe wakamkuta anashinda shambani, anapika boga mwenyewe ndio chakula chake, na nyumba haina pambo. Wakamtolea zawadi ile, asiipokee. Akawaambia, "Heri kuwa huna mali, na kuwaweza walio nazo." Wakaondoka.

---

## 40. Njia na Makolonia.

Kwa desturi za vita, Warumi mbali na watu wangineo mbali. Watu wangine wafanyapo vita, hupiga adui, huteka miji, huteketeza nyumba, huchukua



Digitized by Google

ng'ombe na vyombo na vyakula, labuda hukaa kidogo, hurudi kwao, bassi. Warumi hawaachi inchi yo yote waliyoipata, huimiliki dayima; huwapiga sana adui kwanza, tena huwatuliza, huwazoeza desturi na tabia zao Warumi. Wakawatuliza hivi. Huweka asikari Warumi katika miji huko na huko ya killa inchi waliyoipata. Warumi hao, hutiisha watu waliopo, hulima mashamba, huongoa watu kutambua nia za Warumi na nguvu zao, kama kuasi hakufai, kutii kwafaa. Na miji hiyo ya asikari, ndiyo iliyoitwa makolonia.

Tena Warumi hufanyiza njia kuu na nzuri killa wamilikipo. Hatta na njia hizo ajabu sana. Zatoka katika Rumi, zafika hatta mipakani kwa milki yao, zimenyoka kabisa, zaenda sawasawa milimani boondeni mashambani mitoni, hazipotoki; zimetengenezwa na mawe na chokaa tele, upana wao wa kupisha gari la frasi. Hatta zingine zakaa mpaka leo, zimepata miaka elfeen, zinatumika vile vile siku hizi katika Uingereza na kwenyi inchi zilizo mbali sana na Rumi. Na maana yao, majeshi ya Warumi wapate kupita pote upesi, tena Warumi kuletewa upesi habari za milki yao yote.

Hatta na fumbo hili limejulikana sana, kama "Warumi walitiisha ulimwengu kwa majembe,"—kwa sababu ya njia hizo na tena, killa Mrumi akienda kwa vita huchukua miti na jembe, na killa watuapo usiku majeshi ya Warumi katika vita zao, hufanyiza boma la udongo na miti lisilotwalika na adui, hulala raha na salamu. Ndizo kazi za majembe yao.

Digitized by Google

## 41. Kartago.

Marra walipokwisha kuwatiisha watu wote wa Italia, Warumi wakafanya vita na watu wa mji mkuu, ulioko pwani upande wa kaskazini wa Afrika, ndio Kartago. Na Wakartago ni kwa asili watu wa Turo, Wafoiniki. Wakatoka kwao, wakasafiri baharini, wakaona pazuri pale Afrika pwani kulekea Sikilia, wakajenga mji wakakaa wakasitawi kwa mambo ya biashara na vita pia. Hatta halafu wakaweza sana baharini. Bassi Warumi wakafanyiza vyombo vyingi, wakapigana nao miaka mia. Mwisho wakawashinda, wakamiliki inchi ya Kartago, na Sikilia na Hispanya pia, wakawa wakuu wa bahari yote Mediterraneo.

---

## 42. Regulo.

Warumi wakawa wanapigana na Wakartago. Na Wakartago wakatumia tembo wengi katika vita, Warumi wakaogopa, wakashindwa sana kwanza. Hatta na jemadari mkuu wa Warumi, jina lake Regulo, akatwaliwa akafungwa akachukuliwa kwao. Akashinda huko gerezani amefungwa miaka miwili. Bassi siku moja Wakartago wakapigwa, wengi wakatwaliwa wazima na Warumi. Wakafanya shauri, wakataka kupatana nao Warumi na kuwabadili wafungwa. Wakatuma wajumbe kwa Rumi na Regulo pia, kwa maana mtu huyo mwenyi sifa nyingi na daraja bora kwao, wakamwapisha kwanza,

Digitized by Google

atarudi kwa Kartago gerezani, wasipopata wajumbe kupatana na Warumi.

Bassi Regulo akafika kwake Rumi, akasimama mlangoni nje ya boma, akisema, "Mimi nimetoka kuwa Mrumi, mimi mtumwa wa washenzi; wakuu wa Rumi kukaribisha wageni ndani ya boma ndio haramu. Bassi nimekaa hapa." Hatta mkewe na watoto wake wakamtokea, wala hakufurahiwa moyo nao, akawaambia, "Mimi mtumwa, si mtu mimi, kitu tu." Halafu yake na wazee wakaja, wakafanya baraza huko nje, wakamwambia, "Karibu, kakae mahali pako, mkuu wa Rumi na wewe." Asikubali, akasema, "Enyi wazee, mimi mtumwa wa Wakartago, nimetumika nao kwenda kupatana nanyi." Kiisha kusema haya, akataka kwenda zake. Nao wakamzuia, hatta na wajumbe wa Wakartago wakamsimamisha hapo tena. Hana buddi kukaa. Akatoa maneno haya, "Enyi Warumi, msipatane na Wakartago hatta kidogo, msiache kupigana nao, msibadili wafungwa. Na mimi pia, nikitolewa kurudi kwao, haithuru." Mtu mmoja aliye mkohani akaondoka akamwambia shauri, "Kwani kurudi huko? hawakukuapisha kwa nguvu? thulumu hiyo, siyo haki. Uapo ule haufai neno." Naye Regulo akajibu, "Nimeapa, bassi. Si mwongo mimi, mtumwa mimi lakini Mrumi bado. Najua nitateswa sana hatta kufa. Haithuru." Wazee wa Rumi wakasikitika, hawana buddi kulifuata shauri lake. Wakamsindikiza njiani, na mkewe na watoto wakitoka machozi wakimwomba akae, wasimweze. Akarejea Kartagoni na wajumbe. Wakartago wakafanya uchungu mwingi, wakamkaza ndani ya pipa lenyi misomari mingi, mirefu na ukali, pande zote kwa ndani, wakalifingirisha, akapata maumivu machungu, akafa.

Digitized by Google

## 43. Hanibali.

Siku zile Warumi walipopigana na Wakartago, palikuwa na mtu, jina lake Hanibali, Mkartago. Akiwa mtoto bado, amepata miaka tissia, babaye akamwambia, "Wataka kwenda kwa vita nami?" Na baba yule jemadari mkuu wa Wakartago. Akamwambia, "Nataka." Akamkambia, "Uniapie bassi, katika maisha yako siku zote uwe adui yao Warumi." Akamwapia, akaenda kwa vita, babaye akatiisha inchi ya Hispanya; babaye akafa.

Hanibali hakusahau alivyoapa, akafanya jeshi, akapiga mji mmoja katika Hispanya, uliokwitwa Sagunto. Na mji ule umetegemea Warumi. Bassi Warumi wakapeleka wajumbe kwa Kartago, wamtete Hanibali. Wajumbe wakafika Kartago, wakaleta mashtaka, wasithubutishe. Mmoja wao akakunja joho lake, akasema, "Zimo humo vita na raha. Mwataka ipi?" Wakamwambia, "Upendavyo mwenyewe." Akalikunjua joho, akisema, "Natoa vita." Wakamwambia, "Haya."

Marra huyo Hanibali alijasiria jambo kubwa sana. Yeye mtu mmoja kama kijana kama peke yake, kwani mji wake mbali na jeshi lake moja tu, alithubutu kuwaendea Warumi katika inchi yao, nao taifa kubwa waliozoelea vita miaka mengi wasishindike na mtu; na majeshi yao mengi. Na kwa sababu Warumi waliweza baharini, hana buddi kuwaendea kwa inchi kavu, njia ya milima mengi na hatari nyingi. Hakuona hofu, ginsi alivyo mshujaa na kujijetea nafsi; akasema, "Nikijaliwa kuingia Italia, haikosi makabila ya Italia waliopigwa na Warumi watawaasi, watanisayidia."

Bassi akatwaa jeshi (B.C. 218), nussu watu wa

Digitized by Google

Afrika na wapandao frasi, hodari sana, ndio Wanumidi, nussu Wahispanya, na tembo pia; asikari zake wakampenda sana. Akashika njia upesi. Na vita ya kwanza ndio palepale katika Hispanya, kwani watu walimpingia njia asifike milimani Purenizi, nao wakali wakapigana kwa nguvu. Hanibali akawashinda, lakini nussu ya jeshi lake waliogopa, wakataka kurudi. Akawaacha, akapita milima akaingia Ufransa, ndio inchi ya Wagallo. Na vita ya pili ndio penyi mto Ron, mto mkubwa na uendao kassi, na Wagallo wengi wako ng'ambo, wamesimama ukingoni tayari kupigana na Hanibali anapokivuka. Hanibali akafanya hila akatuma ndugu yake na wapandao frasi kwenda kuvuka mahali pangine na kuzunguka nyuma ya Wagallo. Bassi alipokivuka, wao hao wakatokea ghåfala, wakawafathaisha Wagallo wakakimbia. Akavuka Hanibali na tembo zake pia, akaenda zake upesi kufika milimani Alpi. Na Warumi wamesikia anakuja, wakapeleka jeshi kwa Marselz, utokeapo mto Ron baharini, wasidiriki kumzuia, kwani amekwisha vuka. Wakasema, "Haithuru. Hawezi kupita milima Alpi," jeshi likaenda zake kufanya vita katika Hispanya. Ndivyo walivyomtharau. Na njia ile ya kupita Alpi mbaya sana kweli kweli, yenyi hatari nyingi na mashaka: kwani milima yenyewe mirefu, na yenyi theluji nyingi juu, na njia zisizopitika na frasi na tembo; lakini Hanibali alipanda kwa shidda sana akisumbuka na adui waliomwotea njiani, nussu ya jeshi lake lote likapotea kwa baridi na njaa na taabu na mapigano na kutupiwa mawe, wengi wakaangamia kwa maboromoko na kuteleza na kukanyagwa na frasi; si wengi waliotumbuza upande wa pili nao wamechoka na nussu kufa.

Halafu walipokwisha kupumzika na kupata nguvu ndipo Hanibali aliposhika vita na Warumi. Kwanza

Digitized by Google

akawapiga kwenyi mto Trebia karibu na Po, akavuka milima Apenains na boonde mbaya ya maji na matope, hatta akaharibika jicho moja kwa ugonjwa na kulemewa. Ya pili akawapiga kwenyi ziwa la maji Trasimene. Kwani Warumi walikimfuata upesi, wakaingia mahali pembamba, milima huko na maji huko, jeshi la Hanibali likawaotea, likawakatizia njia mbele na nyuma wasionekane kwa umande wa assubuhi, wakawarukia thóruba moja, wakawapiga sana, wachache tu waliookoka. Marra Hanibali akafika karibu na mji wenyewe Rumi, Warumi hawakuogopa wala kutiishwa hatta kidogo. Husema, "Sisi hufa, mji haufi." Tena mahali alipotua Hanibali na jeshi lake, mwenyi shamba lile aliliuza kwa mnada akapata thamani kubwa, kwani mnunuzi amesema, "Karibu litapatikana tena." Bàssi Hanibali alifahamu Warumi walivyo wagumu, na watu wa inchi alizozipiga hawakuasi. Akaendelea kusini, akawapiga sana marra ya tatu kwenyi Kanni, wakubwa wengi wengi akawaua kabisa na makonsuli pia. Wala hivi hakuwatiisha. Akakaa siku nyingi pale Italia, akawasumbua sana Warumi, lakini Wakartago kwa uvivu na ugomvi hawakumsayidia, na nduguye aliyekileta msaada aliuawa, hakufanikiwa tena. Mwisho hana buddi kuvuka bahari akarudi kwake. Warumi wakamfuata na jeshi kubwa. Wakapigana ya mwisho kwenyi Zama, Wakartago wakashindwa, mji wao ukaharibiwa kabisa na Warumi, Hanibali akakimbia kwa Anatolia (Asia Minor), baadaye akafa (B.C. 200).

Bassi huyo Hanibali mshujaa na mwenyi maarifa ya vita kupita wote, kama Iskander, kama Kaisari.

---

Digitized by Google

## 44. Milki ya Warumi.

Warumi wakashindana na adui miaka mia tena, baada ya kwisha kuwapiga Wakartago; wakatiisha Wayonani na Washami na Wamisri na watu walio-okaa zamani katika Ufransa, ndio Wagallo, na katika Uingereza, ndio Wabritoni. Hatta watu walioizunguka bahari Mediterraneo wote ndio milki ya Warumi. Wakapata mali nyingi nyingi, wakajifunza elimu ya Wayonani na desturi za kiungwana, wakafanikiwa sana. Mioyo yao ikageuka, na desturi zao za kale zikageuka. Maskini wengi mjini, nao hawa-angalii mambo ya mji, mambo yao wenyewe tu, kushiba na kukaa raha bassi. Baraza ya wazee, ndio yenyi nguvu na mamlaka, nao wenyi choyo sana, wakawaonea watu wa zile inchi walizozitiisha, wakawalipisha fetha nyingi kwa thulumu tu. Hatta wakubwa wao wakashindana sana, wakafanyiana vita marra nyingi wao kwa wao. Rumi ikafathaika sana kwa fitina.

---

## 45. Makaisari.

Zamani zile paliondokea mtu aliyepitilia mbali wenziwe wote kwa kuwa hodari na mwenyi akili, hatta huyu Mrumi mmoja aliwaweza Warumi wote. Akawaweza hivi. Aliangalia Warumi walivyoharibika tabia, tena mambo ya serkali yamechafuka, choyo tu na mathulumu kotekote; akataka kuyatengeneza akafanya shauri kubwa sana, ndio kuwa mfalme peke yake.

Naye mwenyewe mtu wa cheo na kizazi chake

Digitized by Google

kizuri. Tena hana hofu. Siku moja alikamatwa na haramia wakamchukua kifungoni wakataka kama reale asharini elfu, makombozi yake. Akawacheka akasema, "Mtapata hamsini elfu, kwani mimi mtoto wa watu; halafu nitawasulubisha lakini." Wasisadiki. Wakaletewa fetha ile wakamfungua. Akakusanya jeshi akaja akawapiga akawasulibisha, kama alivyosema. Tena mtu wa bidii. Alitaka kuweza kuwashawishi Warumi kwa maneno yake mazuri na kuwaongoza apendavyo, akajifunga kuhitimu kuwa msemaji bora. Akahitimu akarudi Rumi, watu wakampenda sana wakamchagua kwa kazi za cheo zingine zingine, akazidi kuwapendeza. Akataka mali, apate kuwafanyia watu karamu na tamasha nyingi na michezo, kwani ndio waliyofurahia mno Warumi wote. Akajipasha deni akasema, "Nitalipa halafu." Wote wakamsifu sana. Lakini palikuwa na wangine wakubwa walioshindana naye wakataka kumwondolea mbali. Akasema, "Hao sitawaweza illa kwa nguvu." Akaenda zake kufanya vita juu ya Wagallo katika Ufransa ndio inchi yao, makusudi apate jeshi la asikari wasioshindika kabisa. Akalipata.

Tumehadithiwa kama katika miaka kumi ya vita ile alivunja miji mia nane, akapiga makabila mia tatu, akapigana na watu wengi, hatta akaua elfu elfu, akafunga elfu elfu, elfu elfu wakaokoka. Nao aliowafunga aliwauza, akapata mali nyingi sana akalipa deni zake akawapa asikari zawadi. Asikari wakampenda mno, tayari kumfia sikuzote. Hatta alipofikia Ingereza, asikari mmoja alipotewa na ng'ao yake, naye ametoa ushujaa sana, ni kupotewa na ng'ao tu akipigana na adui. Bassi Kaisari akamsifu sana, ginsi alivyopigana, yule asikari asijivune hatta kidogo, asema tu, "Ee Kaisari, nisamehe, ng'ao yangu imenipotea."

Digitized by Google

Baada ya miaka kumi aliendea Rumi na jeshi lake. Hapana aliyemsimamia. Walioshindana naye kwanza, wote wakakimbia. Akawafuata akawapiga penyi Uyonani na Misri na Hispanya, akarudi Rumi akatawala peke yake.

Na kutawala kwake kwa nguvu sana. Aliitengeneza serkali. Hakuna kuonea wala kuonewa; wala mwenyi nguvu hapana po pote katika milki ya Warumi illa kwa amri ya Kaisari. Akasuluhisha adui zake kwa upole, kwani aliwaachilia; hatta killa mtu mwenyi akili, akiwa rafiki akiwa adui, humzidishia cheo na nguvu. Akalitengeneza baraza la wazee, wasiwe na nguvu sana, illa kumtolea shauri tu kwa mambo ya serkali, akawaingizia walio rafiki zake na wafuasi wake, wapate kumtii. Akalitengeneza jeshi, hatta akasema, "Mimi sasa natawala wote, bassi vita hapana illa labuda mipakani." Akawaweka asikari wangine mipakani katika inchi zilizo mbali, wangine akawapa mashamba akawalisha katika Italia.. Akautengeneza mji, akajenga mahekalu na majumba, akazifanyiza njia, akawazuia waliofanya fitina; killa mtu mwenyi neno humjia, humwambia, huamuliwa, huenda zake.

Akaitengeneza taratibu ya miaka na miezi, na tarihi za siku, ndio kalendari, kuwa lile lile tunalotumia hatta leo; kwani maarifa yake mengi sana.

Hivi Julio Kaisari alivyopata kusitawi kuliko Warumi wote, hatta na kumpita Iskander na Hanibali na Nebukadnezar kwa kuwa na sifa nyingi, akafanikiwa sana. Hatta jina lake Kaisari limejulikana hatta leo; kwanza wafalme wa Warumi waliotajwa hivi, baadaye wangine. Tena alipewa jina "Imperator," nalo pia limetumika hatta leo, na killa mfalme mkubwa huitwa "Emperor." Tena mwezi mmoja "July," limepata kwitwa hivi kwa ajili ya heshima yake tu.

Digitized by Google

Lakini hakujaliwa maisha mengi. Tangu zamani za wafalme wao wa kale Warumi wote huonea chuki mno hatta kutajwa jina la mfalme na kulinena. Hatta jina hilo haswa naye Kaisari mwenyewe hakukubali kutajwa, asipate kuchukiwa na watu. Alichukiwa lakini, watu nao wangine rafiki zake wakafanya shauri kumua. Siku moja Kaisari amekaa barazani, mtu akaja kumwomba kitu, akasogea karibu, wangine waliokuwako makusudi wakamsonga killa mtu mwenyi jambia yake. Mmoja akamkamatia nguo, mmoja akamchoma mgongoni, Kaisari akastuka akashindana nao; wakamsukuma huko na huko, wakimchoma wakichomana. Hatta akamwona mmoja rafiki yake aliyempenda, naye anamchona, akalia, "Ee Bruto, na wewe pia," akajifunika kwa joho, akalala akafa.

Ndio mwisho wake. Nao waliomua hawakupata raha,—fitina na vita na mapigano wao kwa wao. Hatta alipoondoka mtu wa jamaa yake ndio Augusto Kaisari, akawatiisha adui akawatawala Warumi wote, akawasterehisha watu wa milki yao pia. Kwani Warumi wenyewe wamechoka, wakasema, "Makaisari hao, haya! watutawale. Labuda watatupatia amani na kustarehe." Akatengeneza vizuri mambo yote ya ufalme, huwatendea vema na haki, huweka maliwali katika inchi zote, hufanya hukumu sawa kwa watu na kwa maliwali pia; watu wote watoto wake, si Warumi tu. Ulimwengu wote ukifurahi, ukikaa raha na amani, inchi zote toka Uingereza mpaka Misri na toka mlango wa Jibraltar mpaka bahari Kaspiani. Ulimwengu ukamtii Kaisari wa Rumi, ukamheshimu (B.C. 31).

Ndipo alipozaliwa Bwana wetu Isa Masiya, ndipo ilipoanza milki yake isiyo na mwisho, ufalme wa mbinguni (B.C. 4).

Digitized by Google

## 46. Wayahudi (b.c. 600—a.d. 4).

Tukumbuke mambo ya Wayahudi tangu zamani za wafalme hatta wakati wa kuzaliwa Masiya ulipowadia.

Taifa la Wayahudi liliposita wi kwa nguvu na enzi ndio zamani za mfalme Sulemani (kama b.c. 1000). Tangu siku za mtoto wake walitengana wakapunguka. Walio wa ufalme wa Israeli, ndio makabila kumi, walichukuliwa na mfalme wa Sham, mji wao mkubwa Samaria ukavunjika (b.c. 721). Walio wa ufalme wa Yuda, ndio makabila ya Yuda na Benyamin, walichukuliwa na Nebukadnezar, mfalme wa Babel, Yerusalemi ukaharibika (b.c. 588). Wageni wakakaa katika inchi yao. Hatta 'Kuro, mfalme wa Waajjemi, akaondoka akaupiga Babel akautwaa (b.c. 538). Akawaacha Wayahudi wapendao kurudi kwa Yerusalemi. Wakarudi si wengi, wakaufanyiza mji, wakakaa. Ndiyo zamani za Zerubbabel, na Ezra, na Nehemia, na Haggai, na Zekaria, na Malaki, ndiye nabii wa mwisho (b.c. 400). Tangu b.c. 400 hatta zamani za Bwana wetu Isa Masiya hatunazo habari nyingi za Wayahudi, illa kidogo katika Maandiko yaliyokwitwa Apokrufa. Twajua lakini kama walikitengenezwa tayari kwa kuja kwake Bwana. Wakatengenezwa hivi.

Walitawaliwa na Waajjemi hatta b.c. 330; hawakuonewa; walitoa kodi tu; na mkohani mkuu ndiye mkubwa wao. Akaondoka Iskander akawapiga Waajjemi (b.c. 330), Wayahudi wakatawaliwa na wafalme Wayonani, wengi wakakaa Misri katika Iskanderia, wakajifunza desturi na elimu ya Kiyonani. Waliobaki katika Uyahudi walionewa mno na mfalme mmoja Antioko Epifani, akaondoka

Digitized by Google

Yuda Makabio, akawapiga Wayonani, Wayahudi wakapata uhuru kidogo. Mwisho wakaja Warumi, wakamfanya Herodi mfalme juu ya Wayahudi (B.C. 38). Hivyo Wayahudi walitengenezwa na Muungu kuwa tayari kwa kuja kwake Masiya, aliyenenwa kwao nabii tangu zamani.

Zamani za wafalme wao wenyewe walijisifu kuwa taifa teule la Muungu, wasimtii vema wala kuishika torati, wala kuwasikia manabii.

Bassi walipohamishwa Babel, wakatawaliwa nao Waajjemi, walijifahamu kama wametoka katika kuwa taifa lenyi milki na enzi, wamekuwa taifa lenyi kumwabudu Muungu mmoja na torati ya Musa na ibada ya kweli, ndio sifa zao Wayahudi. Bassi siku zile wakazidi sana kuiheshimia torati na maandiko; waalimu na waandishi wengi wakaondoka, wakafanza mapokeo (ndio maelezo na mafundisho ya watu wenyi hekima,) mengi mengi makusudi kuwa kama boma la kuizunguka na kuilinda Torati, isipungukiwe hatta neno moja, wala harufi moja. Hivyo walijua kama enzi si kitu, illa maneno ya Muungu. Tena walijifunza kuchukia sana ibada ya sanamu, ndio ibada ya makafiri pale Ajjemi waliposhindishwa kwa nguvu, na kuishika ibada ya Muungu mmoja. Na kwa kuwa na hali mbaya na nyonge miaka mengi wakapata katazamia mambo ya baadaye, na kumwomba Muungu, kwani msaada mwingine hapana.

Tena walipotawaliwa na Wayonani, hao Wayonani hodari sana kwa akili, na maarifa, na elimu yote; wakabishana na Wayahudi wa Iskanderia na pangine, wakithubutisha habari za Torati na maana yake. Hatta Wayahudi wakawazoelea, wakaanza kufarikiana wao kwa wao, wangine wakisema, "Sisi wenyi kuishika Torati haswa halisi na mapokeo pia," ndio Mafarisayo; wangine wakisema, "Sisi hatutaki mapokeo mengi, twaishika Torati tu, nayo si sana;

Digitized by Google

labuda nussu si njema; kiyama hapana; malaika hapana," ndio Masaddukayo. Bassi hivyo kwa kushindana kwao, Wayahudi walio watawa ikawaelea, kama kuongeza Torati haifai, na kuipunguza Torati haifai. Kazi ya Torati kuiongoza mioyo ya watu kwa mifano, wamtazamie Masiya na kumngojea kwa kuomba na saburi. Lakini si wengi walioelewa hivyo, kama Anna na Simeon na wangine.

Mwisho wakaja Warumi, nao taifa kubwa lililotiisha mataifa yote likiyashindisha kwa amani. Nao Wayahudi walipata amani, lakini kwa nguvu. Hawakukubali kutawaliwa na mtu. Wakasema, "Masiya atatawala kama Sulemani, kama Yuda Makabio." Lakini sivyo. Mioyo isipokuwa migumu, wangalisema, "Sifa zetu sisi Wayahudi, tumeaminiwa tangu zamani maneno ya Muungu na kumtazamia Masiya. Bassi Masiya ajapo, naye Myahudi, atatawala walimwengu, kama Warumi, lakini sio kwa nguvu na kuwapiga kama Warumi, illa kwa kuongoza mioyo katika njia ya amani, ndio kumjua na kumpenda Muungu. Katika Yeye hapana Myahudi wala mataifa, hapana Myonani wala mshenzi, hapana watumwa wala wangwana, wote mamoja katika Kanisa lake Masiya." Wengi hawakujua lakini Masiya alipokuja, wakamsulubisha. Na msalaba wake ndio kiti chake cha enzi isiyo na mwisho. Shauri lake Muungu limetimilika.

---

## 47. Yerusalemi.

(Aliyetupasha habari hizi za Yerusalemi ulivyoharibika na Warumi, ndiye mtu jina lake Yosefo

Digitized by Google

(Josephus), naye Myahudi na mkubwa, na mwenyi maarifa mengi ya vita. Kwanza akawapigania sana wenziwe, halafu aliwaacha akajitoa kwa Warumi, akaheshimiwa sana nao. Akaenda pamoja nao kwa vita hii ya Yerusalemi).

Tangu zamani za kale, zamani za Musa, Muungu aliwaonya Wayahudi kama wasipomwamini Masiya watakatika wote. Na Bwana wetu mwenyewe aliwaonya kwa mfano, akiwaambia (Luk. xx. 16), "Bwana wa shamba atakuja, atawaharibu wakulima hawa, na shamba lake atawapa watu wangine." Tena siku moja aliuangalia mji Yerusalemi, akalia akisema (Luk. xix. 42), "Ungalijua wewe siku hii hatta nawe yaliyo ya amani! Lakini sasa yamefichwa machoni kwako. Kwani siku zitakujilia adui zako watakapokujengea boma, watakuzunguka, watakuthiikisha pande zote, watakuangusha chini na waana wako ndani yako, wasikuachie jiwe juu ya jiwe; kwa kuwa hukujua majira ya kuangaliwa kwako." Tena watu walipokuwa wakilinena hekalu ginsi lilivyopambwa kwa mawe mazuri na matoleo, akasema (Luk. xxi. 6), "Haya mnayoona, bassi siku zitakuja lisipoachwa jiwe juu ya jiwe hapa lisiloangushwa." Na tena (Luk. xxi. 20), "Bassi mtakapoona Yerusalemi umezungukwa na majeshi, ndipo mtajua kama ukiwa wake ni karibu. Wakati ule walioko Uyahudi wakimbie milimani, na walioko kati mwake waondoke nje, nao walioko mashamba wasiuingie. Kwani hizi siku za kulipia kisasi, yapate kutimizwa yote yaliyoandikwa. Ole wao wenyi mimba na wanyonyeshao siku zile, kwani itakuwa shidda kuu katika inchi na ghathabu kwa watu hawa. Nao wataanguka kwa upanga, watachukuliwa mateka, kwenda mataifa yote; nao Yerusalemi utakanyagwa na mataifa hatta majira ya mataifa yatakapotimia." Na tena (Mat. xxiii. 36), "Amin

Digitized by Google

amin, nawaambia, hayo yote yatawajia kizazi hiki." Hatta na Petro mtume aliwaonya maneno yenyewe ya Musa kama, "Bwana Muungu atawaletea nabii wa katika ndugu zenu kama mimi; msikieni killa atakavyowaambia. Itakuwa killa hayi asiyemsikia nabii yule, atapotezwa katika taifa" (Matend. iii. 21-23). Bassi ndivyo ilivyokuwa. Kwani mwaka A.D. 70, Warumi wakaja wakaharibu Yerusalemi kabisa kabisa. Wakauharibu hivi.

Yerusalemi ndio mji wa nguvu sana. Umejengwa juu ya kilima, kisichopandika pande tatu, kwa ginsi kilivyosimama, boonde chini na maboma ya mawe juu. Nazo boonde zaitwa, moja boonde ya Hinnom, yazunguka upande wa maghrebi na kusini, na boonde ya Yehosafat upande wa mashariki. Upande wa 'nne, ndio wa kaskazini, inchi sawa iliyopitika upesi. Bassi upande huo mji ulijengewa maboma matatu marefu ya mawe makubwa na mazito mno, killa boma lenyi ngome nyingi. Na kilima kile chenyi vilele viwili, na juu yake moja hekalu, na juu ya pili Sayuni, ndio mji wa juu wenyi jumba la mfalme, na katinakati ufa mkubwa na daraja ya kuvukia ufa. Bassi Yerusalemi ulikuwa kama miji minne mizima, killa mji wenyi boma lake. Mtu akilivunja boma la kwanza, ametwaa Bezetha, ndio mji wa nje; akilivunja la pili, ametwaa mji wa pili; bado miwili imesalia. Akilivunja la tatu, ndio amelitwaa hekalu; akiuvuka ufa akiingia katika Sayuni, mji wa juu, ndio mji wote umetwalika. Bassi Yerusalemi ndio mji wa nguvu sana.

Lakini watu waliokuwamo siku zile, hali zao mbaya mno. Hodari wenyewe kwa vita. Hapana watu wapitao Wayahudi kuwa hodari kwa vita na mashujaa, isipokuwa fitina nyingi mjini mle; hawapatani, hupigana tu wao kwa wao, wasiachane. Palikuwa na wakuu watatu, mmoja jina lake Eleazar,

Digitized by Google

naye akawa na watu kama elfu mbili na hamsi mia, akamiliki hekaluni mwa ndani; hawezi kutoka, akaa ndani hapo patakatifu, afanya vita juu ya wale wawili, ajilisha mwenyewe na asikari kwa vyakula na mali nyingi zilizowekwa hekaluni. Na mkuu wa pili, jina lake Yohanna, ana watu kama elfu sita, naye alimiliki nyuani mwa nje mwa hekalu. Naye kama amefungwa; hawezi kuingia ndani, kwani Eleazar yumo, wala kutoka nje, kwani yule wa tatu yuko; vita pande zote mbili. Akakaa akipigana tu. Na wa tatu ndiye Simon. Huyo akamiliki Sayuni, mji wa juu, mwenyi watu kama hamstashara elfu, akafanya vita juu yao wawili. Watu wa mji waliosalia, katika Bezetha na mji wa chini, waliharibika vibaya mno, wakiendewa killa siku na wale haramia waliotawala. Kote ni kuuawa tu, kuonewa, kutozwa mali, kunyanganywa, kuchinjwa burre. Hatta mtu akienda kusali hekaluni (kwani ruksa kwa wote kuingia humo kusali na kutoa thabihu), hatari sana; vita pote hatta katika patakatifu; mishale, mawe, mikuke haikomi.

Bassi mji wenyewe wa nguvu sana, hali ya watu mbaya mno; fitina tu na uthia mwingi; hawapatani illa kwa neno moja, wasishindwe na Warumi, kwani ndio waliowachukia machukio makuu. Wala hawakuangalia maonyo ya ishara zilizowatokea. Kwani tumehadithiwa ya kuwa nyota kubwa yenyi mkia kama upanga ikasimama juu ya mji ikashinda mwaka mzima. Tena katika siku kuu ya Vibanda watu wengi walipokutanika hekaluni, usiku wa manane nuru kubwa ikaangaza juu ya mathbahu na jumba takatifu kama mchana wa aththuuri, ikakaa nussu saa. Tena mlango mkuu wa shaba, mzito sana, shidda sana kuusindika hatta kwa watu asharini, nao upande wa mashariki wa hekaluni kwa ndani, ukafungwa sana kwa pingo za chuma zilizokazwa katika sakafu chini, kumbe mlango huu umefunguka peke

yake kama saa a sita usiku. Tena mshuko wa alasiri ilipokuchwa, magari ya vita na asikari wenyi selaha wakaonekana juu wakienda mbio huko na huko mawinguni, kama wakiizunguka miji wakiitwaa. Tena siku kuu ya Pentekote, wakohani walipoingia hekaluni mwa ndani usiku kufanya kazi ya ungoje mtakatifu wakaona tetemeko kuu, tena mshindo, tena makelele kama ya wingi wa watu wakisema, "Tuondoke twende zetu." Tena palikuwa mtu mkulima jina lake Isa bin Anano, naye akaja Yerusalemi, kabla haijaanza vita, kwa siku kuu; marra akapiga kelele, akilia "Sauti katika mashariki! sauti katika magharibi! sauti katika pepo 'nne! sauti juu ya Yerusalemi na jumba takatifu! sauti juu ya bwana arusi na bibi arusi! sauti juu ya watu hao wote pia!" Ndivyo alivyolia, akizunguka mchana na usiku mitaani mwa mji. Hatta watu wakamwonea hasira na uchungu, wakamkamata wakampiga bakora nyingi, asijitetee nafsi, wala kuwatukana, illa kufuliza kulia vile vile. Hatta wakubwa wakamchukua kwa liwali, akapigwa mijeledi hatta ngozi ikachubuka, mifupa ikawa wazi, asijiombee neno, wala kutoka machozi; killa achapwapo hulia kwa sauti ya huzuni mno, "Ole wake Yerusalemi!" Bassi liwali, jina lake Albino, akamwuliza, "U nani wee? watokapi?" hakujibu, hulia, "Ole wake Yerusalemi!"; hatta liwali akathani ana kichaa akamwondoa. Bassi akashinda miaka saba na miezi mitano, asichoke kulia vilevile killa siku, lakini kwa siku kuu akazidi; akaa peke yake, hakaribishwi na watu; akipigwa hulia, "Ole wake Yerusalemi!"; akipewa chakula hajibu ahsante yake illa hiyo hiyo, "Ole wake Yerusalemi!" Hatta vita ikaja akazunguka bomani na kilio chake, hatima akanena, "Ole wangu na mimi pia!" akapigwa kwa jiwe la Warumi akafa pale pale.

Digitized by Google

Bassi Kaisari akasikia habari kama Wayahudi wabaya na waasi, hawatulii, uthia tu na fitina pote. Akatuma mwana wake Tito kwenda kuwapiga. Tito akatoka Misri akaja Kaisariya, akafanya jeshi kubwa la vikosi vinne, killa kikosi chenyi watu kama elfu saba, akafunga safari akaenda Yerusalemi kwa njia ya Samaria. Wakafika karibu wakatua, mji ukawa kimya, mtu haonekani. Tito akataka kupeleleza mwenyewe, akatwaa asikari wa frasi mia sita akaenda karibu, haoni hatta mtu, akazunguka mji kidogo upande wa boonde ya Hinnom. Marra mlango ukafunguka, Wayahudi wengi wengi wakatokea gháfala nyuma yake, wakienda mbio, wakifukuza asikari, wakamkatizia kabisa njia ya kurudi. Tito akaona hatari, marra akakimbiza frasi akawarukia Wayahudi akiwakanyaga na kuwakata kwa upanga. Wakampigia mishale mingi na mikuke, naye hana selaha, wasimtie jeraha hatta moja; wakamshangilia ushujaa wake, wakamwachia nafasi akaokoka. Asitake tena kujitumainia sana, kwani Wayahudi wajanja sana, hufanya hila siku zote.

Hatta (April 14, A.D. 70) siku ya Pasaka, Tito akafanya matuo mahali patatu, moja katika Mlima wa Zeituni. Wayahudi wakaangalia, wakaona sharti wapatane wao kwa wao, wapate nguvu ya kuwashinda Warumi. Wakapatana siku ile. Marra wakatoka mjini wakawakuta Warumi kikosi kimoja kinatua boondeni pa Yehosafat. Wakawarukia Warumi kama wanyama wakali, mbio sana, Warumi wakastushwa wakasukumiwa nyuma mlimani pa Zeituni. Marra Tito akaletewa habari ya vita hiyo, akatwaa watu akaja mbio boondeni akawasimamisha Wayahudi akawaondosha. Halafu wakarudi tena wengi sana, wakiruka vilevile wakafukuza Warumi: Tito asikubali kwenda nyuma, akaachwa kama peke yake, pote Wayahudi wakimzunguka. Hatta Wa-

Digitized by Google

rumi wakaona haya kumwacha jemadari afanya vita peke yake, wakakusanyika tena, wakaja kwa nguvu wakawapiga Wayahudi, hatta wakawashinda. Wayahudi wakarudi zao mjini.

Ikawa siku ya Pasaka; hatta siku zile za shidda nyingi, Yerusalemi ukajaa watu waliokuja kuabudu; wangine wakaomba ruksa kuingia hekaluni kutoa thabihu, naye aliyemiliki hekaluni ndani ndiye Eleazar, na Yohanna avizia nyuani nje. Wakapewa ruksa. Walipokiingia, watu wa Yohanna wabaya sana wakajigeuza nguo wakafutika panga nguoni, wakaingia pamoja nao. Marra wakatupa nguo wakatoa panga, wakaanza kuwaua watu wa Eleazar; nao wakakimbia wakajificha mashimoni chini ya hekalu. Halafu wakarudi juu wakapatana na adui zao. Lakini wengi waliokuja kuabudu waliuawa burre palepale, wasiwe na hatiya.

Warumi wakakata miti, wakaharibu mashamba, wapate peupe pa kujongezea bomani mitambo na vyombo vya kulivunjia boma. Siku moja wakaona kundi la watu wakitoka mlangoni, wakitetemeka kama wakitupwa nje na wenzio wakihofu Warumi, wakitaka kurudi mjini wasiweze, na wenzio wa ndani kama wakiwapigia mawe juu ya ukuta. Warumi wakaajabu, wangine wakatwaa selaha wakaenda karibu mlangoni kuwakamata walio nje; kumbe Wayahudi wakatokea wengi wakiwazunguka pande zote, wakiwachoma na kukata na kutupia mishale, mawe, killa kitu, Warumi wengi waliuawa, wachache waliookoka; Wayahudi wakawacheka sana kwa kudanganywa vile, wakawatukana. Hatta na Tito akawakemea vikali, akisema, "Wayahudi walio waana wa kufa hutenda yote kwa akili, na shauri, na taratibu; nao Warumi walio washindaji hawajiwezi, huenda vitani pasipoamriwa." Akataka kuua wangine kwa athabu, wenzio wakawatetea, akawasamehe.

Digitized by Google

Bassi Warumi walipokwisha kufanyiza peupe na sawa mbele ya mji, walisogea karibu na boma la kwanza, wakajipanga hivi. Wa mbele asikari safu saba, tena wenyi mata, tena nyuma wenyi frasi safu tatu; wakaufunga mji upande wa kaskazini. Na boma hili. la kwanza lina nguvu sana, urefu wake mikono thelathini, na minara tissaini, na mawe yake makubwa yasiyovunjikana wala kubomoshwa. Bassi Tito akauzunguka mji kutafuta mahali pasipojengewa sana, akachagua pasipo boma refu sana; vita ikaanza kufanyika. Na desturi za Warumi katika kutwaa 'miji yenyi boma la nguvu ndizo hizi. Kwanza hufanyiza visugulu vya magogo na udongo karibu na boma; tena hujenga ngome kama majumba marefu ya mbau na chuma yenyi órofa nyingi, huzijongeza karibu na ukuta, na juu ya ngome hupandisha watu wenyi mata, nao hupiga mishale mengi katika juu, huondosha adui walio juu ya boma. Tena hufanyiza mitambo ya kutupia mikuke na mawe, yakwitwa balista na katapulti, yenyi nguvu za watu thelathini, yatupa mawe mbali sana kama mikono sita mia, yaua watu wengi thóruba moja. Tena hufanyiza kama banda lenyi mabati manene ya chuma hodari sana, asikari wengi huingia ndani humo, husogeza banda bomani kwa mitaimbo na magurudumu, nao wako chini ya mabati, hawapigikani na adui wala kwa mawe wala kwa mikuke; hutenda kazi kwa salamu, huvunja boma, hulibomosha kwa vyuma hatta kupenya ndani. Tena kuna kitu kimoja chatumika sana kwa vita zamani za kale, ndio kama gogo zito la mti limetiwa kipande cha chuma kikubwa nchani, latundikwa sawasawa kwa mnyororo juu ya boriti, lipate kuning'inia huko na huko. Bassi likiisha kuletwa karibu ya ukuta, watu wengi hulishika gogo upande wa nyuma, hulivuta mbali sana, marra huliacha, gogo larudi

Digitized by Google

zake kwa nguvu nyingi, laenda kwa shindo kuu, lagongagonga ukuta, likiyaponda mawe kwa ncha yenyi chuma. Hivi hufanyika marra nyingi, hatta ukuta kubomoshwa. Na kitu hiki chakwitwa, "kondoo ndume" (ram), kwani chatenda kazi kama kondoo akipiga pembe kwa nguvu. Bassi na siku ile Warumi walifanyiza visugulu, wakatengeneza ngome na mabanda, wakapiga balista na katapulti na makondoo pia; vita ikashikika kwa nguvu. Nao Wayahudi hupiga mitambo yao, hutupa mikuke yenyi moto ndio kuunguza vyombo vya adui, hutokea nje, hupigana vikali kama simba, wasiwakomeshe; makondoo yakigongagonga kwa mashindo makuu, hatta mnara mmoja wa boma ukaanguka. Marra Wayahudi wakajifanya kama wamechoka, Warumi wakalegea kidogo wakitenda shughuli zao; kumbe Wayahudi wakatoka nje wengi kama nyuki, wakileta vinga vya moto, wakawafukuza walinzi, wakachoma mitambo na vyombo vya vita. Tito mwenyewe akaja na asikari wa frasi akaua watu thenashara peke yake, akakimbiza Wayahudi, akatwaa mmoja mzima akamsulubisha palepale. Wote wakalala usiku, kimya kote na giza na usingizi; ikawa shindo kuu, inchi ikatetemeka, kama mlima ukianguka, wote wakastushwa mno, wakashika selaha, wakangojea adui. Lakini adui hapana, kimya vile vile. Akaja Tito, wakasikia habari ya kuwa ngome moja ya juu ya kisugulu, kwenda juu kwake kama mikono settini, imeanguka peke yake. Wakatulia tena. Assubui wakashika vita kama kwanza, makondoo yakigongagonga tu sikuzote, hatta boma likabomoka kidogo; Wayahudi wakachoka, wakakimbilia boma la pili. Warumi wakaingia Bezetha, wakavunja boma lote la kwanza.

Walipokwisha, waliendea boma la pili. Na hapo pia vita ikawa kali sana, hatta usiku hakuna raha,

Digitized by Google

wakikesha wakiviziana. Marra kwa marra Wayahudi hutokea nje kupigana. Hatta siku moja walipotokea pale, mtu Mrumi, jina lake Longino, akafanya kiume sana, akawarukia Wayahudi wengi peke yake, akachoma mtu mmoja kinwa kwa mkuke, akamua, akautoa mkuke, akamua mwingine kwa mkuke ule ule, akarudi kwao salamu. Tena Wayahudi wakafanya hila. Ngome moja bomani ikianza kuvunjika na makondoo, waliondoka wote illa mtu jina lake Kastor, na wenziwe kumi. Nao wakakaa wakaonekana juu ya ngome kama wakigombana sana wao kwa wao. Kastor akimwita Tito akitaka kujitoa, wangine wakikataa. Wakagombana sana, kama wakiuana, hatta Tito akaamuru vita inyamaze kidogo, akataka kusikia maneno yao. Akamwambia Yosefo kwenda karibu, asikubali, akisema, "Hila hiyo." Bassi mtu jina lake Ainea akasema, "Mimi ntakwenda." Akaendelea bomani chini, Kastor akamwambia, "Haya, daka fetha," akamtupia jiwe kubwa katika juu, lisimfikie, kwani alikinga, likamumiza asikari aliye karibu yake. Tito akaghathabika sana, akiona amedanganywa, akaishika vita kwa bidii sana. Hatta Kastor mwenyewe na watu wake walichoma moto ngome yao, wakajifanya wakiruka motoni, kumbe wamerukia shimoni tu la kupenyezea ndani ya mji. Siku ya tano Wayahudi wakashindwa, wakakimbilia boma la tatu, Tito akamiliki mji wa chini. Akataka kupatanisha watu waliomo, akatangaza killa mtu asiye asikari arudishiwe mali zake. Bassi Wayahudi walio asikari wakasema, "Mwoga huyo," hawakubali mtu apatane na Tito; huchinja waliotaka amani wote, huzidi kufanya ushujaa; vita kali ikaanza tena palepale, wakaua Warumi wengi. Kwani Warumi hawajui kwa kwenda, Wayahudi wapajua pote, huwanyemelea adui, hutokea gháfala, huwapiga thóruba moja.

Digitized by Google

Hatta Warumi walifathaika; akaja Tito akawasimamisha kidogo, asiweze kuwazuia Wayahudi; akatokea na watu wake nje ya boma, wakawa kama hawajalitwaa kabisa. Wakapigana sana siku tatu, wakalitwaa marra ya pili, wakalivunja pia.

Lakini boma la tatu bado limesalia, nalo kubwa sana, lenyi ngome nyingi, na zilizo kubwa ndio Antonia upande wa hekalu, na Mariamne, na Faselo, na Hippiko. Kwani ngome hizo kama majumba marefu sana ya mikono kama themanini, yaliyojengwa na mfalme Herode; zikapambwa sana ndani kama nyumba za kifalme, zenyi vyumba vingi na birika za maji, na behewa, na bustani. Bassi Tito akaona shidda kuzitwaa, akapumzisha jeshi lake muda wa siku 'nne akafanya siku kuu, asikari wote wakajipamba vizuri na selaha na frasi, wakacheza mbele yake; wakapewa killa mtu mshahara wake wa mwezi. Na Wayahudi wote wakatazamisha Warumi wakicheza vizuri vizuri mbele ya Kaisari. Walipokwisha, wakafanya vita tena.

Kwanza Tito akamtuma Yosefo (Josephus) kwenda karibu na kutoa maneno kwa Wayahudi ya kuwashawishi wajitoe wenyewe na mji pia. Akatoa maneno mengi mazuri, ikawa fitina mjini. Kwani asikari wa Eleazar, na Yohanna, na Simon, walio watu wa vita, hawakukubali maneno yake, wakamtukana sana wakampigia mawe na mishale. Wangine wakataka sana kujitoa kwa Warumi. Bassi je? hawana buddi. Njaa inazidi, yauma sana; tena waonewa mno na wale asikari. Bassi wakipata nafasi wengi walitoroka, wangine wakauza mali zote, wangine wakameza thahabu na johari, wakakimbia kwa Warumi, halafu wakazipata tena chooni. Marra asikari wakawazuia wangine wakawachinja palepale, walio wenyi mali. Tena wakaenda nyumba kwa nyumba hunyang'anya chakula, wakivunja mi-

Digitized by Google

lango, wakikuta watu ndani wanakula huwasonga, hatta na kutoza kanwani makombo wanayomeza. Nao wasionyang'anywa na asikari, hunyang'anyana wao kwa wao; kwani njaa ikawageuza kuwa kama wanyama; hatta mke amwibia mumewe, na mtoto mamaye, na mama mwanawe, hatta kwa maziwa ya matiti. Wangine masikini hutoka nje ya boma usiku, hutafuta boga na majani, wakirudi hutwaliwa vitu na asikari, wasiorudi hukamatwa na Warumi; wakasulubishwa wengi wengi, hatta hamsi mia kwa marra moja, hatta haikutosha misalaba wala nafasi ya kuwasulubishia. Hivyo Tito alitaka kuwatia hofu Wayahudi, wasidumu kupigana. Lakini haifai. Walikata tamaa tu, wakisema, "Tukijitoa, tusijitoe, mamoja; tufe tu."

Bassi Warumi wakatenda kazi kwa bidii siku sabatashara; hatta May 27, ndio visugulu vinne vikamalizika, wakapandisha mitambo na vyombo vya vita juu, wakataka kuendea boma; kumbe inchi ikatikisika ikachafuka kama bahari, ikatoka moshi mzito, na ndimi za moto, marra na visugulu vyenyewe na minara na mitambo yote ikatumbukia shimoni mwa moto ikaangamia. Na maana yake, Yohanna amefukuafukua chini, akaweka lami, kiberiti, hatari nyingi chini, akatia moto. Hivyo kazi nyingi za Warumi imekuwa burre. Wasilegee lakini. Baada ya siku mbili wakaanza kugongagonga boma. Wayahudi watatu walio mashujaa mno ajabu wakatoka nje wakachoma moto mitambo na makondoo. Warumi wengi wakaja, wasiweze kuwashinda. Moto ukazidi, Wayahudi wakatokea wakawarukia walinzi wakawaua wakifukuza Warumi, wakifanya ukali sana hatta karibu kuwashinda. Mwisho Tito akasikia habari akaja mwenyewe na jeshi, akapigana sana; hatta Wayahudi wakarudi mjini. Halafu akafanya baraza ya majemadari, akawatolea shauri

Digitized by Google

hivi, "Kazi zetu zote zimeharibika burre; haifai kuzitengeneza tena. Tujenge boma na sisi kuzunguka mji pande zote. Watu watashindishwa kwa njaa, watajitoa." Marra wote wakajenga boma la maili tano, ndio urefu wake, la kuuzunguka mji wote; likafanyika upesi upesi kwa siku tatu, kwa ginsi walivyotenda kazi kwa bidii nyingi. Marra njaa ikazidi mjini, ikawa mbaya mno. Nyumba zikajaa wazee, na waanake, na watoto, wakifa wasilie wasizikwe. Bassi ye? hapana mzishi; wakakaza macho kwa hekalu; kimya pote, illa waharamia wakivunja nyumba, wakinyang'anya nguo hatta za mayiti, na kuzichoma kwa upanga, ndio mchezo wao. Mayiti zikaoza, nazo nyingi sana, na herufu mbaya mno; hatta zikatupwa nje ya boma, boonde zikajaa damu, na mifupa, na taka za mayiti zikioza pale wazi. Wengi wakataka kutoroka, na kuutoa mji. Marra Simon akajua hila yao, akawafisha wengi; wangine wakawakimbilia Warumi wakapewa chakula; wakala mno kwa sababu njaa, wakafa. Wangine wakaonwa watafuta thahabu na johari katika mavi yao wenyewe; marra Waarabu na Washami walio pamoja na Warumi wakasema, "Labuda wengi wamemeza thahabu yao," wakaua watu kama elfu mbili, wakayatumbua matumbo waipate thahabu. Asikubali Tito uovu huo mkuu akamshuhudisha Muungu, kama siye aliyefanya; akataka kuwaua wale wauaji. Njaa ikazidi sana mjini, watu wakala hatta vilivyowekwa wakf na vilivyo vitakatifu; wakapekua jaani na samadini; pishi ya ngano ikapata reale themanini ao mia. Hatta kwa miezi miwili u nussu, mayiti zilizotupwa na kuzikwa kwa jumla, zapata zayidi ya mia elfu.

Warumi wakashika vita tena. Kwanza wakafanyiza ngome za miti na vyombo vya miti; lakini miti hapana, yote imetumikiwa mbali; bassi waka-

Digitized by Google

enda kuitafuta mwendo wa nuss u siku (maili kumi), ndipo wakaipata wakaileta kwa shidda sana. Wakakaribia boma penyi ngome iliyokwitwa Antonia, wakipigiwa mawe mengi na mishale, wakatoa majiwe manne, wakapumzika. Halafu usiku boma likabomoka kidogo, Warumi wakasema, "Kesho tutalitwaa." Walipoamka assubui kumbe boma lingine limejengwa ndani na Wayahudi palepale. Tito akawasukuma sana asikari wake kuliendea, wasithubutu. Hatta paliondokea mtu jina lake Sabrino, Mshami, naye mfupi na mwembamba, lakini moyo wake mgumu sana, akasema, "Mimi hapa tayari kujitoa kwa ajili yako, ee Kaisari." Akatwaa ngao na upanga akaenda saa a aththuuri, watu edashara wakamfuata nyuma. Akapanda juu ya boma, kwani Wayahudi hawakuweza kumzuia. Walijaribia ginsi zote, wakimfingirishia mawe, wakimtupia mishale isiyohesabika, wasimshinde. Hatta alipofika juu, alijikwaa jiweni akaanguka, marra Wayahudi wakamrukia tena vikali wakimchomachoma; akaondoka magoteni akawapinga awezavyo akitoka damu kwa jeraha hatta akachoka, akafunikizwa pia na mikuke akafa. Baada ya siku mbili Warumi kumi na tano wakaenda usiku, wakapanda juu ya boma wakawaua walinzi wakapiga paanda sana wakaingia ngomeni Antonia. Marra Tito akaja na jeshi akawasayidia wakaitwaa ngome, wakataka kulitwaa na hekalu, kwani karibu. Vita ikawa gumu sana, Warumi na Wayahudi wakachanganyika pamoja katika pembamba wakikanyagana wakichapana kwa panga, wakisonganasongana, pasipo taratibu; hatta Wayahudi wakashinda, Warumi wakarudi ngomeni Antonia wakakaa. Illa, mtu mmoja wa upande wa Warumi hakukubali kushindwa; jina lake Juliano. Naye akawarukia Wayahudi akawatawanya, akapenya ndani ya hekalu peke yake, wenziwe katika ngome

Digitized by Google

Antonia wakamtazamisha kwa ushangao, alivyofanya vita peke yake na kuua watu wengi naye mmoja tu. Hatta akateleza akaanguka, kwani amevaa viatu vyenyi misomari ya chuma chini, ikateleza juu ya sakafu ya mawe laini sana hekaluni. Marra Wayahudi wakaja tena wakamzunguka wengi wengi, naye akajifunika kwa ngao akawachoma akilala kwa upanga, wasiweze kumchoma yeye, kwani amevaa chuma mwilini mwote. Lakini afanyeje? mtu mmoja tu, nao adui wengi, wakamkata vipande vipande, akafa. Wakamchukua.

Tangu hapo Wayahudi wakapunguka; hawana mtu wa kutoa thabihu za subuhi na jioni hekaluni. Tito akasikia habari, akamtuma Yosefo (Josephus) kushuhudia marra ya pili, akasema nao maneno mengi, watoke nje kupigana, wala wasiharibu ibada ya hekaluni. Asiweze kuwashawishi. Bassi Tito akaamuru kuvunja kabisa boma penyi ngome Antonia, na kufanya njia pana, na peupe mbele ya hekalu, asikari wengi wapate kukaribia na kuleta vyombo vya vita. Kwani pembamba kwanza, wala nafasi hapana. Walipokwisha, akachagua watu hodari akawatuma usiku kuliendea hekalu; naye mwenyewe akaketi juu ya ngome kutazama nani aliyepigana vema, na waoga pia. Kwa sababu hiyo vita ikawa kali sana. Kwanza usiku walipigana, wasitambulikane vema mtu na mwenziwe kwa giza, Warumi wakasogeana wakafanya makundi, Wayahudi wakatawanyika wakapigana mmoja mmoja; hatta wengi waliouawa na wenzio kwa maana giza. Weupe ukapanda, wakashika vita vile vile hatta saa a tano, wasiendelee hatta thiraa mmoja wale hao wala hao, kwenda mbele ama nyuma. Wote wakarudi kwao.

Palikuwa na vita nje ya mji, kwani Wayahudi walikwendea adui boondeni mwa Yehosafat kwa

Digitized by Google

ghâfala, wasidiriki. Wakakimbia. Mrumi mmoja jina lake Pedanio, akakimbiza frasi wake, akampatia Myahudi akikimbia, akainama akamshika akamchukua kwa nguvu zake nyingi juu ya frasi akamletea Kaisari.

Halafu Wayahudi wakafanya hila. Hekalu limezungukwa na matao, na juu ya matao mvungu na dari. Bassi wakajaza mvunguni mle chini ya dari majani mengi, kuni, fito, mafuta, lami, killa kitu cha kuchochelea moto, wakaondoka wenyewe. Marra Warumi wakaona wameondoka wasijue hila yao, wengi wakapanda darini kwa ngazi wakataka kulitwaa hekalu. Walipokwisha kujaa juu Warumi wengi, ndipo Wayahudi waliwasha moto, moto ukazidi sana, kukawa mashaka makuu. Warumi wangine wakaruka nje wakavunjika mifupa, wangine wakaruka ndani hekaluni, wakauawa na adui, wangine wakajichoma wenyewe kwa upanga, wengi wakazungukwa na moto wakaungua palepale mbele ya macho ya wenzio na Kaisari pia. Palikuwa na kijana Mrumi jina lake Longino, shujaa sana, yuko motoni juu ya dari; hatta Wayahudi wakamshangaa, wakamlilia, "Shuka hapa kwetu, utaokoka." Lakini ndugu yake Mrumi alimshurutisha akinena, "Ndio aibu sana, kujitoa. Bora kufa." Hatta yule kijana akatwaa upanga, akajichoma pale pale wazi, akafa. Palikuwa na mwingine, jina lake Artorio, amekamatwa na moto juu huko darini, akamwita Mrumi mwenziwe kwa sauti kuu, akisema, "Mimi naruka chini, nakurithisha mali yote niliyo nayo, ukinidaka tu." Akaja mbio kumdaka. Yule akaruka akaanguka juu yake mwenziwe kwa mshindo, akamponda akafa, mwenyewe akaokoka.

Siku zile njaa ikazidi ikauma mno. Watu wakala ngozi, na majani, na taka. Palikuwa na mwanamke, jina lake Maryamu, binti Eleazar, anakaa mjini,

Digitized by Google

naye kazi yake hutafuta cho chote cha kula, huleta kwake; marra asikari na Warumi huingia humnyang'anya kile kidogo, huchukua. Yule mke hufanya uchungu, huwatukana, wasipende kumulia mbali lakini. Hatta njaa ikamchoma ndani kwa maumivu mabaya mno. Akawa na mtoto mchanga, àkamtwaa, akamua, akampika, akamla nussu, nussu akaiweka. Manuko ya kilichopikwa yakaenea nje ; marra haramia wakaja wakavunja mlango, wakamtoza kwa jeuri kile chakula. Akawaambia, "Hatta mimi nimewawekea nussu." Akafunua baki la mtoto. Wakastuka wakakaa kimya ; akasema, "Haya bassi, mle nanyi; mimi nimekula; ninyi wenyi shauko kuliko mama? msipotaka, niachie." Wakaenda zao kwa hofu na tetemeko.

Na namna ya hekalu ya siku zile ndiyo hii. Limesimama juu ya kilima; na kilima kile kimejengewa kuta mbavuni tangu chini boondeni hatta juu, kuta ndefu sana za mikono mia tatu, ndio urefu wao. Illa upande wa kaskazini ukuta si mrefu mno, wenyi nguvu lakini na ngome kubwa Antonia. Na hekalu lenyewe, ndilo kwanza uwanja mkubwa nje, nao mrabba, wenyi ukuta nje na matao na nguzo za mawe meupe mazuri mno ya mikono asharini na tano, na milango kenda na sakafu ya marmar laini sana. Ukiingia ndani ya uwanja, marra waona jengo kubwa limesimama katikati, kuta zake za mikono kama hamsini, na milango kumi iliyofunikwa na thahabu na fetha, na madaraja ya kupandia milangoni; na mlango mmoja, ulioitwa Mzuri, wa shaba safi wote wa mikono hamsini; na ndani ya milango uwanja wa pili, wenyi mathbahu kubwa ya shaba; na upande wa magharibi ndipo Patakatifu, penyi ukumbi wa mikono themanini urefu wake, na mlango mkubwa wa thahabu, na juu ya mlango mzabibu umefanyizwa kwa thahabu tupu; shina lake, na matawi yake,

Digitized by Google

na matunda yake, yote thahabu. Na ndani ya Patakatifu kinara cha meshmaa chenyi matawi saba, cha thahabu; na meza ya thahabu yenyi mikate ya wonyesho; na mathbahu ya kuvukizia uvumba. Na zege iliyo juu yake nyeupe kama mlima uliofunikwa na theluji, imetiwa pote mismari ya thahabu. Bassi ndiyo namna yake hekalu na patakatifu penyewe.

Bassi tuwarudie Warumi. Moto ule ulipokwisha kuteketeza matao ya nje na dari, Warumi waliingia katika uwanja wa kwanza, wakaleta tena makondoo na mitambo, wakashika kugonga kuta za uwanja wa pili. Wasiweze, kwani majiwe makubwa mno. Hayavunjiki wala hayaondoleki. Wakaleta ngazi wakapanda, wakafika juu; marra hutupwa chini na Wayahudi, watu na ngazi pia. Hatta Tito akasema, "Leteni moto, mkachome milango." Wakachoma, thahabu na fetha ikayeyuka, mbau zikaungua, moto ukala usiku na mchana. Wayahudi wakashangaa wakanyamaza. Halafu wakatoka nje kwa mlango wa mashariki wengi wengi wakawarukia Warumi, wasiwashinde wakarudi ndani. Tito akafanya baraza, akawashauri maakida yake, "Tufanyeje? tuliharibu kabisa jumba hilo kubwa na zuri, ajabu la ulimwengu, ama tulilinde zima?" Wangine wakasema hivi, na wangine hivi. Tito akaamuru kuuzuia moto, akaingia ngomeni Antonia, akasema, "Kesho ntalitwaa kwa nguvu." Siku ile ndiyo Aug. 10, ile ile Nebukadnezar aliyoliharibia hekalu la Sulemani. Ikawa jioni, Tito akaenda kulala. Marra lio kubwa, mtu akaja mbio akinena, "Moto! moto! hekalu linateketea." Ndivyo ilivyokuwa. Warumi walikuwa kwanza wakiuzuia moto, wakaja Wayahudi wakapigana. Marra Warumi waliwafukuza hatta mlangoni pa patakatifu. Mmoja akapanda juu ya bega la mwenziwe akatupa kinga la moto ndani, moto ukawaka ukaanza kula. Wayahudi wakapiga

Digitized by Google

kelele kuu, wakashika vita tena. Tito akaja akaamuru wazuie moto, Warumi wasimsikie hatta kidogo; huenda mbio, huruka, hukanyagana, huitana kwa vita, hutupa vinga, huchinja watu waliomo, asikari, masikini, waanake, watoto,—wafu chungu chungu, damu pote kama mito. Tito akaingia patakatifu pa ndani, akatazamisha uzuri wake kwa ushangao, akatamani sana kupalinda. Hakupata. Asikari wakaja, kama wanyama, kama wenyi wazimo, wakauchoma mlango; moto ukala, bassi. Ungaliona mlima wote, kama mlima wa moto, unang'aa, unatoka moshi, mashindo ya majengo yakianguka, ndimi za moto zikiruka mawinguni, vilio na makelele ya watu wakichinja, wakichinjwa, wakiungua kwa moto, wakifa kwa njaa, wakijiua. Mwisho kimya. Warumi wakaja majeshi majeshi wakatua palepale palipo hekalu, wakampigia Kaisari vigelegele vingi vya shangwi na furaha, wakagawanya mateka.

Lakini Yerusalemi haijatwaliwa bado yote. Kumesalia mji wa juu, ndio Sayuni, umesimama juu ya kilima chake, karibu na hekalu, na ufa mkubwa katinakati, na daraja ya kuvuka toka hekalu hatta Sayuni. Nao Sayuni wenyi boma kubwa pande zote na ngome tatu zilizo ajabu kwa urefu na upana na uzuri wa ndani; na jumba la mfalme limo. Na Simon na Yohanna walikimbilia Sayuni na asikari wao; bassi Warumi hawana buddi kushika vita tena hatta kuutwaa mji wa juu. Kwanza Tito akasimama penyi daraja, akatoa maneno ya kuwashawishi wajitoe. Wasikubali, akasema, "Vema. Mtauawa wote pia." Tena akaamuru asikari wafanye visugulu vile vile, na kuvunja boma la Sayuni. Wakaenda kutafuta miti; shidda sana kupata, yote imekatika kwa matumio ya vita; sharti kwenda maili thenashara, ndipo yakapatikana. Wayahudi

Digitized by Google

wengi wakakimbilia Warumi; wangine wakataka, hawakudiriki, wakauawa kwanza na asikari wa Simon na Yohanna. Mkohani mmoja akamtolea Tito vyombo vitakatifu vya hekaluni, vilivyofichwa chini mashimoni, kinara cha meshmaa chenyi matawi saba, na meza ya thahabu, na vyuo vya torati. Na waliojitoa wakaachiwa maisha, wakauzwa utumwani. Bassi kwa siku kumi na nane visugulu vikafanyizwa, boma likaanza kugongwa na makondoo chini, katapulti na balista zikafanya kazi juu kutupa mawe na mikuke na mishale ya moto. Bassi mahali pamoja boma likavunjika kidogo, minara ikaanguka. Marra Wayahudi wakapotelewa na moyo wakafathaika, wakakimbia. Hatta Yohanna na Simon wakapiga mbio nje kuendea boma la Warumi na kuokoka. Wasidiriki kupenya, wakafukuzwa nyuma mjini, wakatawanyika na asikari, wengi wakaingia mashimoni; kwani mashimo mengi sana katika Yerusalemi, mji wote umechimbuliwa na kufukuliwa chini; wengi wakakamatwa. Nao Warumi kazi yao kuchinja tu, na kuchoma moto pote, moto na damu zikashindana, hatta pana mahali damu ikazimisha moto. Hatta wakaisha. Tito akaingia Sayuni, akashangaa sana kwa maboma na ngome kuwa za nguvu sana, akaamuru zivunjwe kabisa kabisa, illa ngome tatu zilizo kubwa zikasazwa kuwa kumbusho la vita. Warumi wakapenya mashimoni wakaona mali nyingi mno ajabu. Na hesabu yao waliouawa elfu elfu na mia elfu. Na waliokamatwa elfu tissaini na saba. Wazee wakachinjwa, walio wazuri na wanene wakachukuliwa Rumi; waliobaki huchukuliwa Misri kwa kazi ngumu za kuchimba mawe, na ya kupigana katika amfiteatro kwa mchezo. Hatta na yule Yohanna alitafutwa sana, asipatikane; akajitoa akaachiwa maisha. Lakini Simon akaingia shimoni, akakaa siku nyingi,



Digitized by Google

Tito akaenda zake. Halafu njaa ikamshika Simon, akavalia vizuri, akatokea kwa gháfala katika shimo, kama kivuli. Warumi wakastushwa, halafu wakajirudia, wakamshika; Tito akasikia habari akaamuru apelekwe Rumi.

Naye Tito akaenda Rumi, akafanya siku kuu ya furaha na shangwi kwa vita zake zote, vitu vitakatifu vya Yerusalemi vikatembezwa wazi mbele ya watu wote na sanamu ya mji ulivyowekwa na kuvunjika, na Wayahudi wengi wafungwa na mateka wakatembezwa; mwisho na Simon akachinjwa, kwani ndiye mkuu wa adui wao Warumi.

Bassi ndio habari ya kuharibika Yerusalemi, Wayahudi wote waliosalia wakatawanyika, wakakaa katika miji ya mataifa mangine mangine wasichanganyike nao wala kusharikiana, hukaa mbali peke yao kwa hali nyonge na ya kutharauliwa; lakini wangine wamejipatia utajiri mwingi mno. Baada ya siku nyingi twaona Muungu atawaonea rehema na kuwarudisha mjini kwao. Tena katika mji Rumi kuna tao kubwa lililojengwa na Tito kuwa ukumbukumbu wa vita hizo; liko hatta leo, lenyi kazi nyingi ya nakshì na sanamu ya shangwi ya siku kuu ile, na vyombo vitakatifu ndio kinara cha meshmaa chenyi matawi saba, na meza ya thahabu, na vyuo vya Torati vilivyotembezwa mbele ya watu wa Rumi.

MWISHO.

Digitized by Google

Richard Clay & Sons, Limited,
London & Bungay.

Digitized by Google